Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA PILI

### Kikao cha Nne – Tarehe 11 Februari, 2011

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

### HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA A. SILIMA)**:

Tamko la Sera ya Fedha, Mapitio ya Nusu Mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania Februari, 2011 *(Monitary Policy Statement of Bank of Tanzania, The Midterm Review, February 2011).*

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 37

**Ujenzi wa Machinjio ya Kisasa Kwenye Mikoa ya Wafugaji**

**MHE. FREEMAN A. MBOWE (K.n.y. MHE. ROSE K. SUKUM)** aliuliza:-

Ni ukweli usiopingika kuwa mifugo ni rasilimali kubwa kwa nchi hii; Mkoa wa Manyara ni miongoni mwa mikoa yenye rasilimali kubwa ya mifugo kwa kuwa na ng'ombe 1,263,436, kondoo 262,456, mbuzi 1,085,552 na mifugo mingine kama kuku, nguruwe, bata na kadhalika, ambapo idadi hiyo ni sawa na ng'ombe asilimia saba na mbuzi asilimia nane ya mifugo hapa nchini:-

(a) Je, kwa nini Serikali imeshindwa kujenga machinjio ya kisasa kwenye mikoa hii yenye mifugo mingi kama ilivyo Mkoa wa Manyara hususan Wilaya ya Hanang ambayo takriban asilimia 80 ya wakazi wake ni wafugaji?

(b) Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kuwaendeleza wafugaji kwa kuwapa mbinu mbalimbali za uzalishaji na usindikaji wa mazao ya mifugo kama vile maziwa na ngozi; ujuzi ambao hawana kwa kipindi hiki?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Kamil Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa, Serikali ikishirikiana na Taasisi mbalimbali pamoja na Sekta Binafsi chini ya Mpango wa *Private Public Partnership (PPP)*, imekuwa ikihamasisha na kuchangia ujenzi wa machinjio za kisasa nchini. Mifano ya jitihada hizi ni pamoja na ujenzi wa machinjio ya Sakina Mkoani Arusha, yenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 300 na mbuzi 400 kwa siku; Dodoma Mkoani Dodoma yenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 200 na mbuzi 150; Ruvu Mkoani Pwani ambayo itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 800 na mbuzi 400 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukarabati wa machinjio katika Mamlaka za Serikali za Mitaa unafanywa na Serikali kupitia mipango mbalimbali ikiwa ni pamoja na *DADPs* na Mfuko wa Kuendeleza Zao la Ngozi. Kwa mfano, machinjio ya Wilaya ya Hanang, katika mwaka 2006/2007, yalikarabatiwa kwa shilingi milioni kumi toka *DADPs* na kwa mwaka 2008/2009 hadi 2010/2011, yalikarabatiwa kwa shilingi milioni 18.46 kutoka Mfuko wa Kuendeleza Zao la Ngozi. Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, pamoja na Sekta Binafsi, inaendelea kutafuta fedha ili kujenga machinjio ya kisasa kama ilivyofanyika katika Halmashauri jirani ya Simanjiro, ambayo chini ya utaratibu wa *Private Public Partnership (PPP)*, inajenga machinjio ya kisasa huko Naberera, itakayokuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 40 na mbuzi/kondo 40 kwa siku.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *DADPs*, inatoa mafunzo ya uzalishaji na usindikaji wa mazao ya mifugo kwa wakulima na wafugaji huko huko vijijini na katika Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo vya Tengeru (Arusha), Morogoro (Morogoro), Mpwapwa(Dodoma), Madaba (Ruvuma), Mabuki (Mwanza), Kikurura (Kagera) na Buhuri (Tanga). Katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, jumla ya wafugaji 346 kutoka Hanang walipatiwa mafunzo ya ufugaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa, nguruwe na kilimo hai. Aidha, Wilaya ya Hanang ilipatiwa jumla ya shilingi milioni 26.3 kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kuboresha zao la ngozi na usindikaji wake. Katika mwaka 2010/2011, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, imetenga jumla ya shilingi milioni 64 kupitia *DADPs* kwa ajili ya kutoa mafunzo ya uzalishaji na usindikaji wa mazao ya mifugo kwa wafugaji hususan mazao ya maziwa na ngozi.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa wafugaji wa Mkoa wa Manyara pamoja na kwamba wamesema kuwa kutakuwa na machinjio ya kisasa, ni vyema kuwa na soko ambalo litakuwa linasaidia Wanamanyara kwa sababu ni wafugaji wakubwa; na pia wawekewe sekondari au upili kwa maana ya kwamba soko hilo litawasaidia wafugaji wadogo wadogo kwenda kuuza mazao yao ya mifugo karibu na kuweza kupima mazao hayo kwa kilo badala ya kuuza kwa kukadiria tu. Muda mwingine unakuta ng'ombe ana kilo mia mbili lakini huuzwa kwa shilingi laki tano au laki tatu. Kwa hiyo, naomba Serikali iweke upili kwenye Mkoa wa Manyara ili Wanahanang pamoja na Wanamanyara wote wauze mazao yao kwa faida badala ya kupeleka Dodoma au Arusha au Dar es Salaam.

(ii) Kwa kuwa akina mama ndiyo wanaotunza mifugo hiyo basi ninapendekeza waelekezwe kupata masomo ili waweze kuboresha mifugo hiyo na waweze kupata fursa ya wao kuweza kujiendeleza kupata faida kwa mifugo hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, masoko hasa haya ya upili yanahitajika na kwa Kanda ya Kaskazini kuna mawili au matatu; moja lipo Meserani Wilayani Monduli; na lingine lipo Themi Wilayani Arumeru na pia lingine lipo Weruweru Moshi Vijijini. Nakubaliana na ushauri alioutoa, lakini masoko kama Sera inavyosema; ni jukumu la Halmashauri husika ama Mkoa husika kujipanga na katika vikao halali kupendekeza kwamba ni masoko yepi yanapaswa kuwekwa.

Ninamuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, maadam na mimi ni mdau, maana natoka kwenye Mkoa huo, waweke mapendekezo kwenye Halmashauri na Mkoa ili uwezekano huo uwepo wa kujenga masoko hayo ya mifugo ambayo ni *secondary*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili; nakubaliana pia na ushauri maana ilikuwa ni ushauri badala ya pendekezo. Kama nilivyosema, chini ya utaratibu wa *D by D*, mipango yote inaibuliwa kutoka chini na kujadiliwa na Halmashauri na hivyo maadam Mheshimiwa aliyeuliza swali ni Mbunge na anaketi katika vikao halali vya Halmashauri, yeye atoe mapendekezo hayo na yakiungwa mkono, Kiwizara tutatoa *support* inayotakiwa ili hilo pia liweze kufanyika.

Na. 38

**Ujenzi wa Barabara ya Lami Toka Kyaka-Kasulo (BENACO)**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais alipokuwa Mji Mdogo wa Nyakaiga Wilayani Karagwe aliahidi kuwa barabara kutoka Kyaka – Bugene – Kasulo (Benaco) itajengwa kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza na kukamilika?

(b) Je, ni lini upembuzi yakinifu utaanza na kukamilika ili ujenzi wa Barabara ya Bugene hadi Kasulo (BENACO) utaanza na kukamilika?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami Barabara ya Kyaka-Bugene, yenye urefu wa kilomita 59.1, ulisainiwa tarehe 30 Julai, 2010 kwa gharama ya shilingi bilioni 64.96. Muda wa utekelezaji wa Mradi ni miezi 27 na kazi zimepangwa kukamilika mwezi Oktoba, 2012. Kwa sasa mkandarasi yuko kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi.

(b) Katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, kiasi cha shilingi milioni 620 kimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Bugene – Kasulo, yenye urefu wa kilomita 121. Mchakato wa kumpata mhandisi mshauri wa kufanya kazi hii unaendelea. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2011. Aidha, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Bugene – Kasulo zitaanza baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina na fedha za ujenzi kupatikana.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri sana na yenye faraja kwa Watu wa Karagwe, lakini nilitaka kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwanza, ninajua kwamba barabara hiyo itapitia makazi ya wananchi ambako itabidi kubomoa nyumba za wananchi pamoja na mali zao; sasa nilitaka nijue je, Serikali imejiandaa kiasi gani kutoa fidia halali kwa Wananchi wa Jimbo la Karagwe?

(b) Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kutoa ahadi nzuri ya kwamba fedha zikipatikana kipande cha Barabara ya Bugene mpaka BENACO - Kasulo itajengwa; je, MheshimiwaWaziri uko tayari kuwapa matumaini Wananchi wa Jimbo la Karagwe kwamba bajeti ijayo ya 2011/2012 fedha hizi zitatengwa?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika**,** napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba, katika sehemu ya Kiaka hadi Bugene, yenye jumla la kilomita 59.1, mkandarasi amekwishateuliwa na kwa sasa hivi anafanya *mobilisation* na gharama za ujenzi huo ni zaidi ya shilingi bilioni 69.96.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la fidia na bahati nzuri Mheshimiwa Blandes ni Mwanasheria, tunazingatia sheria na hapa tutazingatia Sheria Namba 13 ya Mwaka 2007, wale ambao wako nje ya *road reserve* watalipwa fidia na wale ambao wako ndani ya *road reserve* waanzae kubomoa leo.

Kuhusu swali la pili ni kwa namna gani tumejiandaa katika sehemu iliyobaki ya kutoka Bugene hadi Kasulo, yenye jumla ya kilometa 121; kazi zimekwishaanza kwa kumtafuta *consultant* na mtu wa kufanya upempuzi yakinifu pamoja na usanifu. Jumla ya shilingi milioni 620 zimetengwa katika bajeti ya mwaka huu, atakapopatikana *consultant* na kufanya *design.* Tutafanya maandalizi ya kuandaa *tender* kwa ajili ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya kujenga sehemu hiyo iliyopangwa. Vilevile katika sehemu hiyo nayo, wananchi ambao wako ndani ya *road reserve*, wasitegemee kulipwa fidia kwa sababu sheria ni msumeno na ni lazima tuizingatie.

Na. 39

**Ahadi ya Serikali Kuwalipa Wafanyakazi wa Mgodi wa Kiwira**

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO** aliuliza:-

Serikali katika Bunge la Tisa ilitangaza kuwalipa Wafanyakazi wa Mgodi wa Kiwira na kuuchukua Mgodi huo ili kuumiliki na kuzalisha umeme:-

(a) Je, kwa nini Serikali haijawalipa wafanyakazi hao mpaka sasa?

(b) Kwa kuwa Shirika la NSSF limeleta kwa maandishi Serikalini nia ya kununua madeni yote ya Mgodi wa Kiwira. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya suala hili?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, suala la Mgodi wa Kiwira ni suala ambalo Serikali imekuwa ikilitolea maelezo kila mara hapa Bungeni hususan suala la wafanyakazi wa mgodi huo. Aidha, ni kweli Serikali ilitangaza kupitia Bunge la Tisa kuwa, italipa wafanyakazi wa mgodi huo mishahara yao. Baada ya tangazo hilo, Serikali imefanya malipo ya malimbikizo ya mishahara yao ya miezi 15 kwa awamu mbili kama ifuatavyo: Awamu ya kwanza ilifanyika katika Kituo cha Kiwira kwa madai yanayoishia mwezi Julai, 2010; na awamu ya pili imefanyika mwezi wa Januari 2011 kwa madai ya malimbikizo ya kuanzia mwezi Agosti, 2010 hadi Januari 2011.

Malipo yamelipwa hadi kufikia Januari kwa mategemeo kuwa, baada ya hapo wahusika watakuwa wanalipwa kwa utaratibu wa kawaida kwa sababu tumeshawaingiza katika bajeti yetu inayoendelea sasa hivi.

(b) Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba, 2010 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), uliwasilisha maombi Serikalini kwa ajili ya kuuendeleza mgodi huo. Kufuatia maombi hayo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi na Shirika la *Consolidated Holding Corporation*, ambalo lipo chini ya Wizara ya Fedha, tumeanza mchakato wa awali kutathmini ombi hilo ili kujiridhisha kama NSSF wanaweza kuendesha shughuli za uchimbaji wa makaa ya mawe na uzalishaji wa umeme kabla ya kuutoa mgodi huo kwao. Hivyo, baada ya mchakato (tathmini) hiyo kukamilika, Serikali itaweka bayana suala hili na endapo atakuwa amekidhi masharti, atamilikishwa mgodi huo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri.

(a) Serikali ilitangaza hapa Bungeni kwamba, itauchukua Mgodi wa Kiwira na kuumiliki, lakini mpaka tunavyozungumza hivi sasa, haijafanyika tathmini yoyote ya mali na madeni ya mgodi kwa ajili ya Serikali kuweza kuuchukua na tayari mmoja wa wakopeshaji kupitia Benki ya CRDB ametangaza kuufilisi mgodi na hivyo kuhatarisha mali na uwekezaji mkubwa ambao Serikali uliufanya katika mgodi huu; Serikali haioni haja ya kuharakisha zoezi na kuumiliki mgodi huu na kuupa kwa Taasisi ya NSSF ambayo tayari wameonesha nia ya kuhakikisha kwamba wanalipa madeni yote ambayo ni ya Mgodi huu ili waweze kuzalisha umeme?

(b) Mheshimiwa Spika, majibu ya Mheshimiwa Waziri ya kusubiri mchakato uendelee Wizara ya Fedha hayaoneshi uharaka au upo mkakati wa Mgodi wa Kiwira katika kumaliza tatizo la umeme nchini; na jana takriban kwa saa mbili nchi nzima ilikuwa haina umeme na *TANESCO* wametangaza zaidi ya megawati 230 zimeondoka katika Gridi ya Taifa; Waziri wa Nishati na Madini analiambia nini Taifa kuhusu Taifa hili? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba, dhamira ya Serikali ya kufanikisha uendelezaji wa Mgodi wa Kiwira iko pale pale na kinachoendelea sasa hivi tangu tutangaze hapa Bungeni ni masuala ya kiutaalam, ambayo ni lazima tuyafanye kwa utaratibu unaoeleweka ili kuhakikisha kwamba, tunapokwenda kuwekeza na kuuendeleza Mradi ule pasiwe na mashaka yoyote katika mradi huo.

Mheshimiwa Spika, muda wote Serikali imekuwa ikifanya kazi yake kwa utaratibu na umakini kuhakikisha kwamba, Mradi ule unaendelezwa. Kwa hiyo, mchakato unaendelea kwa taratibu za kawaida na ndiyo maana tumekuwa tukishiriki vikao kadhaa ambavyo nina hakika Mheshimiwa Zitto anafahamu pia kwa sababu kwa kiasi kikubwa taasisi ambazo zinashirikishwa katika eneo hili ikiwemo NSSF yenyewe ni taasisi ambayo iko chini ya Wizara ya Fedha. Mikutano inaendelea vizuri na masuala yanayojadiliwa ni kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, niseme kuhusu tathmini ama jambo ambalo linaendelea kuhusu Mgodi wa Kiwira kama kigezo cha kuelezea udharura na utashi wa Serikali kumaliza tatizo la umeme hapa nchini. Natambua leo ukiongelea masuala ya umeme nchini, kwa kiwango kikubwa Watanzania wana hasira kubwa kutokana na adha ya mgao wa umeme. Ninaomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu, muda wote Serikali imekuwa na dhamira ya kutokuwa na hili tatizo la umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba umenipa muda mfupi, nakuomba radhi, tunafahamu leo tusingekuwa hapa kama mgodi au uzalishaji wa umeme kupitia gesi ya asili kule ARTUMAS Mkoani Mtwara ungefanikiwa kwa megawati 300 kama isingekuwa tatizo la mdororo wa uchumi ulioikumba dunia mwaka 2008/2009. Tusingekuwa na ajali hii ya Mgodi wa Kiwira leo tungekuwa na megawati 200. Kwa hiyo, kipindi cha mwaka 2006 mpaka leo tungekuwa tumeingiza kwenye Gridi ya Taifa zaidi ya megawati 500.

Tunasema haya ni mambo yanayotokea, hata nchi zilizoendelea matatizo kama haya yanatokea. Niseme kwa kifupi sana ni mikakati ipi iliyopo sasa hivi ya kuhakikisha kwamba tatizo la umeme linaendelea kudhibitiwa hapa Tanzania pamoja na adha tunayopata leo Watanzania.

Kwanza, tumeshaagiza jenereta za kuzalisha umeme megawati 100 kwa Dar es Salaam kwa kutumia gesi asili, Mwanza megawati 90 kwa kutumia mafuta mazito. Serikali imeshanunua mafuta kwa ajili ya kuwasha mitambo ya IPTL ambayo ina uwezo wa kuzalisha megawati 100. Mafuta yapo Dar es Salaam na sasa yanaendelea kupelekwa katika kituo cha uzalishaji wa mafuta.

Kingine, niwakumbushe Watanzania, tuna mgodi ambao tumeshaubuni wa Kinyerezi kwa kushirikiana na Kampuni ya SUMITOM ya Japan, megawati 240 zitawekwa pale Dar es Salaam, pale Somanga Fungu megawati 230 kwa kushirikiana na sekta binafsi. Vilevile tunaendelea na mikakati mingine kuhakikisha kwamba, tunaboresha huduma hiyo katika maeneo mengine. Tuna Mradi sasa wa kupanua miundombinu ya kuzalisha gesi asili kutoka Songo Songo Kisiwani kuja Dar es Salaam, Mradi ambao sasa hivi unafanyiwa kazi kwa usimamizi wa uratibu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji *(EWURA). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali muda wote imekuwa na dhamira ya dhati, kikubwa ni changamoto za kweli lakini kazi inaendelea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naomba Mheshimiwa ulete Kauli ya Waziri kuhusu hili ili isiingie kwenye swali, inakuwa kidogo haijakaa sawasawa. Nimemwona Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ingawa huyu ameshachukua dakika kumi kwa swali hilo tu.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, suala la umeme ni zito sana na tumepata Kauli nyingi kutoka kwenye Serikali na kwa Viongozi kadhaa kwamba, mgao wa umeme utakuwa ni historia. *(Makofi)*

*TANESCO* wametangaza kwamba wanapata hasara ya shilingi bilioni tatu kila siku. Hii *crisis* ya Taifa. Mheshimiwa Waziri atueleze jibu moja; mgao wa umeme unakwisha lini?

**SPIKA:** Nimeshamwagiza Waziri atengeneze Kauli ya Mawaziri. Naomba utumie nafasi hiyo kuliko hii tafadhali. Naona iletwe Kauli ya Waziri badala kueleza saa hizi. *(Makofi)*

Na. 40

**Kuanza na Kukamilika kwa Miradi Viporo na ile Mipya ya Umeme Wilayani Mbozi**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Serikali iliahidi kukamilisha Miradi Viporo ya Umeme Wilayani Mbozi ikiwemo ile ya Ruanda-Iyula-Idiwili, Mahenje-Iyunda, Nanlewa-Vwawa-Hasamba pamoja na kuanza miradi mipya ya Mlowo-Isansa na Igamba-Itaka:-

Je, ni lini Miradi viporo hiyo na ile mipya itaanza kukamilika?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Miradi hii bado unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai 2011. Naomba kuwakumbusha kwamba, Miradi yote iliyo chini ya udhamini wa Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), ratiba yake ya ukamilikaji ni mwishoni mwa mwaka huu na ndiyo maana tunapenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla, tunapotoa jibu la Mheshimiwa Mbunge mmoja anayeulizia kwenye Miradi inayohusika na inayofadhiliwa na Serikali kupitia utaratibu wa Mfuko wa Nishati Vijijini, jibu lake linawahusu Watanzaia kupitia Bunge hili katika Majimbo yote na maeneo yote ambayo yanafadhiliwa na Mradi huu. Miradi hii inatekelezwa na Mkandarasi *M/S Rousant Limited* chini ya usimamizi wa Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO).* Gharama za Miradi hii katika Wilaya zote za Mkoa wa Mbeya ni shilingi bilioni 4.3, fedha hizi ni kwa ajili ya kazi zifuatazo:-

Kwa Wilaya ya Mbozi, inahusu kupeleka umeme katika Vijiji vya Ruanda, Iyula, Idiwili, ikiwa ni sehemu mojawapo ya miradi hii, lakini pia maeneo ya Mahenje, Iyunda Nanlewa, Vyawa, Hasamba pamoja na kuanza Miradi mipya ya Mlowo, Isansa, Igamba na Itaka, ambapo njia ya umeme msongo wa kilovoti 33, urefu wa kilomita 11, kilovoti 0.4 urefu wa kilomita 7 itajengwa na kufunga vipoza umeme vinne.

Wilaya ya Mbeya, kupeleka umeme katika Vijiji vya Santilya kwa Mheshimiwa Lukson Mwanjale, Ilembo, Tembela, Imazu na Horongo, ambapo njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 urefu wa kilomita 36, kilovoti 11 urefu wa kilomita nne; kilovoti 0.4 urefu wa kilomita 6, itajengwa na kufunga vipoza umeme vitano.

Wilaya ya Chunya kwa Mheshimiwa Mwambalaswa, kupeleka umeme katika Vijiji vya Lupa na Tingatinga ambapo njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 urefu wa kilomita 44, kilovoti 0.4 urefu wa kilomita nne itajengwa na kufunga vipoza umeme vinne. Wilaya ya Rungwe, kwa Mheshimiwa Profesa Mwandosya pamoja na Mheshimiwa Profesa Mwakyusa, kupeleka umeme katika Vijiji vya Luteba, Mwakaleli na Matamba, ambapo njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 urefu wa kilomita nane, kilovoti 0.4 urefu wa kilomita tano itajengwa na kufunga vipoza umeme vitatu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine wanaohusika na Miradi hii kwamba, kwa ujumla kazi zote zilizopangwa za Miradi hii zinaendelea vizuri na zitakamilika katika kipindi kilichopangwa, kama nilivyosema, mwishoni mwa mwaka huu. Ahsante sana.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba, mimi ni Mbunge wa Mbozi Mashariki siyo Magharibi, nina hakika alikosea tu kwa sababu anajua Mheshimiwa Waziri. Maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Miradi ya Umeme wa Ruanda, Iyula, Idiwili, Mahenje, Igunda na Vwawa Hasamba ina umri karibu miaka kumi, mpaka leo haijatekelezwa na Serikali imekuwa inatoa ahadi ya mara kwa mara, pamoja na Waziri kutuhakikishia pesa zimepatikana kwa sababu miradi hii awali ilielezwa kwamba imekamilika mwaka jana haikufanywa hivyo na leo anasema itakamilika Julai, mwaka huu: Je, anawahakikishia wananchi wa maeneo hayo niliyoyataja kwamba ahadi ya Serikali kukamilisha miradi ya umeme mwezi Julai mwaka huu ina ukweli?

(ii) Mheshimiwa Spika, umeme kutoka Igamba kwenda Itaka ni ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais mwaka juzi alipokuja Mbozi lakini pia na mwaka jana bahati nzuri aliongozana na Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Ngeleja; na Mheshimiwa Ngeleja mwenyewe akatoa ahadi kwamba umeme huo pia utakelezwa kwa maana kutoka Igamba kwenda Itaka; na kwa sababu kwenye majibu utekelezaji wa umeme wa kutoka Igamba kwenda Itaka haupo; je Mheshimiwa Waziri atatuhakikishia sasa Wananchi wa Igamba, Halungu mpaka Itaka kwamba Miradi hiyo itaonekana kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka huu?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba radhi, mara ya kwanza ilikuwa ni kosa la utamkaji. Kuhusu utekelezaji wa Miradi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameulizia kwa upande wa swali la kwanza la nyongeza; ratiba ipo hapa, nimesema Miradi yote inayofadhiliwa na REA kwa ujumla wake, itakamilika kwa mpango uliopo mwishoni mwa mwaka huu. Katika hali ya kawaida ya utekelezaji, iko

Miradi ambayo inatekelezwa mapema zaidi na itakamilika mapema zaidi kabla ya mingine lakini programu nzima itakamilika mwisho wa mwaka huu.

Kuhusu ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais na mimi nilikuwepo siku hiyo kuhusu Mradi wa kufikisha umeme katika maeneo ya Igamba, Haluu hadi Itaka, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Zambi kwamba; ni kweli maombi hayo tumeshaanza kuyafanyia kazi tangu tulipofanya ziara ile mwaka jana. Tunaendelea kuweka katika bajeti ijayo, kwa hiyo, ahadi iko pale pale na tutaendelea kuitekeleza kama tulivyoahidi. Ahsante sana.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Nami ningependa kuiuliza Serikali ahadi ya kuleta umeme katika Vijiji vya Bukoli, Katoro, Lwamgasa imekuwa ni ya muda mrefu sana; ninaomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni lini hasa utekelezaji wake utaanza?

**SPIKA:** Ukweli huko anakujua, haya naomba ujibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, ni kweli wenzangu wanafahamu ukweli huu na hili nalijibu kwa niaba ya wananchi katika maeneo yote ambayo wananufaika na Mradi wa Ufadhili wa MCC. Tumekuwa tukitoa taarifa hapa na tutaendelea kufanya hivyo na hapa umetoa maelekezo kwamba, tulete Kauli ya Serikali tuwakumbushe tena Watanzania kupitia Bunge hili Tukufu. Utekelezaji wa Miradi ya MCC umeshaanza na ni kama nilivyosema nilivyokuwa najibu swali juzi hapa, kwa sasa hivi hatua iliyofikiwa ni ulipaji wa fidia kwa wale ambao wanaathirika na Mradi huo. Kwa haraka haraka, Mikoa inayohusika ni Mwanza, Dodoma, Morogoro, Mbeya, Iringa na Tanga.

Tunarajia kwa utaratibu wa programu ilivyo, ifikapo mwezi wa 11 au mwezi wa 12 mwaka kesho, utekelezaji wa Miradi yote katika hiyo Mikoa utakuwa imeshakamilika, kasoro eneo la mto Malagarasi ambako mwanzoni tulidhania kwamba, ingekwenda sambamba na utekelezaji huu utakuwa umeathirika baada ya kilichojitokeza kugundua kwamba pale kuna viumbe adimu; kuna konokono fulani ambao wamekwamisha uendelezaji wa Mradi ule. Shukrani kwa wafadhili na tunawashukuru sana wafadhili wetu, wamekubali kufanya tathmini ili Mradi uliokusudiwa kule katika Mto Malagarasi uendelee katika eneo lingine. Habari njema ni kwamba, huenda tukawa na kiasi kikubwa zaidi ya kiasi cha umeme kilichokusudiwa mwanzoni katika eneo hili. Nafahamu Mheshimiwa Zitto pamoja na Wabunge wote wa Kigoma, mnalifahamu vizuri eneo la Igamba III, ndiko tunakofanyia tathmini.

Na. 41

**Suala la Bei Ndogo ya Miwa Baada ya Viwanda vya Sukari vya Mtibwa na Kilombero Kubinafsishwa**

**MHE. AMOS G. MAKALLA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaingilia kati suala zima la bei ya miwa Mtibwa ili wakulima waweze kufaidika nayo?

(b) Je, ni lini Serikali itaingilia kati tatizo la ulipaji mishahara, mafao na stahili nyingine kwa wafanyakazi waliopo kiwandani na waliostaafu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mbunge wa Mvomero, lenye sehemu (a) na (b) Kama ifuatavyo:-

(a) Ili kuhakikisha wakulima wanafaidika na bei nzuri ya miwa wanayozalisha, Serikali kupitia Bodi ya Sukari Tanzania, iliwezesha mazungumzo kuhusu uandaaji wa mkataba kati ya mmiliki wa Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa na wakulima wadogo wa miwa wa Mtibwa. Mkataba huo wa kuuziana miwa uitwao *Cane Sale Agreement-Full Division of Proceeds (DoP),* uliotiwa saini tarehe 13 Agosti, 2009 una lengo la kumwezesha mkulima kupata faida kutokana na miwa anayoizalisha na kuiuza kwa mwenye kiwanda. Kimsingi, Mkataba huo hauna tofauti kubwa na Mkataba uliopo kati ya Kiwanda cha Sukari cha Kilombero na Wakulima Wadogo. Serikali inachosisitiza ni kuwa, kila upande wa Mkataba huu utekeleze wajibu wake; wakulima watekeleze wajibu wao wa kutayarisha miwa kwa wakati na kwa viwango vya ubora vilivyowekwa; na kiwanda kikishachukua miwa hiyo, kiwalipe wakulima ndani ya siku 40 zilizoainishwa ndani ya *Cane Sale Agreement-Full Division of Proceeds (DoP).*

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Mtibwa kinamilikiwa na mtu binafsi kwa asilimia 100. Wakulima wasipokubaliana na bei wanayopewa, Mkataba uliopo kati yao na mwenye kiwanda, unawaruhusu wakulima kumtafuta mkaguzi wa hesabu wa kujitegemea kuhakiki hesabu na inapobidi kupeleka suala lao kwenye usuluhishi kulingana na sheria za nchi. Mara kadhaa, Wakulima wa Mtibwa wamekuwa wakitoa malalamiko yao kwa Viongozi wanapowatembelea wakiwemo Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Mbunge na wengine wengi, kuhusu bei ndogo ya miwa na kucheleweshewa malipo. Hata hivyo, ni muhimu kwa kiwanda kupunguza gharama zisizo za lazima ili malipo ya wakulima yaendane na soko la sukari na yawe na ulinganisho na viwanda vingine hapa nchini.

Wizara yangu kupitia Bodi ya Sukari, itaendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa wakulima juu ya kilimo cha mkataba ili waelewe haki na wajibu wao.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, Kiwanda cha Mtibwa kinamilikiwa na kuendeshwa na mtu binafasi kwa asilimia mia moja; hivyo, mahusiano ya mwekezaji na wafanyakazi yanatawaliwa na Sheria ya Kazi ya Mwaka 2006, ambayo pia iliunda Taasisi ambazo mwajiri na mfanyakazi anaweza kuzitumia kupata ahuseni iwapo kutatokea kutofautiana katika mahusiano yao kazini.

Napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Amos Makalla, kwa swali hili zuri na kutoa wito kwa wawekezaji wote katika mashamba na viwanda vya mazao, kuheshimu mikataba wanayoingia na wakulima na kuheshimu masharti ya uwekezaji waliyokubaliana na Serikali ili kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza kwa kukiuka makubaliano.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri kwa majibu kwa swali hili lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Ieleweke kwamba wakulima wa miwa wanaheshimu sana huo Mkataba aliousema na wamekuwa wakiuza miwa na hawajawahi kukiuka Mkataba na mara kwa mara mwekezaji ndiye ambaye amekuwa akikiuka Mkataba huo. Pia sijui kama Waziri anazo taarifa za kutosha kwamba wenzetu wa Kilombero miwa sasa hivi *liniment* kumi ya tani moja wanauza shilingi 55,000 lakini Mtibwa bado shilingi 38,000; tofauti ya shilingi 16,000; na anaposema kwamba wakulima watafute mkaguzi wa nje aje akague hesabu zinazotengenezwa na mwenye kiwanda anayemiliki asilimia 100; je, kazi hiyo kwa nini Serikali isiingilie kati iifanye yenyewe? *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa kwa muda mrefu Viongozi mbalimbali wa Kitaifa wamesikia tatizo la wakulima kutokulipwa fedha zao kwa wakati na hata hivi majuzi mimi nilipokwenda na kupiga kelele akalipa tarehe 7 mwezi wa pili na amekuwa halipi wakulima kwa wakati: Je, Serikali inaingiliaje kati kuona kwamba anaheshimu Mkataba na kuwalipa wakulima fedha zao kwa wakati na kuwalipa mafao wastaafu katika Kiwanda cha Mtibwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nafahamu kwamba, viwanda hivi viwili; Mtibwa na Kilombero, vinatofautiana katika malipo. Kama nilivyosema, Mtibwa yenyewe inamilikiwa kwa asilimia 100 na mtu binafsi. Kile kingine cha Kilombero ambacho anakilinganisha, chenyewe angalau kina uzoefu mkubwa kuliko hata hiki cha Mtibwa kwa sababu wale walianza zamani, ukitazama hata utaratibu wa uendeshaji wao ni tofauti kidogo, ukokotoaji ni tofauti kidogo, hata utoaji wa taarifa zao ni tofauti. Ninachotaka kusema tu hapa ni kwamba, nakubaliana na Mheshimiwa Makalla kwamba, ipo haja ya kutoa ushauri kwa Wakulima wa Mtibwa angalau kuanza kutambua haki zao.

Yeye anasema kwamba wanajua kila kitu, lakini mimi ninafikiri mahali ambapo kuna sheria na makubaliano kati ya wakulima na mwenye kiwanda, zipo taratibu ambazo ndizo zinatawala Mkataba ule. Kwa hiyo, nilichosisitiza hapa ni kwamba, ipo haja ya sisi watu wa Serikali kuwashauri kwanza wakulima kuelewa ni nini kilichomo kwenye Mkataba wao ili watakapokwenda kupeleka malalamiko, yasitokee mambo mengine ambayo yanaweza kusababisha wakashindwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ninaelewa kwamba, Kilombero wanatoa shilingi 56,000 kwa tani wakati wenzao ni shilingi 38,000 kwa tani. Yote haya yanatokana na ule ukokotoaji wa yale mahesabu na yanatokana na kwamba, Mtibwa wana *accounts* zao na Kilombero wana *accounts* zao na kila mmoja hesabu zake anazificha. Nataka niseme tu

kwamba, ninakubaliana na yeye, sisi kama Serikali tutaendelea kushauri na kuwasaidia wakulima kwanza waelewe haki zao za msingi na tayari *SUDECO* wameshakwenda wamejitahidi kuwasaidia wakulima hao na ndiyo kazi yetu. Tutaendelea kufanya hivyo kuwasaidia ili hatimaye pande zote mbili ziweze kuheshimu Mikataba kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi.

Na. 42

**Baadhi ya Shule za Kata Kufanywa za Kilimo**

**MHE. KIBONA N. ALIKO** aliuliza:-

Ingawa suala la Kilimo cha Kwanza limekuwa kipaumbele cha kwanza, lakini bila kutoa elimu kwa watu haliwezi kufanikiwa:-

Je, Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kufanya baadhi ya shule zetu katika Kata au kwenye Wilaya ziwe na mchepuo wa kilimo na ufundi ili kutoa elimu stahiki ya kilimo na ufugaji ili vijana wetu wapatiwe taaluma itakayowasaidia kujitegemea kimaisha kupitia Sekta ya Kilimo na Ufugaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kibona Aliko, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mfumo rasmi wa utoaji elimu katika stadi za kilimo na ufugaji unaohusisha ufundishaji katika shule na vyuo vinavyomilikiwa na Serikali na watu au taasisi binafsi. Wizara na Asasi za Serikali zinazosimamia utoaji wa mafunzo ya kilimo na ufugaji ni pamoja na hizi zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilito, Chakula na Ushirika katika Vyuo vya Kilimo *(Ministry of Agriculture Training Institutes – MATIs),* Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi katika Vyuo Vya Mifugo *(Livestock Training Institutes)*, Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Watoto katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika Shule za Sekondari mchepuo wa kilimo; vyuo vinavyosimamiwa na Mamlaka ya Elimu ya Ufundi *(VETA)* na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine *(Sokoine University of Agriculture – SUA).* Wizara ya Kilito, Chakula na Ushirika inavyo vyuo 13 vya kufundisha wataalam wa kilimo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Wizara inashirikiana na Sekta Binafsi katika kuviendesha vyuo viwili vya kufundisha wataalam wa kilimo vilivyopo Kilalacha, Wilayani Moshi katika Mkoa wa Kilimanjaro na Igabiro Wilayani Muleba katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, kupitia mfumo huo, shule za sekondari zina nafasi kubwa na muhimu ya kuwaandaa vijana wa Taifa letu katika fani ya kilimo kuliko asasi nyingine zote. Mpaka sasa, shule za sekondari zilizosajiliwa kama shule za mchepuo wa kilimo ni takriban shule 350 kati ya shule 4,102 za sekondari zilizopo.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha vijana wengi wa Tanzania wanapata fursa ya kupata elimu katika shule zenye mchepuo wa kilimo, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI*)* na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kuhakikisha shule nyingi zaidi zinakuwa na mchepuo wa kilimo. Aidha, Wizara yangu itaendelea kuihamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika utoaji wa elimu kwa wakulima na wataalamu wa kilimo katika ngazi ya Sekondari, Vyuo Vya Astashahada, Shahada na Uzamivu.

**MHE. KIBONA N. ALIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, naomba nimuulize kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa amesema kwamba ili shule iweze kusajiliwa inahitaji kukidhi vigezo vya kufundisha masomo tisa na katika masomo tisa somo la kilimo halimo; na kwa kuwa kwenye swali langu la msingi sikuzungumza kwamba kila shule iwe ni ya kilimo; je, Waziri haoni kwamba ni muhimu sasa katika Wilaya zetu angalau shule moja kati ya zile zote za Kata iwe shule ya kilimo?

(ii) Waziri amezungumzia juu ya udahili wa wanafunzi wetu wa somo au kozi ya kilimo katika Chuo Kikuu cha Sokoine; kwa maelezo yake, idadi ya wanafunzi waliodahiliwa ni 93. Mimi ningependa kumuuliza; kwa vile Taifa limetangaza kaulimbiu ya Kilimo Kwanza Namba Moja; je, Waziri haoni kwamba idadi hiyo kusikika masikioni mwa Watanzania kwamba kuna wanafunzi 93 waliodahiliwa kwa ajili ya kuwaandaa kuwa walimu wa kilimo katika shule zetu ni namba ndogo mno?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kibona, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, vipo vigezo ambavyo ni lazima kuvikidhi kabla hujaruhusiwa kuingiza mitaala ya aina yoyote. Ninataka tu nimueleweshe Mheshimiwa Kibona kwamba, somo la kilimo katika ngazi anayoizungumza, ninavyojua ngazi ya shule za sekondari, lenyewe linasimamiwa na masomo ya msingi ya sayansi kama yale ya bailojia, kemia, sasa lile somo linakuwa kama ndiyo mahali pa kuanzia. Kwa hiyo, sidhani kama hili ni tatizo kubwa kwamba, somo la kilimo ndio linaweza likasababisha kama halipo basi kisiwe kigezo. Ninafikiri bado hakuna kilichoharibika, midhali kuna dhamira ya kuweka masomo hayo katika ngazi hiyo, inawezekana kabisa ilimradi tu suala hili liibuliwe katika shule zetu liingizwe katika mitaala na wahusika wapitie; sidhani kama kuna tatizo lolote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udahili wa *SUA;* mimi nimetaja idadi hiyo lakini labda ningependa akipata nafasi zaidi nimpe idadi ya wanafunzi walio katika vyuo vyetu kwenye kila ngazi mpaka kufikia kwenye shahada na hiyo nitampa peke yake. Kwa hivi sasa, napenda tu itoshe nimwambie hivi; wataalamu tarajiwa katika ngazi ya shahada ni 1,221, ambao tayari wapo katika Chuo Kikuu Cha Kilimo Cha Sokoine, hao tunawatarajia, lakini sikuwa na maana ya 93 tu, labda hao ndiyo wamedahiliwa na kwamba, ndiyo tunaowatarajia tu. Tunao 1,221 ambao tayari tunawatarajia wahitimu na wakihitimu tutaendelea kuajiri na wakati huo huo chuo kinaendelea kudahili kama inavyofahamika. Vilevile siyo kwamba, tunatarajia Chuo Kikuu cha Sokoine tu, Vyuo Vikuu vipo vingi na hawa watu wamo sokoni. Hata wanaotoka kwenye Vyuo Vikuu vya Nje ya nchi pia wanayo nafasi ya kuajiriwa kuchukua nafasi hizi za kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, kwa upande huu wa Maafisa Ugani, pamoja na kwamba sikuulizwa hili; naomba nitoe pongezi kubwa sana kwa Halmashauri ya Wilaya ya Same, kwa sababu imekuwa ya kwanza kabisa katika Tanzania nzima, kuajiri Maafisa Ugani 58 na kukamilisha, kila kijiji cha Halmashauri ile sasa kina Afisa Mgani mmoja. *(Makofi)*

Na. 43

**Vigezo Vya Malipo ya Pensheni Kwa Askari Polisi Wastaafu**

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH** aliuliza:-

Je, ni vigezo gani vya usawa vinavyotumika kuwalipa pensheni na viinua mgongo Watumishi wa Jeshi la Polisi wanapostaafu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuleta usawa katika malipo ya pensheni, mahesabu ya kiinua mgongo na pensheni kwa wastaafu wote yanafanyika kwa kutumia mshahara wa mwisho na muda aliofanya kazi mstaafu. Kwa upande wa askari polisi, askari akiajiriwa hupewa mikataba ya miaka mitatu mitatu na akiwa amefanya kazi kwa jumla ya miaka 12 mfululizo anatakiwa kuchagua ama aajiriwe katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni (Pensheni) au katika masharti ya Mkataba wa *Gratuity.*

Mheshimiwa Spika, askari aliyechagua kuajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni atakapofikia muda wa kustaafu, atalipwa kiinua mgongo na pensheni na kwa yule aliyechagua masharti ya mkataba, atakapostaafu atalipwa kiinua mgongo tu.

Mheshimiwa Spika, vigezo vya usawa vinavyotumika kuwalipa pensheni na kiinua mgongo Watumishi wa Jeshi la Polisi ni muda wa utumishi wao katika Jeshi na pia ngazi ya mshahara wa mwisho aliyofikia askari huyo.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa Jeshi letu la Polisi limejengeka kinidhamu, hawawezi kudai haki zao kwa maandamano au kwa fujo; ni kwa nini wanacheleweshewa malipo yao hawalipwi kwa wakati?

(ii) Kulingana na hali ya maisha ilivyopanda malipo haya inaonesha hayalingani na maisha; Mheshimiwa Waziri anafikiriaje kuwalipa nyongeza juu ya malipo yao haya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu ucheleweshaji wa malipo; Serikali haina nia ya kuchelewesha malipo ya wafanyakazi au wastaafu. Inapotokea kuchelewa, kunakuwa ama kuna sababu kuhusu kumbukumbu au sababu nyingine zinazohusu taarifa za mstaafu. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, malipo haya hayacheleweshwi na yanalipwa kila askari atakapostaafu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyongeza ya malipo; nakubaliana na yeye kwamba, ugumu wa maisha unaongezeka na si askari polisi tu ambao wanapambana na tatizo hili. Siku zote Serikali ina nia itakapoweza kupata nafasi kuyashughulikia malipo kwa kuongeza nyongeza kwa wafanyakazi wote. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa inaonekana kuna matatizo baina ya Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Fedha katika suala la kuwalipa hawa wastaafu, kinachotokea ni askari anastaafu lakini anaambiwa ati mchango wake *NSSF* haujafikishwa kunakotakiwa na hilo linasababisha kucheleweshwa kwa malipo yake. Je, ni lini sasa Wizara ya Mambo ya Ndani itawaagiza watendaji wake kuhakikisha kwamba makato yote yanayokatwa yanapelekwa kwa wakati ili hilo isiwe sababu ya kumcheleweshea mtu haki yake kwa jambo dogo kama hilo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii adhimu, kwanza, kumshukuru Mheshimiwa Khalifa, kwa swali lake zuri. Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kupitia Bunge lako Tukufu, inamhakikishia

Mheshimiwa Khalifa na Waheshimiwa wengine kwamba, tutafanya kila linalowezekana kufuata ushauri alioutoa.

Mimi ninadhani ni ushauri mzuri, tutawahimiza watendaji wote wahakikishe kwamba, makato haya ya Wafanyakazi na Watumishi wa Jeshi la Polisi yanapelekwa kunakohusika. Mimi kama Waziri, namhakikishia kwamba, tutafanya jitihada kwa kadiri ya uwezo wetu, kuhakikisha kwamba jambo hilo linafanyiwa kazi na kipindi kifupi kijacho matunda yake yataonekana. *(Makofi)*

Na. 44

**Kodi Katika Zana za Kilimo**

**MHE. JITU V. SONI** aliuliza:-

Ingawa Serikali inayo azma kubwa ya kukuza na kuinua Sekta ya Kilimo, lakini azma hiyo nzuri inaweza isifanikiwe jinsi ilivyokusudiwa ikiwa Serikali haitaangalia upya eneo linalohusiana na kodi kwenye zana mbalimbali za kilimo:-

Je, ni lini Serikali itaangalia upya suala zima la mfumo wa utozaji kodi za aina mbalimbali kwenye zana za kilimo kama vile tairi la trekta, sahani za jembe, *harrow, planter*, mashine za maji ya umwagiliaji, *motor vehicle licence* kwa trela za trekta, kodi na ushuru wanaotozwa wazalishaji wa mbegu nchini ili kukuza Sekta ya Kilimo na kulipatia Taifa pato na mkulima aweze kufaidika na kilimo chenye tija?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mbunge wa Babati Vijijini, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuvutia wawekezaji katika kilimo, ikiwa ni pamoja na kusamehe kodi za mitambo na mashine mbalimbali zinazotumika kwenye kilimo, zikijumuisha msamaha wa ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na hata kodi za mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutazama maeneo ambayo nimeyataja hapo juu katika maelezo yangu ya jumla, ni dhahiri kwamba, zana nyingi za kilimo tayari zimeshapatiwa msamaha wa kodi na Serikali. Pamoja na hatua hizi ni azma ya Serikali kuona kwamba, mfumo wa utozaji wa kodi kwenye zana za kilimo unaendelea kupitiwa mara kwa mara ili kutoa fursa kubwa zaidi kwa wakulima walio katika sekta hii ambayo ni muhimu katika kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia lengo hili, ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya Serikali kuanza utekelezaji wa Kilimo Kwanza, pamoja na mambo mengine, iliunda Kamati ya Kodi ya Kilimo Kwanza. Kamati hii pamoja na kazi nyingine, imepewa jukumu la kuzichambua kwa kina kodi za vivutio vinavyohitajika kutolewa katika Sekta ya Kilimo na kuwasilisha mapendekezo Serikalini. Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge ni wadau muhimu katika hili, nawaomba wajitokeze kutoa michango yao ya mawazo kwenye Kamati hii ili marekebisho yanayohitajika yafanywe kwa wakati.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Je, ni lini Serikali kwa nia nzuri itarekebisha mfumo wa namna ya kutoza kodi? Kwa hivi sasa kodi katika zana za kilimo na vipuri vyake, tunatozwa bei ya kununua na baada ya hapo inajumuishwa bei ya usafirishaji *(freight),* bei ya *insurance* na baada ya hapo ndiyo unatozwa hiyo kodi *(import duty);* ile jumla kuu inakuja kutozwa *VAT*. kwa hiyo kama ni asilimia mbili ya *import duty* kwenye matairi kwa mfano na asilimia 18 ya *VAT* utakuwa umelipia ile *freight* pamoja na bima, *import duty* halafu *VAT* utakuwa umelipia bei ya kununua, *freight, insurance* na *import duty*. Kwa hiyo, siyo ile asilimia 20 ambayo ipo pale, utakuwa umelipa zaidi ya asilimia 28; na kama *import duty* ni asilimia 10 utakuwa umelipia asilimia 35. Je, mfumo huo, ni lini Serikali itaurekebisha ili uende na viwango na kupunguza gharama?

(ii) Je, ni lini Serikali itapeleka wataalam wetu wa kodi katika mafunzo ya kilimo na zana zake ili tusilumbane; mara nyingi wafanyabiashara na wakulima wanaoagiza zana za kilimo na vifaa vyake wanalumbana kwa sababu wanaambiwa hivyo vifaa ni *multipurpose;* mfano, sahani za jembe, matairi ya trekta, wanaweza kutumia zaidi ya kilimo; lakini sahani ya jembe utaitumia wapi zaidi ya kwenye kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Jitu Soni, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Kuhusu suala la ukokotoaji kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba, mambo yote yanayohusu kodi za vifaa vya kilimo, yanatakiwa yapelekwe kwa sasa kwenye Kamati hii ya Kilimo Kwanza, ambayo iko wazi na inapokea mawazo. Kwa hiyo, kwenye hili nilikuwa namwomba Mhehimiwa Jitu na Wabunge wengine kwamba, mawazo kama haya yawasilishwe kwa sababu si suala la lini, hili suala linaweza likafanyika wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwapeleka mafunzo watozaji kodi kwenye zana za kilimo, suala la mafunzo ni suala zuri na tunalichukua na tunaweza kuwapeleka wakati wowote ambapo hali itaruhusu. Hata hivyo, utozaji wa kodi wa zana za kilimo unaoendelea sasa, unafanywa chini ya maelekezo au ushauri wa wataalam wa kilimo, ambao ndiyo wanaleta *division*, yaani *HA Code* kwa ajili ya ku-*define* kile kifaa au zana ambayo inataka kuletwa kwenu kutozwa kodi. Ni kweli kwamba, kuna baadhi ya vifaa au zana hasa *pump multipurpose*. Kuna orodha imekuwa *deemed* kuwa ni bidhaa za mitaji ambazo zinashughulikiwa. Maelezo ya msingi na hatua zinachukuliwa kutozwa kodi zinatoka na hiyo *HA Code* ambayo inakuwa imetoka kwenye kilimo. Pamoja na hivyo, ushauri wake ni mzuri na tutauzingatia na kuuchukulia hatua ipasavyo. *(Makofi)*

Na. 45

**Uhitaji wa Chuo Kikuu Kanda ya Ziwa**

**MHE. EZEKIA D. WENJE** aliuliza:-

Ingawa kumekuwepo na juhudi za kupanua Elimu ya Juu hapa nchini lakini Kanda ya Ziwa haina Chuo Kikuu hata kimoja:-

Je, kwa nini Serikali isione kwamba huu ni muda muafaka wa kujenga Chuo Kikuu katika Kanda ya Ziwa au kukipandisha hadhi Chuo cha Ualimu Butimba kuwa Chuo Kikuu kamili? Kanda ya Ziwa haina Chuo Kikuu hata kimoja cha Serikali au Chuo cha Umma.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, katika Kanda ya Ziwa kuna vyuo vitatu ambavyo ni Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino kilichopo Mwanza, Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba cha Bugando kilichop Mwanza na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania chenye matawi katika Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa pamoja na nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, mchakato wa uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Kilimo Mkoani Mara umeanza na hadidu za rejea kuhusu mchakato mzima wa uanzishwaji wa Chuo hicho Kikuu cha Kilimo Mkoani Mara zimeandaliwa tayari kwa kazi tajwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupandisha hadhi Chuo cha Ualimu Butimba kuwa Chuo Kikuu Kamili, Serikal ilitoa agizo mwaka 2008 la kutovipandisha vyuo vya kada za kati kuwa vyuo vikuu kamili kwa sababu vyuo hivi vinahitajika katika kutoa taaluma kwa

maendeleo ya nchi. Kwa kuvipandisha vyuo vya kada za kati kuwa vyuo vikuu, tutakuwa tunaua taaluma maalum ambayo inahitajika kwa maendeleo ya nchi. Suala la msingi ni kwa Serikali kushirikiana na wadau mbalimbali kuanzisha vyuo vikuu vipya badala ya kuvipandisha hadhi vyuo vya kada za kati. Aidha, ikumbukwe kuwa vyuo vikuu vyote ni vya kitaifa na kimataifa kwani udahili wa wanafunzi unafanyika kutoka sehemu zote za nchi na nje ya nchi bila kujali chuo kikuu kimejengwa Kanda ipi ya Tanzania.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Elimu, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kanda ya Ziwa ni moja ya Ukanda ambao una idadi ya watu wengi, lakini hivi vyuo binafsi kama St. Augustine University inakuwa na *internal policy* ambayo ni tofauti na Vyuo Vikuu vya Umma vinavyoendeshwa, ndiyo maana inafikia wakati hata mwanafunzi anafukuzwa au anasimamishwa masomo kama hajamaliza kulipa ada. Sasa leo kama mwanafunzi anatoka Mtukura anachaguliwa kwenda kusoma Mkwawa kule Iringa halafu Serikali inampa mkopo asilimia 60, inafikia wakati huyu mtoto anayetoka Mtukura hatafika kwa kukosa nauli; je, kwa nini Serikali isione kwamba wakati umefika wa kujenga Chuo kingine Mwanza kitakachosaidia vijana wengi wanaotoka Kanda ya Ziwa?

**TAARIFA**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA**: Taarifa ya kufanyaje; hata hajauliza swali lake! Naomba aulize swali lake kwanza. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunilinda. Swali la pili ni kwamba; kwa kuwa tunacho Chuo cha Uvuvi cha Nyegezi pale Mwanza na uchumi mkubwa wa watu wa Kanda ya Ziwa unategemea uvuvi; sasa kwa nini Serikali isione ni muda muafaka wa Chuo kama cha Uvuvi cha Nyegezi kupandishwa kuwa chuo kikuu kitakachotoa mafunzo yanayoendana na masuala ya uvuvi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ezekiel Dibogo Wenje, kwa ufupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, tayari hadidu za rejea zimeshaandaliwa kwa ajili ya kuanzishwa Chuo Kikuu cha Umma Mkoani Mara kwa sababu Mkoa wa Mara ni moja kati ya mikoa iliyoko Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa kudahili wanafunzi au Bodi ya Mikopo inavyotoa fedha kwa wanafunzi, huwa hatuna ubaguzi kwa hivyo vyuo vya umma na vyuo vya binafsi. Serikali inajali sana muunganiko wa sekta hizi. Kwa hiyo, suala la

kwamba, vyuo vya umma na vyuo binafsi vinatofautiana katika huduma za kiserikali, nadhani kuwa ukiangalia udahili wa wanafunzi na utoaji wa Bodi ya Mikopo, tunakwenda kwa pamoja kwa vyuo vyote.

Kuhusu kuanzisha Chuo cha Uvuvi Mkoani Mwanza, tunatambua Serikali hii ya Awamu ya Nne kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, anaitambua sana Sekta ya Uvuvi. Kwa hiyo, Wizara yangu tutashirikiana pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tuweze kuangalia kama uwezekano utakuwepo wa kuanzisha programu kwa masuala ya uvuvi kule mwanza. Ahsante.

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, niko nyuma kabisa ya muda na maswali bado ni mengi, kwa hiyo, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis.

Na. 46

**Tofauti ya Mishahara ya Walimu Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara**

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS** aliuliza:-

Elimu ya Sekondari hadi Chuo Kikuu ni ya Muungano na Mitaala na Mitihani yote hutayarishwa na Baraza la Mitihani la Taifa na hata wasimamizi wa mitihani hulipwa na Serikali ya Muungano chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi lakini kuna tofauti ya mishahara ya Walimu wa Tanzania Zanzibar na wale wa Tanzania Bara:-

(a) Je, kwa nini mishahara ya Walimu wa Tanzania Zanzibar inatofautiana na ile ya Walimu wa Tanzania Bara?

(b) Je, Serikali haioni kuwa tofauti hiyo inachangia kushuka kwa kiwango cha ufaulu wa mitihani mara zote kwa upande wa Tanzania Zanzibar?

(c) Je kwa nini Tanzania Zanzibar kusiwe na ofisi maalum ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambayo itakuwa ikishughulikia mwenendo mzima wa masomo ya sekondari na mafao ya walimu kama ilivyo kwenye sekta nyingine za Muungano?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raya Ibrahim, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, suala la elimu ya juu pamoja na Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania ni miongoni mwa masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la mishahara ya watumishi wa umma wakiwemo walimu, siyo suala la Muungano, hivyo kila upande wa Muungano una utaratibu wake. Mambo yanayochangia kushuka kwa ufaulu ni mengi siyo mishahara pekee. Baadhi ya sababu za kushuka kwa ufaulu ni ukosefu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, uwezo mdogo wa walimu na wanafunzi, mazingira duni ya kufundishia na kujifunzia na uongozi mbaya wa shule husika.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa uendeshaji wa elimu ya sekondari siyo moja ya masula ya Muungano; hivyo basi, hakuna ofisi maalum ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania Zanzibar, inayoshughulikia uendeshaji wa masomo ya sekondari na mafao ya walimu. Hata hivyo, katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuna Idara ya Elimu ya Juu ambayo inaratibu masuala ya Elimu ya Juu kwa pamoja.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, kwa majibu yake mafupi, mazuri na yenye kueleweka. Pamoja na hayo, nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa suala zima la Baraza la Mitihani la Taifa ni suala la Muungano na mpaka sasa kwa Zanzibar hakuna ofisi; je, kuna utaratibu gani wa kuanzisha ofisi Zanzibar?

(ii) Kama upo utaratibu wa kuanzisha ofisi Zanzibar; ni lini ujenzi huo ama shughuli hiyo itaanza?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya mawili ya nyongeza ya dada yangu, Mheshimiwa Raya Ibrahim, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, moja ya taasisi za kimuungano katika Wizara yetu ni suala la Baraza la Mitihani. Naomba nimjulishe Mheshimiwa Raya kwamba, akienda pale Ofisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, tayari tuna ofisi ndogo inayoshughulikia masuala ya Baraza la Mitihani Zanzibar. Hata hivyo, Serikali kwa kuangalia umuhimu wa Muungano, tayari tunao uwanja pale Zanzibar ambao tunategemea katika bajeti ya mwaka 2011/2012, tutaanza ujenzi wa kujenga ofisi nzuri kabisa pale Zanzibar ya Baraza la Mitihani.

Na. 47

**Utendaji Mbovu wa Idara ya Ardhi Wilaya ya Tarime**

**MHE. NYAMBARI M. NYANGWINE** aliuliza:-

Wilaya ya Tarime ina historia ya muda mrefu ya migogoro ya kijamii ikiwemo ya ardhi licha ya jitihada zinazofanyika miongoni mwa wanajamii wenyewe kwa

kushirikiana na Serikali, Viongozi wa Madhehebu ya Dini pamoja na wazee ili kupata ufumbuzi wa migogoro hiyo:-

Je, kwa nini Serikali inaendelea kuwalinda watendaji wabovu wa Idara ya Ardhi Wilayani Tarime kwa kutowachukulia hatua zinazostahili kutokana na makosa yaliyokithiri?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inayo taarifa juu ya utendaji usioridhisha wa baadhi ya ofisi za ardhi nchini. Moja ya sababu za utendaji huo ni baadhi ya watumishi kutozingatia maadili na kanuni zinazosimamia taaluma zao. Hata hivyo, naomba kutamka wazi mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali haiwalindi na wala kuwavumilia watendaji wabovu wa idara za ardhi bali huwawajibisha pale inapothibitika kuwa wamevunja maadili ya kazi zao. Ili kuondokana na kero hiyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itatathmini utendaji wa Maafisa wa Idara ya Ardhi nchini kote, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. Iwapo itabainika kuwa, Watumishi wa Idara hiyo siyo waadilifu, itawachukulia hatua za kinidhamu ikiwemo kuwaachisha kazi. Katika kutekeleza azma hii, naomba kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Watendaji wa Halmashauri kwa ujumla wao husimamiwa na Mabaraza ya Madiwani, ambamo Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe. Kwa hiyo, wana nafasi kubwa katika kuwasimamia watendaji hao chini ya Wakurugenzi wa Halmashauri ili Serikali za Mitaa zisaidiane na Serikali Kuu kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa watumishi wote wa Sekta ya Ardhi kuhakikisha kuwa wanatimiza majukumu yao kikamilifu na kwa uadilifu.

**MHE. NYAMBARI M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Pamoja na majibu mazuri ya Waziri lakini ifahamike kwamba Tarime migogoro ya ardhi ndiyo chanzo kikubwa sana kinachosababisha watu wanapigana mara kwa mara mpaka wanauwana. Je, Serikali itasaidiaje kupima baadhi ya maeneo ya Miji Midogo kama vile Silali, Nyamwaga, Nyamongo na Lusuti ili kupunguza migogoro kama hii inayotokea mara kwa mara?

(ii) Kuna baadhi ya watu pale Tarime wanaojiita vigogo walimilikishwa maeneo ya wanavijiji kama vile Ibaso na Nyandoto kinyume cha sheria; je, Serikali itasaidiaje kurudisha maeneo hayo kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999, wajibu wa kupendekeza upimaji wa ardhi katika eneo ambalo liko chini ya mamlaka ya vijiji ni jukumu la Halmashauri inayohusika ambayo itapendekeza kwa Kamishna wa Ardhi kwamba, eneo hilo lipimwe na wahusika kupewa miliki.

Mheshimiwa Spika, ningetoa wito kwa Mheshimiwa Mbunge kwamba, Halmashauri yake ifuate utaratibu wa kuleta mapendekezo ili maeneo hayo aliyosema kwamba yanahitaji kupimwa, yaweze kuingizwa katika mpango na hatma yake kupimwa na wananchi kumilikishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili juu ya wamiliki au wavamizi wa ardhi, Sheria ya Ardhi ambayo ni ya Mwaka 1999, kifungu cha 175, kinakataza mtu yeyote kuvamia na kutumia ardhi ambayo hajaruhusiwa kufanyia hivyo. Ningeomba Mheshimiwa Mbunge, atupatie orodha ya watu waliovamia ardhi katika maeneo yake ili hatua zifaazo ziweze kuchukuliwa.

Na. 48

**Kuwapatia Huduma Muhimu Wananchi Waliohamishwa Kipawa na Kinyamkera**

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA** aliuliza:-

Serikali iliwahamisha Wananchi wa Kipawa na Kinyamkera kwenda Ukonga, Kata ya Pugu, Mtaa wa Kinyamwezi ili kupisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wananchi hao wanapata mahitaji muhimu kama barabara, maji, umeme na kituo cha afya?

(b) Baadhi ya wananchi waliopewa viwanja walikuta vimeshauza kwa watu wengine; je, Serikali ina mpango gani wa kutoa viwanja vingine pamoja na fidia kidogo kwa wananchi hao ukizingatia wameshatumia fedha walizotegemea kujengea?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eugen Mwaisilinga Mwaiposa, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Ili kutekeleza mpango wa Serikali wa kupanua Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, wakazi waliokuwa wanaishi eneo la Kipawa walilazimika kuhamishwa ili kutoa nafasi ya upanuzi wa Kiwanja hicho.

Zoezi la kuhamisha wananchi hao lilifanyika kuanzia Septemba, 2009 na lilichukua takriban miezi miwili kukamilika. Wakazi wote waliohamishwa walilipwa fidia kwa mujibu wa sheria na kupatiwa viwanja vipya katika eneo la Pugu Kinyamwezi na Pungu Kajiungeni, Wilaya ya Ilala.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, iliwahamisha Wakazi wa Kipawa kwa ajili ya kupisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere. Katika kutekeleza azma hii, Wizara iliwasiliana na TAMISEMI kwa ajili ya kutenga maeneo ya makazi mapya. Upimaji wa viwanja hivi ulizingatia taratibu za mipango miji zikiwemo kutenga maeneo kwa ajili ya vituo vya afya, huduma za barabara, maji, umeme, masoko, michezo, maeneo ya kuabudia, kuzikia na hata vituo vidogo vya polisi. Hivi sasa barabara zimechongwa. Kwa kushirikiana na TAMISEMI, Wizara za Nishati na Madini, Maji na Wizara ya Afya, ni matarajio yangu kuwa huduma nyingine kama vile za afya, maji na umeme zitapewa kipaumbele na Wizara husika kwa kuzingatia uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, baadhi ya viwanja vilivyokuwa vimetengwa kwa ajili ya wakazi hao vilivamiwa na watu ambao siyo walengwa na hivyo kuleta usumbufu kwa wananchi waliohamishwa kutoka Kipawa. Ili kuondoa kero hii, Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, ilichukua hatua ya kuwaondoa wote waliovamia viwanja na kuvigawa upya kwa walengwa. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa sasa tatizo hilo limemalizika na wananchi waliohamishwa kutoka Kipawa wanaendelea na shughuli zao za ujenzi wa Taifa.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Waziri:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali kwa kipindi kirefu imekuwa na utaratibu wa kutathmini mashamba ya wananchi na kuwaacha kwa muda mrefu bila kuwalipa fedha zao na huku wananchi hawa wakiwa hawawezi kuendelea kuzitumia sehemu hizo kwa shughuli za kiuchumi; na kwa kuwa Serikali inajua kabisa kuwa hiki ni kinyume cha utaratibu na Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999:-

(i) Je, Serikali sasa iko tayari kusahihisha jambo hili kuweza kuendelea kuweka uhusiano mzuri kati ya Serikali na Wananchi?

(ii) Kwa kuwa wananchi waliohamishwa kutoka Kipawa na Kigilagila wanazidi 2,000; na kwa kuwa wananchi hao walihamia katika Mitaa mitano ya Kata ya Pugu wakiwa na watoto wao wanaosoma shule za msingi na watoto hawa wamejiorodhesha; na kwa kuwa Shule za Pugu kwa sasa na kwa ghafla idadi ya wanafunzi hao imeongezeka sana: Je, Serikali sasa iko tayari kusaidia jambo hili la dharura angalau kutupatia madawati kwa shule hizo ili kuwanusuru watoto wasiendelee kukaa chini?

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nikiwa nimesimama kwa mara yangu ya kwanza katika Bunge lako Tukufu, kwanza, naomba niwasalimie Wananchi wa Muleba na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala la ucheleweshaji wa fidia ni kero kubwa sana kwa Wananchi, ambayo sasa hivi Serikali na Wizara yangu, tuko mbioni kuhakikisha kwamba tunairekebisha.

Mheshimiwa Spika, ninawasilisha.

Na. 49

**Kusita kwa Huduma katika Bandari ya Lindi**

**MHE. SALUM K. BARWANY** aliuliza:-

Bandari ni lango la kibiashara na usafirishaji kote duniani, lakini Bandari yetu ya Lindi haitoi huduma zake ipasavyo kwa sababu ya kujaa mchanga na kusababisha Meli zisiweze kutia nanga Bandarini hapo na kusababisha mfumko wa bei kutokana na usafirishaji wa bidhaa kwa barabara ambao ni ghali sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuondoa mchanga kwenye Bandari ya Lindi na kuweka mazingira mazuri ili kuendelea kutumika na kuinua Pato la Taifa na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Serikali imezingatia mapendekezo ya utafiti uliofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kupitia Kampuni ya Hamburg Port Consulting ya Nchini Ujerumani mwaka 2009, ambao ulibainisha kuwa, mchanga unaojaa unasababishwa na kuwepo kwa mkondo wa maji unaoingiza mchanga karibu na gati. Utafiti huo ulipendekeza moja kati ya mambo mawili yafanyike: Kujenga upya gati lililopo na kuongeza urefu kwenda majini kwa mita 100 ili kuendelea kufunga meli zenye kina kifupi cha kuanzia mita nne. Awali meli zilikuwa zinafunga mita kumi kutoka kwenye gati kwenda majini; na kujenga gati jipya eneo lingine.

Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, ina mpango wa kujenga upya gati hilo ikiwa ni pamoja na kuongeza urefu kwa mita 100 kwenda majini kama ilivyopendekezwa na ripoti ya utafiti. Hatua za awali za maandalizi zimeanza ambapo kazi ya kupima *(Survey)* ili kukadiria gharama za Mradi ilianza mwezi Novemba, 2010 na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Februari, 2011 na hatua itakayofuata ni

kutafuta Mkandarasi. Kazi ya ujenzi imepangwa kuanza katika Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Je, Waziri yuko tayari kulieleza Bunge lako Tukufu hili taratibu zote za mchakato wa ujenzi wa Bandari hiyo ili Wananchi wa Jimbo la Lindi wajiridhishe kwamba, Serikali yao sasa imeliona hilo na kulifanyia kazi?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Salum Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu ya msingi, lakini ninakubali Serikali iko tayari kuwataarifu wananchi hivyo na kwamba, gharama na usanifu vyote tunakamilisha katika kipindi nilichokitamka.

Na. 50

**Matumizi ya Eneo la Uwanda Game Reserve**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliulliza:-

Sehemu kubwa ya ardhi ya eneo la Uwanda Game Reserve lililopo Tarafa ya Kipeta imemezwa na Ziwa Rukwa na kufanya wanyama na viumbe wengine kutoweka kwenye eneo hilo; na kwa kuzingatia kuwa wananchi wa vijiji vilivyopo kandokando ya eneo hilo hawana ardhi ya kulima na wanaojaribu kulima kwenye eneo hilo hukamatwa na kunyang'anywa mazao yao na askari wa wanyamapori:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiwaruhusu wananchi kutumia ardhi hiyo iliyobaki kwa shughuli za kilimo kwa sababu wanyama wameshatoweka?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa eneo hilo linakodishwa kinyemela na maafisa wanyamapori kwa baadhi ya watu kulima na kutoza fedha ambazo hazifikishwi Serikalini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mbunge wa Kwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Pori la Uwanda lililopandishwa hadhi na kuandikishwa kama Pori la Akiba kwa Tangazo la Serikali Na. 275 la Mwaka 1974, lina sifa nzuri za bioanuwai ambazo zinafaa kwa uhifadhi wa wanyamapori, hasa wakati wa kiangazi kutokana na uwepo wa unyevunyevu

unaosababishwa na mafuriko ya mara kwa mara kutoka Ziwa Rukwa, uwepo wa wanyamapori maarufu na adimu kama vile sheshe, twiga chotara na swala wa aina mbalimbali pamoja na kuwepo kwa madini aina ya magadi ambayo ni kivutio kwa ndege wa aina mbalimbali. Vilevile eneo hili ni mapito ya wanyamapori *(corridor),* hususan tembo kati ya Pori la Akiba Rukwa–Lukwati na Hifadhi ya Taifa ya Katavi. Hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa bioanuwai zilizoanishwa hapo juu, Wizara yangu inaona bado kuna umuhimu wa kuendelea kuhifadhi rasilimali zilizopo katika pori hilo. Eneo hilo pia ni kiungo muhimu katika ikolojia ya maeneo yaliyohifadhiwa ya Hifadhi ya Taifa ya Katavi na Pori la Akiba la Rukwa-Lukwati. Hivyo basi, uanzishwaji wa kilimo na makazi katika eneo lililopendekezwa utaongeza mwingiliano wa shughuli za uhifadhi na wananchi utakaosababisha migogoro kati ya wananchi na wanyama wakali na waharibifu.

(b) Kuhusu suala la Maafisa Wanyamapori kukodisha kinyemela baadhi ya wakulima na kuwatoza fedha ambazo hazifikishwi Serikalini; hili kama linafanyika ni kosa la jinai na ni kinyume cha Sheria na maadili ya kazi. Tunaomba wananchi watoe taarifa Wizarani au TAKUKURU ili pale tutakapofanikiwa kuwakamata tuweze kuchukua hatua za kinidhamu ikiwemo kuwafukuza kazi.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa eneo lote la Uwanda Game Reserve limezungukwa na vijiji ambavyo vimesajiliwa kisheria; na kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la wingi wa watu katika eneo lile hadi kusababisha wananchi kukosa mahali pa kulima na hivyo kulazimika kuingia kulima na hadi sasa hivi eneo lote limelimwa lina mazao; wananchi wanasubiri kusulubishwa wakati wa mavuno:-

Je, Serikali haioni kwamba ni muda muafaka kwa sasa kuitazama Sheria hiyo ili wananchi waweze kuwa huru kutekeleza Azimio la Kilimo Kwanza?

(ii) Ni lini Waziri atapanga ziara katika eneo hilo ili kwenda kujionea hali halisi jinsi wananchi wanavyopata shida na maeneo ya kulima? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, umeuliza maswali yako vizuri sana na kwa kifupi. Mheshimiwa Waziri na wewe ujibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ignas Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, niombe tu kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, maeneo haya yaliyohifadhiwa yana faida nyingi sana ambazo haziishii tu kwenye uwepo wa wanyamapori, lakini pia yanasaidia kurekebisha hali ya hewa katika nchi likiwemo suala zima la upatikanaji wa mvua.

Ninaamini kabisa kwamba, Tanzania ni kubwa sana, bado yako maeneo mengi ambayo yako nje ya hifadhi. Tukiwa na mipango mizuri ya matumizi bora ya ardhi, bado

tunaweza tukatumia ardhi yetu iliyoko nje ya hifadhi na hii iliyoko kwenye hifadhi ikaendelea kusaidia kuboresha *eco-system* na hali ya hewa ya nchi yetu. Utafika wakati ambapo kweli tutaona kabisa kwamba, ardhi iliyoko nje imekwisha na kwa sababu hii ni hifadhi, ndiyo hapo tutakapoamua kwamba hiki tulichokiweka kwa akiba sasa tukitumie.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kufanya ziara, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, mapema iwezekanavyo hasa baada ya Bunge hili, nitapanga ratiba ya kutembelea maeneo mbalimbali likiwemo eneo la Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA**: Mheshimiwa Mbunge, wewe kazi yako ni kumbana tu Waziri.

Na. 51

**Hali ya Unyanyasaji wa Kijinsia Nchini**

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Bunge letu Tukufu lilitunga Sheria ya Unyanyasaji wa Kijinsia; na mara kwa mara tunasoma taarifa mbalimbali kwenye vyombo vya habari jambo linaloashiria kuendelea kwa unyanyasaji wa kijinsia:-

(a) Je, tangu kutungwa kwa sheria hiyo Serikali imefanya tathmini au utafiti kuhusu hali ya unyanyasaji nchini kama imepungua au la; na kama bado; je, iko tayari kufanya utafiti huo kuona sababu za msingi hasa za unyanyasaji huo?

(b) Kabla ya utafiti huo; je, Serikali inachukua hatua gani za dharura kuona kuwa unyanyasaji unakomeshwa katika jamii yetu ili Watanzania wa jinsia zote waweze kunufaika na uhuru wa nchi yetu?

(c) Je, hali ya Tanzania ikoje katika mizania ya Dunia kuhusu unyanyasaji wa kijinsia; je, kuna taarifa yoyote inayoonesha kuwa nchi yetu ina kiwango gani cha unyanyasaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu**:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), ((b) na ( c ) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 1998 Bunge lako Tukufu, lilipitisha Sheria kuhusu Makosa ya Kujamiiana *(The Sexual Offences (Special Provisions) Act (SOSPA))* kama ilivyorekebishwa mwaka 2002. Sheria hii imefanya mabadiliko katika Sheria kadhaa nchini, ikiwemo Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania. Pamoja na kuwa hakuna tafiti rasmi zilizofanywa na Serikali kuhusu kuongezeka au kupungua kwa hali ya unyanyasasaji nchini, zipo taasisi mbalimbali zisizo za kiserikali

ambazo zimefanya tathmini ya sheria hii. Hata hivyo, Serikali hupata taarifa za matukio ya unyanyasaji wa kijinsia kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa yale matukio yanayoripotiwa kwao. Taarifa hizi zinaonesha kuwa kesi za ubakaji na ulawiti zimekuwa zikiongezeka kila mwaka badala ya kupungua.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tathmini za utekelezaji, Sheria hii ilifanyiwa mapitio na Tume ya Kurekebisha Sheria Mwaka 2009 ili kuhakikisha inakidhi malengo yaliyotarajiwa. Mapendekezo hayo yamewasilishwa kwenye Wizara husika kwa hatua zaidi. Hii inaonesha wazi kuwa, Serikali inafuatilia kwa karibu utekelezaji wa mafanikio ya sheria husika ili ikidhi matarajio ya jamii.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na tatizo hili. Hatua hizi ni pamoja na uzinduzi wa kampeni ya "Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto" uliofanywa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 24 Mei, 2008 na kuendelezwa kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru za mwaka 2009.

Serikali pia imeandaa Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto kuanzia mwaka 2001 hadi 2015, ambao pamoja na mambo mengine, mafunzo yanayohusu kuzuia ukatili wa kijinsia, yamekuwa yakitolewa kwa wasimamizi wa sheria wakiwemo Polisi, Mahakimu, Maafisa wa Magereza, Watendaji wa Vijiji na Viongozi wa Kimila.

(c) Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani *(WHO)*, ukihusisha mataifa mbalimbali, unabainisha kiwango cha ukatili wa kijinsia nchini kuwa ni asilimia 31 vijijini na asilimia 23 mijini. Hiki ni kiwango cha kati ukilinganisha na mataifa mengine duniani yaliyooredheshwa kwenye taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa, kuwepo kwa Sheria peke yake hakuwezi kuviondoa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia bali jitihada za pamoja zikifanyika katika kuielimisha jamii juu ya haki za binadamu, maadili mema na upendo, tatizo hili litapungua na kutoweka kabisa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Leticia Nyerere, kusaidiana na Serikali kuendelea kuwaelimisha wananchi katika maeneo yao ili waweze kutambua madhara ya vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia na kuviacha.

**MHE. LETICIA M. NYERERE**: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo mazuri, naomba nimuulize maswali mawili na nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Je, ni kwa nini vitendo vya ukeketaji vinaendelea nchini bila Serikali kuchukua hatua yoyote?

(ii) Ni kwa jinsi gani Serikali inawasaidia Wanawake walioathirika kisaikolojia baada ya kufanyiwa vitendo vya kikatili, kupigwa, kutukanwa matusi kwenye majukwaa na kunyimwa haki zao za msingi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Leticia Nyerere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba ifahamike kwamba, ukeketaji dhidi ya watoto ni kosa la kikatili na kosa la jinai. Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni ya Adhabu (Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania), inatoa adhabu isiyopungua kifungo cha miaka mitano na isiyozidi kifungo cha miaka 15.

Mheshimiwa Spika, nakiri kwamba, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya kuzuia vitendo vya ukatili dhidi ya watoto hasa katika baadhi ya Wilaya hapa Tanzania, lakini si kwamba Serikali imelala au haifanyi chochote.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mnamo Desemba 16, 2010, Mahakama ya Wilaya ya Tarime, ilimhukumu ngariba ambaye alihusika na kutaka kuwakeketa watoto wawili kwenda jela miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sio kwamba tumelala, ni kweli kuwakamata mangariba wote na wazazi wote ambao wamefanya hivi vitendo ni ngumu kwa sababu inahusisha ushirikiano mkubwa sana wa jamii mpaka na watendaji. Lakini tutaendelea. Naomba nitoe rai kwamba haitoshi kumaliza vitendo vya ukeketaji kwa kutumia sheria. Wizara yetu itaendelea kutoa hamasa kwa jamii, hasa tutawahusisha wanaume kwa sababu wao wanachangia kwa kiasi fulani wanapokataa kuoa watoto wasiokeketwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Leticia Nyerere, ni wazo zuri la kuwepo kwa vituo vya kutoa msaada wa kisaikolojia kwa waathirika wa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia. Lakini naomba niseme Serikali mpaka dakika hii haijaanzisha mpango huo, lakini tunashirikiana na wadau mbalimbali wanaotoa msaada wa kisaikolojia. Kwa mfano, *Women Legal Centre (WLC),* TAMWA wana kitu kinaitwa *Crisis Centre* kwa ajili ya wahanga wa udhalilishaji wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, nadhani umefika wakati jamii zetu kuachana na vitendo hivi vya kikatili dhidi ya watoto. Je, kuna umuhimu wowote wa kuendelea kuwakeketa watoto wa kike? Sidhani kama kuna umuhimu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Tulihitaji mwisho wa namna hii kwenye maswali, maana mlikuwa mmeshaanza kusinzia.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, naomba tuangalie kifungu 68(7), naomba kukisoma. "Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo kwa papo au baadaye kadri atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Spika, wakati nimeuliza swali la 48, wakati uliponipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, sikupata jibu la swali langu la pili la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Mwongozo wangu ni kwamba kwanza nakubaliana na wewe kwamba mimi ndio nilifanya makosa kwa sababu nilimwita Waziri ambaye hahusiki. Kwa hiyo, ukimwita Waziri ambaye hahusiki, atajibu kama alivyojibu. Kwa hiyo, hiyo tunaelewa utaweza kujibiwa wakati mwingine suala lako la nyongeza. *(Makofi)*

Tunaendelea, tunazo taarifa mbalimbali ambazo zimeletwa mbele yetu. Kwanza kabisa, tuna Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini - Mheshimiwa Januari Makamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kuwa kuna kikao kifupi cha Kamati leo tarehe 11 Februari, 2011 mara baada ya kipindi hiki cha maswali Ukumbi Na. 231. Kwa hiyo, wajumbe wale wapya wa Kamati hiyo waende chumba Na. 231.

Halafu mwenyewe nina tangazo, naomba kesho Waheshimiwa Wabunge Wanawake msikilize. Kesho saa 4.00 kwenye Ukumbi wa Msekwa, wanawake wote Wabunge naomba mkusanyike pale, tuna kazi moja ya kuwaeleza kuhusiana na kazi ya Chama cha Wabunge Wote Wanawake *(TWPG)*, halafu tunataka tueleze pia mafanikio yaliyoweza kupatikana kwa kipindi kilichopita na wakati huo huo kutakuwa ni kikao cha Uchaguzi. Kwa hiyo, naomba msikose kwa sababu ni muhimu sana katika maisha yetu ya miaka mitano hapa ndani. Kwa hiyo, naomba msikose kesho saa 4.00 kwenye Ukumbi wa Msekwa.

Halafu kuna Mheshimiwa Eng. Mohamed Mnyaa, yeye ni Kiongozi wetu wa Michezo, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Klabu ya Michezo ya Bunge *(Bunge Sports Club)* imeandaa fomu ya usajili wa michezo kwa kila Mheshimiwa Mbunge ambazo zimegawiwa kwa kila Mbunge. Hivyo mnaombwa kuzijaza na kuzirudisha mara moja. Aidha, wanamichezo, Waheshimiwa Wabunge wanaombwa kukutana siku ya Jumamosi tarehe 12 Februari, 2011 kuanzia saa 12.00 Uwanja wa Mpira wa Jamhuri kwa ajili ya kuanza mazoezi rasmi. Kwa hiyo, wote mkusanyike huko muanze mazoezi rasmi. Tulikubaliana kwamba mjaze fomu kuwaelekeza madereva wawachukue wapi, nadhani mlifanya hivyo. Usafiri wa

kuwachukua na kuwarudisha Waheshimiwa Wabunge kutoka sehemu wanakokaa utakuwepo.

Halafu nina Mheshimiwa Jenista Mhagama, yeye Katibu wa *Caucus* ya Chama cha Mapinduzi anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM wakachukue barua zao za uchaguzi ndani ya Chama. Ananiomba niwatangazie Wabunge kwamba Wabunge wa CCM wapitie katika Ofisi ya CCM hapa Bungeni ghorofa ya kwanza kushoto chumba cha mwisho ili wapatiwe barua zao zinazohusiana na uchaguzi. Kwa hiyo, kuna uchaguzi ule mwende mkachukue fomu au barua zenu.

Tangazo lingine ni la Tanzia, Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Kheri Khamis Ali, yeye ni Mbunge wa Jimbo la Kwamtipura Zanzibar, amefiwa na mama yake mzazi leo hii tarehe 11 Februari, 2011 huko Zanzibar. Utaratibu wa kuhakikisha anasafiri unaendelea kufanyika.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ndio mwisho wa matangazo, tunaendelea.

**MWONGOZO WA SPIKA KUHUSU TAARIFA YA DHARURA**

**SPIKA:** Taarifa gani ya dharura?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa mujibu wa kifungu Na. 47.

**SPIKA:** Nafahamu inasema nini taarifa yenyewe.

**MHE. ENG. STELLA M. MARTIN:** Ndio. Hapa karibuni tulipata taarifa kupitia vyombo vya habari juu ya udhalilishaji wa watoto katika eneo la Mwananyamala. Tunaomba Mheshimiwa Waziri anayehusika aweze kututaarifu ili tuweze kujua kwa sababu ni jambo ambalo linagusa jamii.

**SPIKA:** Pamoja na kwamba ni kweli taarifa hiyo tungependa kuipata, lakini sio taarifa ya dharura.

**HOJA ZA SERIKALI**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa, kabla sijamwita mchangiaji anayefuata, katika kipindi hiki tulikuwa tumepata barua kutoka kwa *Tanzania Federation of Disabled People Organisations*. Hawa wanaomba… Naomba niiache kwa sababu sijaipitia katika utaratibu unaohusika. Matangazo yake nitayatoa baadaye.

Kuna Chama cha Wafanyabiashara ambao wanaongoza *Foundation* ya kufanya kazi *Public and Private Initiative* walitaka kuonana na mimi leo, lakini nilifikiria kwamba kwa sababu ni kitu muhimu na Kamati zimeshaundwa nawaomba tukutane tarehe 13 saa 5.30 asubuhi katika ukumbi ambao nitawatangazieni baadaye na Wenyeviti wa Kamati zilizochaguliwa. Kwa sababu kama ni suala linalohusiana *Private Public*

*Partnership* ni vizuri hao Wenyeviti wangu kwa sababu wako kwenye *sector* mbalimbali wakakutana na hawa wageni, tukaongea pamoja halafu tuweze kukubaliana, kuliko mimi peke yangu kuongea na hawa wageni. Kwa hiyo, naomba Wenyeviti wote siku ya Jumapili saa 5.30 tukusanyike kwenye ukumbi ambao tutawaambieni jioni ili kusudi tuweze kuongea na hawa wageni. Hii nitaitangaza baadaye.

Tunaendelea na uchangiaji wa hotuba hii. Kama nilivyowaambieni, orodha ni ndefu, kuanzia Jumatatu Mawaziri wataanza kuzungumza humu katikati na wenyewe watapewa dakika kumi kumi tu. Kwa hiyo, nianze na Mheshimiwa Bura, sijui kama yupo!

Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Freeman Mbowe tulishamuacha jana kwa sababu alikuwa na dharura. Tafadhali endelea kuzungumza.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza nikiwa nazungumza mara ya kwanza rasmi tangu nimechaguliwa kuwa Mbunge wa Hai. Kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ameniwezesha kurudi tena katika nyumba hii baada ya kukosa kwa miaka mitano kwa majukumu mengine ya kitaifa. Kipekee, naomba niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Hai ambao walinichagua kwa mapenzi yao bila rushwa kurudi katika nyumba yetu hii.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni na ni Mwenyekiti wa Chama, ninaomba niwashukuru Watanzania wote walioshiriki Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Wametupa kura za kutosha, nyingine hatujajua zilipo, lakini kwa vyovyote vile, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa yote. Ninachopenda tu kuwahakikishia Watanzania ni kwamba tutawafanyia kazi, na Wabunge wetu wako salama na tunawaomba waendelee kutupa ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote, Wenyeviti wa Kamati zote za Bunge zilizochaguliwa na Waheshimiwa Wabunge wote kutoka vyama vyote. Ni matumaini yangu kwamba tutafanya kazi kwa ushirikiano mzuri. Sisi kama Kambi ya Upinzani tuko tayari kufanya kazi na Wabunge wote ila tunawaomba Wabunge watuelewe kwamba wasiwe na hofu kuhusu sisi na mkakati wetu na utaratibu wetu wa kufanya kazi. Tuvumiliane, tutaheshimiana na tutawapa ushirikiano wale wote wanaohusika kwa sababu tunajenga nchi moja, tusigombane bila sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kwenye hili, nimpongeze Rais kwa kuwa msikivu, na Rais anapofanya jema tutampongeza, Serikali yake inapofanya jema tutaipongeza na Chama chochote kitakapofanya jambo jema kwa Taifa letu, tutakipongeza. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu moja ya msingi sana, kuridhia mabadiliko au kuitafuta upya Katiba ya Nchi yetu. Hili ni jambo la msingi ambalo limesisitizwa na wadau wengi kwa muda mrefu na kwa kweli mchango wangu leo ningeomba zaidi nizungumzie jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, nitawaomba sana mnisikilize kwa sababu jambo hili ni kiungo cha Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya awamu mbalimbali ambayo kama Taifa tumepitia, ziko nyufa nyingi zimejengeka. Katiba ya nchi sio milki ya Chama chochote cha Siasa na hatuna sababu ya kupigana vikumbo kutafuta nani mmiliki kwa hoja ya Katiba, tuangalie tunakusudia kutengeneza Katiba itupeleke wapi. Ni ukweli ulio wazi kwamba Katiba haikuwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, haikuwa kwenye hotuba ya Rais na ilikuwa kwenye ilani ya Chama chetu na pengine vyama vingine. Lakini Mheshimiwa Rais aliona umuhimu wa jambo hili, akaamua kulichukua. Huu ni uungwana, ustaarabu na huo ni uongozi. Kwa hiyo, tuwaombe wenzetu walio Serikalini wajue kwamba CHADEMA ina hazina kubwa sana ya fikra na wanapoona kuna jambo lolote wanapenda kulipata kutoka kwetu wasiwe waoga kutu-*consult* kwa ajili ya msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani yetu ya Uchaguzi hatujaitafutia *Intellectual Property Right*, kwa hiyo, wana ruhusa ya kutafuta chochote ambacho wanafikiri kina maslahi ya Taifa, lakini wawe na uungwana mdogo tu wa ku-*acknowledge* kwamba wazo hili zuri tumelipata ndani ya CHADEMA na sisi tutawapa mawazo ya ziada.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, Katiba ikifanyiwa kazi vizuri inaweza ikajenga mshikamano wa Taifa, inaweza ikaondoa majeraha makubwa sana ambayo yameanza kujengeka kati ya Vyama vya Siasa na Serikali, inaweza ikaondoa makovu makubwa sana katika jamii ambayo yameanza kujitokeza hasa kwenye masuala kama ya dini, inaweza ikaleta mshikamano wa ajabu sana katika Taifa, ikatujengea uzalendo, tukakubaliana wote kwamba hii ndiyo Katiba yetu.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunaiomba Serikali na kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyokuwa ametoa tamko kwamba hii *process* ya kuanza mambo ya Katiba tuifanye haraka sana kwa sababu huu ndio ufumbuzi wa kudumu na wa muda mrefu wa matatizo yetu ya Taifa. Kupitia Katiba hii nina hakika tutapata fursa ya kutoa mapendekezo mbalimbali ya namna ya ku-*overhaul* mfumo wetu wa utawala kwa sababu mfumo wetu wa utawala kama nchi ndio chimbuko kubwa sana la matatizo yetu ya kiuchumi na ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, leo Serikali yetu au ukiangalia utaratibu wote wa utawala wa nchi uko kwenye Serikali Kuu, Serikali Kuu hii inazidiwa. Kwa hiyo, Mawaziri waliotoa kauli mbalimbali za kuelezea lakini kwa kweli Mawaziri wetu wanazidiwa na kazi kwa sababu tumechukua mamlaka yote ya nchi tumeyajaza katika Serikali Kuu Dar es Salaam. Ni vyema tunavyokwenda kwenye Katiba, tukaangalia sera ya CHADEMA inazungumza habari ya *decentralisation* kwa kupeleka mamlaka zaidi katika ngazi za chini na kupunguza mfumo mkubwa wa utawala juu, tukaurudisha kwa wananchi chini na maamuzi mengine yakafanyika chini tukapunguza mzigo kwa Serikali Kuu.

Leo Waziri mmoja wa Kilimo anazungumzia kilimo nchi nzima halafu mnasema kilimo ni *priority*. Sasa ni vyema katika kilimo tukarudi katika utawala wetu wa majimbo. Kwa hiyo, sekta nyingine za kijamii ama za kiuchumi zitarudisha mamlaka

yake katika ngazi za chini. Mambo fulani fulani makuu yakabaki katika *Central Government,* masuala kama ya Fedha, Uhamiaji na Mambo ya Ndani, Ulinzi na Usalama na masuala ya nchi za nje. Lakini kulundika kila kitu Dar es Salaam tunawaonea Waheshimiwa Mawaziri, wanakimbia kila siku na siku zote wanakuwa hawakamilishi majukumu ambayo wameyapanga. Kwa hiyo, naomba sana hilo Waheshimiwa tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba tuna hofu sana. Mimi naomba Waheshimiwa Wabunge msiwe na hofu. Mna hofu sana na kwa mujibu wa *survey* mbalimbali ambazo zimefanyika na kipekee pengine nizungumzie hii *survey* ya *Poverty and Human Development Report* ya 2007 inatoa takwimu za kutisha sana kwamba kati ya Watanzania wote hawaaminiani. Asilimia 78 ya Watanzania hawaaminiani. Kwa Dar es Salaam asilimia 85 ya wananchi hawaaminiani. Sasa wananchi tumejaza hofu, tunafanya mambo mengi kwa hisia ukiwaona watu wa Vyama vingine vya Upinzani unaona ni adui, ukiona watu wa Serikali unaona ni adui. Sasa vitu hivi ni vyema tukavijua kwamba kama Taifa tuna sababu sana ya kushikamana. Tuna matatizo mengi ya msingi ambayo tunastahili kushauriana na kusaidiana ili tulete neema kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana.

**SPIKA:** Nakushukuru wewe pia.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya pili kuzungumza leo. Lakini pia nachukua nafasi hii ya kwanza kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Lushoto ambao wameamua kwa dhati kabisa kunirejesha kama Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua muda ni mfupi, pengine nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri ambayo imejaa kina na ina maelezo mazito.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, namshukuru sana Waziri Mkuu kwa majibu yake ya jana ambapo aliulizwa maswali kwa dharura na aliweza kutoa majibu ya kina. Kutokana na majibu hayo, namshukuru pia leo mdogo wangu, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, amebadilika sana kutoa maelezo na kama atakuwa na tabia hii kwa kweli mimi sioni tatizo mahali popote lilipo. Naamini majibu ya Waziri Mkuu jana yaliweza kutoa picha halisi ya hali ilivyotokea Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara jirani na Arusha na pengine nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Arusha pamoja na Kamati yake ya Ulinzi kwa kudhibiti hali ile ambayo imesababishwa bila sababu yoyote kama alivyosema Waziri Mkuu. Mimi nafikiri kwa sababu tunajenga nyumba moja, basi tuepuke sana kutafuta umaarufu kwa kutumia migongo ya watu. Aliyoyazungumza ndugu yangu ni ya msingi na mimi nakubaliana kwamba tunajenga nyumba moja, ni

lazima tushirikiane na tusaidiane. Amezungumza kwa kifupi kwa sababu ya muda suala la *consultation*.

Mimi naamini kama Mbunge na naamini kama Chama cha Mapinduzi hatuwezi kukataa *consultations* ambazo ni *constructive*. Ukituletea yale ambayo ni ya msingi tutaelewa. Suala la kudandia hoja sio kweli. Maamuzi ya Katiba yameamuliwa katika Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Sasa hii inatoka wapi kuanza kusifiana kwa hoja? Tukishachaguliwa, tofauti yetu inakwisha humu ndani, wote tunashiriki kama Wabunge, hakuna aliye na hoja nzito wala hoja hafifu. Kila mmoja atazungumza kwa kutetea maslahi ya nchi yetu na maslahi ya wale anaowawakilisha ambao ni watu wa Jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachosema tu ni kwamba kauli hizi zilizoanza kutokea leo zikiendelea, hivyo kweli nina uhakika tutajenga Bunge moja, Bunge bora na Bunge la kuwatetea wananchi. Kwa ajili ya muda, nisingependa sana nijielekeze katika suala hili, lakini napenda tu nieleweke kwamba kwa kweli Upinzani ukiweza kuelewa wajibu wake kama Upinzani kutoa hoja za msingi, kuishauri, kuikosoa Serikali mimi sioni tatizo. Tatizo linatokea mtu mmoja kuonekana yeye ni kidume zaidi. Haturuhusu na pia kuijaribu Serikali, hatutaruhusu. Wewe unapowaambia watu twendeni tukawakomboe watu kwenye Kituo cha Polisi, haiwezekani!

Mimi nilikuwa Mkuu wa Mkoa tena namshurkuru sana ndugu yangu Shirima, ameweza kuituliza hali ile na kwa kweli mimi naikubali na napongeza sana Serikali. Hata mpaka leo wale waliosababisha wako nje na wanatamba na wamesabibisha vifo vya watu, lakini kwa sababu ya subira zilizoko ndani ya Rais wetu na Chama chetu cha Mapinduzi na Serikali yake. Vinginevyo hatua kali zingechukuliwa wale mpaka sasa hivi wangekuwa lupango. Katika utawala wangu kama *Governor* sikuwa mtu wa kuchezea. Nikisema nitafanya, nitafanya kwa mujibu wa Sheria lakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nije katika mchango. Nianzie kwenye vipengele vile vya vipaumbele. Kipengele namba tano. Kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ameliweka katika mipango yake suala la kutumia fursa ya kijiografia ya nchi yetu na kuifanya Tanzania kuwa lango kuu la biashara na usafirishaji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati. Mimi nianze kwa kusema kwamba Rais amefanya busara ameweka Wizara inayohusiana na uchukuzi. Mimi nafikiri wakati muafaka leo kufikiria uanzishwaji wa Reli iendayo kwa kasi, kwenda katika maeneo ya Kigoma, Mwanza, Shinyanga ili tuunganishe maeneo ya nchi yetu. Dunia yote leo ukitaka ujue maendeleo ya nchi angalia jinsi mwenendo wa shughuli za uchukuzi zinavyokwenda. Ukifika Heathrow Airport leo ndege zinavyopishana, zinapishana kama ndege za kawaida unajua uchumi wa nchi hii unakwenda. Ukienda Hong Kong meli zilivyojazana una uhakika kwamba nchi inakwenda, kwa sababu *movement* ya *cargo, movement* ya watu ndiyo kiashiria muhimu cha kuonesha uchumi wa nchi unaibuka.

Kwa hiyo, hili kwa mara ya kwanza Rais amelitamka, ninauhakika likisimamiwa vizuri na sekta inayohusika nchi itapanuka na itapasuka sasa hivi na tutaanza kulipa mikopo tunayodaiwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kwa sababu ya muda, nizungumzie kipaumbele kile cha 12 ambacho Rais amezungumzia suala la kuongeza mara dufu juhudi za kuhifadhi mazingira. Mimi natoka Jimbo la Lushoto, na Wilaya ya Lushoto kwa ujumla Kuna janga ambalo haliinyemelei Lushoto tu peke yake, lakini linanyemelea nchi nzima. Kutokana na uchafuzi wa mazingira, hivi sasa liko tatizo la uhaba wa maji katika vyanzo vya maji. Ukifika Lushoto sasa hivi maeneo mengi ya vyanzo vya maji vya asili vimekwisha na sio Lushoto peke yake ni nchi nzima. Nafikiri suala la mazingira kwa kweli lingepangiwa utaratibu kamili na ukatolewa mwongozo.

Kubwa lililotufikisha hapa ni kule kuvuna mali za asili hasa misitu bila kuangalia madhara ya baadaye. Lushoto ni nchi iliyojaa miti, lakini hata ile miti iliyokuwa imepandwa na Serikali yote imevunwa na leo kule ni wazi kabisa. Sasa nasema turudishe juhudi zile zile na tusaidie kutengeneza programu ya haraka. Mimi nina uhaba wa maji Lushoto eneo ambalo hatukutegemea kuwa hivyo. Maeneo mengi kulikuwa na maji yanabubujika, sasa yamekauka. Hili ni tatizo na ni kweli kwamba lazima tulichukulie hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa muda huu mfupi niliopata, napenda kurudia sana umoja wetu utajengeka kama tutaheshimiana kisiasa na kila mmoja akitii haki za kila mmoja na mimi nashauri na napenda kusema kwamba wenzetu Arusha wameonesha mfano, uwezo wa Serikali mpaka Mikoani ni mkubwa, msije mkathubutu. Ukijaribu, utakiona cha mtema kuni. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia uhai na uzima na leo hii mimi binafsi akaniwezesha kuwemo katika Bunge lako Tukufu kwa mara ya pili.

Pili, naomba nichukue nafasi hii niwashukuru wanachama wa chama changu pamoja na viongozi wangu wa Chama cha Wananchi *(CUF)* ambao wamenijalia wakaniona ninafaa kurudi tena katika Bunge lako Tukufu, Mwenyezi Mungu awazidishie imani.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba nikushukuru wewe na nikupongeze kwa Mwenyezi Mungu kukujalia kukupa nafasi hiyo kama mwanamke wa mwanzo na inshallah Mungu akuwezeshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze katika mambo matatu kama Mwenyezi Mungu atanijalia kutokana na dakika zenyewe. Suala la kwanza, naomba nizungumzie suala la afya. Hivi karibuni nimesikia taarifa kwenye magazeti kwamba kuna mama ambaye amejifungua kwa bahati mbaya sana Daktari aliagiza mama yule apelekwe kwenye Hospitali nyingine kwa ajili ya matatibabu zaidi, lakini muuguzi mmoja akamzuia na badala yake akapoteza maisha. Mama amejifungua mapacha, ana ukosefu wa damu, Daktari ameagiza lakini wakamzuia kwa sababu eti hajalipa Sh. 155,000/-. Jamani, muuguzi aliona bora Sh.155,000/= kuliko uhai wa mama huyu ambaye badala ya

kujifungua mapacha wale akaweza kuwalea pengine angeweza kutupatia mapacha wengine Taifa likazidi kuendelea mbele!

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali isimamie kwa kina kabisa suala hili na kuona tatizo lilikuwa wapi, na kama kuna mtu ambaye alidharau na kusababisha kifo cha mama huyu, basi ashughulikiwe ipasavyo. Ni jambo la unyanyasaji, jambo la kukiuka haki za binadamu, ni jambo la kukiuka haki za binadamu, na ni jambo la kuvunja sheria. Mama mjamzito siku zote humu ndani ya Bunge tunakuwa tukimpigia kelele kuhusu suala la mama wazazi na wajawazito. Juzi Mheshimiwa Waziri nilimsikia anazungumzia suala la kutafutiwa usafiri kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa na hawa wazazi, ila naomba kitu kimoja. Pamoja na Mheshimiwa Waziri kusema kwamba Wabunge walipiga kelele sana humu kwamba wanataka kupewa vibajaji Mheshimiwa akaweka sawa kwamba ni bajaji ambazo zitakuwa na muundo wa *ambulance*. Mheshimiwa nasisitiza sana kama tunaujua uchungu wa mwana, basi hiyo *ambulance* iwe *ambulance* kweli.

Kama tunaujua uchungu wa uzazi, tusione kama tunakwenda kumchukua mgonjwa na mgonjwa kama hali bado inaruhusu unaweza kumpakia kwenye bajaji. Lakini mzazi, *no!* Haiwezekani jamani! Lazima tuliangalie kwa umakini mkubwa suala hilo. Huwezi ukampakia kwenye pikipiki au bajaji au vinginevyo. Lazima apate *ambulance* ambayo itambeba yeye na muuguzi na mama anayekwenda kumsaidia pengine. Naomba sana tusilichukulie kimzaha suala la uzazi, sio suala la mzaha kabisa. Ni suala la kuliangalia kwa umakini mkubwa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa kina na Serikali ione umuhimu wa kuwatafutia wazazi *ambulance* waweze kuwafikisha Hospitali. Vinginevyo itabidi basi kule hospitali labda tuandae chumba cha dharura au *maternity waiting room* kabla hujapata uchungu ufike pale Hospitalini. Vinginevyo huwezi kukaa kwenye pikipiki ukaenda Hospitali kwa nia ya kujifungua.

Mheshimiwa Spika, naomba nije kwenye suala la elimu. Elimu yetu tunaiona inashuka kwa kiasi fulani kwa sababu hatufaulishi vizuri wanafunzi. Lakini kuna tatizo ambalo sijui kama Serikali inaliona. Tatizo la uhaba wa Walimu ni tatizo la uhaba wa Walimu ni tatizo kubwa ambalo linachangia kufeli kwa wanafunzi wetu. Huwezi ukawapeleka wanafunzi 100 darasani Mwalimu akawa na uwezo wa kuwafundisha na tukatarajia ufaulu.

Haiwezekani tumejenga shule nyingi za Kata, tunamshukuru Mwenyezi Mungu, tunaishukuru Serikali lakini shule hazina Walimu. Ukienda shuleni ukiuliza shule hii ina wanafunzi wangapi na walimu wangapi utaambiwa kuna Mwalimu mmoja. Masomo yanayofundishwa pale utakuta ni mawili au matatu kwa kujitahidi sana Mwalimu atafundisha masomo matatu. Mtihani unapokuja hauchagui shule kwamba shule hii ina Walimu au haina, shule hii masomo haya wamesoma au hawakusoma. Mtihani unaokuja ni mmoja, tunatarajia nini? Hawawezi kufauli. Kabisa haiwezekana mwanafunzi kufaulu bila kufundishwa. Mwanafunzi wa Chuo Kikuu ndiye anaingia darasani akapewa *lecture* kidogo ndiyo akaenda kutafuta mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda unakwenda, naomba nizungumzie suala la Muungano. Naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake na nalishukuru

Bunge hili kwamba tumekuwa tukipiga kelele sana kuhusiana na Muungano kwamba la msingi ni kuimarisha na kudumisha Muungano wetu, lakini kuna mambo ya kero za Muungano ambalo ni la muda mrefu, tunazitaja sana humu, Tume nyingi zimeundwa, kuna mmoja juzi alizitaja mimi sitaki nizitaje, nilikuwa Waziri kivuli wa Muungano, nimeshazitaja kero na nimeshazitaja sana Tume, lakini inaonekana hata Mheshimiwa Rais anapoagiza pengine watendaji wanakuwa hawashughuliki.

Naomba Kamati ambayo inakaa kushughulikia na kutatua kero za Muungano taarifa zake wazilete ndani ya Bunge hili Tukufu, kila kero ambayo wameipatia ufumbuzi wasingoje kuulizwa swali. Wakishafanya kazi, ripoti watuletee, jamani kero hii imepatiwa ufumbuzi. Pia naomba nishauri vyombo hivi, Baraza la Wawakilishi na Bunge ni vyombo muhimu sana, wanaweza sana kushughulikia kero hizi za Muungano. Kwa hiyo, naomba sana isifanye yale mambo yakawa siri kila taarifa wanayoifanya kazi watulitee wasingoje mpaka tukauliza maswali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kero moja kubwa ilikuwa ni Rais wa Zanzibar kuondolewa madaraka yake katika Serikali ya Muungano. Hiyo ni kero kubwa ambayo hadi leo haijapatiwa ufumbuzi. Lakini la pili ambalo linasababisha kero na sasa humu ndani ya Bunge limekuwa ni gumzo linazungumzwa kwamba Wazanzibar ni wachache. Kero hii inasababishwa na Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi wanapojaji Wabunge wa Viti Maalum kwa kutumia wingi wa kura wakati wakijua kwamba Wazanzibar tuko kidogo ni kosa moja ambalo linafanywa na hatimaye litakuwa ni kero.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Mheshimiwa Abeid Aman Karume walipounganisha nchi hizi hawakujali wingi wala uchache, hawakuangalia Wazanzibar ni kidogo au wengi au Watanganyika ni wengi, *no*! Waliangalia umuhimu wa kuwa wamoja. Sisi ni ndugu, tuna udugu wa asili tuungane pamoja na tukaunganishwa katika baadhi ya mambo bila kujali wingi au uchache wa Watanzania. Naomba sana Tume ya Uchaguzi nayo iangalie namna gani ya kurekebisha Sheria ya Uchaguzi katika kuangalia wingi wa kura katika kugawa Wabunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante. Ile ya kugawa Viti Maalum kufuatana na kura zinazopatikana sio Tume, ni Sheria tuliyotunga sisi hapa na Katiba. Kwa hiyo, mchakato unaokuja basi mtafanyia kazi nalo hilo kama ni lazima.

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nitumie fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa rehema zake nyingi alizotujalia na pia nikushukuru wewe na kukupongeza kwa nafasi uliyonayo kwa kukiongoza chombo hiki kikubwa na kuandika historia ya akina mama Watanzania kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais imekusanya mengi na mazito yenye umuhimu wa aina yake kwa maslahi na faida ya nchi yetu. Mheshimiwa Rais

ametaja vipaumbele 13 kwa namna alivyoviona na vyote vina lengo la kupunguza umaskini wa Mtanzania na kumnyanyua kiuchumi. Katika vyote hivyo, naomba nigusie vichache tu navyo kwanza nianzie sekta ya kilimo. Tunaelewa wazi kwamba Watanzania wengi wanaajira kupitia kilimo.

Kilimo chetu bado kinakabiliwa na changamoto nyingi na nadhani nishauri tu kwa haraka haraka na mengi yameshasemwa juu ya kilimo, lakini niseme Mapinduzi ya Kilimo kwa kupata zana za kileo hili litachukuliwa hatua kwa taratibu. Lakini kwa maeneo yale ambayo mifugo kwa kutumia wanyama kazi ipo nadhani tusikae nyuma kwa kusubiri matrekta ambayo yatatugharimu na kupatikana kwake na kuyaeneza Tanzania nzima muda hautatusubiri.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunakabiliwa na hali ambayo hatuwezi kui-*control* kabisa. Ni mabadiliko ya hali ya hewa. Mabadiliko ya hali ya hewa yanakuja wakati wowote na nadhani tujipange kukabiliana na hiyo hali kwa kuweka mbegu zetu bora, mbegu hizi ziwe za muda mfupi, mbegu ambazo zitakuwa zinachukua uhimili wa wadodo waharibifu vilevile maradhi na tuangalie kwamba tunahitaji mbegu ambazo zitakuwa zinazalishwa kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, kuna Mikoa yetu ambayo wenzetu wamebahatika kuwa na mifugo mingi, lakini tunahitaji mifugo ambayo itakuwa na tija badala ya kuwa na mifugo mingi hawafaidiki nayo. Hapa Waheshimiwa Mawaziri wenye dhamana wa taasisi hizi sasa wajipange kuona kwamba mifugo yetu inaleta faida ndani ya nchi hii, tunakula nyama, tunauza ngozi lakini pia tunawatumia kwa kuleta maendelo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tuna maeneo yetu ambayo watu wetu wanatumia maziwa kwa ajili ya uvuvi (maziwa haya siyo yale ya ng’ombe, ni maziwa ya maji na Bahari ya Hindi iliyotuzunguka). Sasa hivi tunazunguka kufukuzana na wavuvi wa maeneo haya kwa kutumia mitego ambayo haistahiki, inaharibu mazingira ya maeneo hayo. Tutaendelea kufukuzana nao hao wavuvi, lakini lazima tutafute mbadala, badala ya kutumia mitego ambayo haina faida waweze kutumia mitego ambayo italeta tija. Lakini, tusisahau sasa kwamba hawa wanatafuta riziki halali. Ili waweze kuipata riziki hiyo, tufanyeje? Uwezo wao ni mdogo, umaskini ni mkubwa. Lazima tutafute namna basi ya kuwawezesha kuvua bila kuharibu mazingira hayo, lakini na wao wapate riziki stahiki.

Mheshimiwa Spika, suala la uwekezaji katika taasisi hizi, nadhani tulenge Watanzania wenye uwezo waweze kuwekeza katika sekta za kilimo, mifugo na hata uvuvi. Nadhani tujenge mazingira sasa ambayo waone kwamba iko haja badala ya wafanyabiashara wetu wengi kukimbilia kule Thailand, labda kwenda Hong Kong kutazama biashara za namna hiyo, lakini kumbe wanaweza wakawekeza ndani ya nchi hii, tukapata ajira kubwa kwa vijana, akina mama wakafaidika, mazao yetu ya kilimo na mifugo yakaweza kwenda kwenye viwanda vyetu na viwanda vikaweza kuleta faida tena kurudisha kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, ndani ya kilimo, mifugo na uvuvi tunaweza pia tukapata mbolea ambayo mazao yatakayotoka huku yatapata soko zuri katika hoteli zetu za kitalii.

Kwani tunavyofahamu wageni wetu hawa wanaokuja, mazao yanayotokana na mbolea za chumvi hayana soko kwa wenzetu. Hivyo, ni vyema tuweze kutumia sekta hizi, mazao haya kupata faida.

Mheshimiwa Spika, haraka haraka, nataka niseme alilozungumzia Mheshimiwa Rais; Umoja wa Watu! Mheshimiwa Spika, neno hili lina umuhimu wake wa kina kirefu sana, lina thamani kubwa tunapokuwa nalo na lina gharama nzito tunapolikosa.

Mheshimiwa Spika, umoja wa watu uliopatikana Zanzibar leo umetugharimu sana. Nakuomba sana na Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba kilichopatikana Zanzibar sasa hivi wakithamini, ni thamani kubwa, ni heshima ya nchi hii, ni heshima ya Watanzania popote pale walipo, sio suala la kubeza kamwe. Umoja hautopatikana pale palipoondoka amani na utulivu. Umoja bila kupendana, umoja bila kushirikiana, umoja bila kushikamana hautokuwepo. Lakini, tunapokuwa tunakejeliana juu ya dhana ile iliyofikiwa, nadhani tutakaa mahali pabaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tushukuru sana kwa Mwenyezi Mungu na tuwapongeze viongozi walioweza kukaa wakaliona lile. Mheshimiwa Rais Mstaafu, Dr. Karume, Katibu Mkuu wa *CUF*, Malim Seif Shariff Hamad, Mungu awajape umri. Wale waliosaidia, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, hotuba yake ya tarehe 30 Desemba kwa Bunge la Tisa, Mheshimiwa aliumia na akasema anasononeshwa na hali ya kisiasa Zanzibar. Ilikuwa ni hali ya kutisha, hali ya aibu, nchi ile ilizaa Wakimbizi, ni aibu kwa Taifa hili. Leo yale yamekwisha, yamesahaulika, nadhani sasa ni wajibu wetu kusimama pamoja kushikamana tukajenga heshima Mungu aliyotujalia badala ya kukebehi na kujeli.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wako nauheshimu sana, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyeniwezesha kufika hapa. Lakini pia nawashukuru sana wapigakura wangu akina mama wa Mkoa wa Dar es Salaam walioniwezesha kufika hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba nami, kwa sababu ni mara ya kwanza nisimame hapa, basi nikupongeze wewe kwa kuwa Spika wa kwanza mwanamke. Namwomba Mwenyezi Mungu akuzidishie, akupe kila lililokuwa la heri katika kuendesha Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba yake nzuri na mwelekeo. Nina hakika ni baada ya kazi nzuri ya miaka mitano wakaona wamchague tena na kweli wameona jinsi alivyojipanga kuweza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya chama chetu pamoja na kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata mafanikio. Ninampongeza sana. Mpango wa Baraza la Mawaziri inaonekana fika kabisa kwamba Serikali imejipanga vizuri sana katika kutekeleza vipaumbele vyote 13 ambavyo ameviweka.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nimpongeze Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa subira, kwa sababu hapa katikati pamekuwa na vuguvugu kubwa sana, migomo na kila aina ya fujo. Lakini, Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri Mkuu wamekuwa na subira na hatimaye leo tunaona kama subira inataka kuzaa matunda kwa maneno ambayo Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani aliyoyatoa kwamba yanatoa matumaini badala ya kusema kwamba nchi isitawalike, sasa tunasema itawalike na ifanye kazi ambayo wananchi wanaitarajia. Tunatarajia kuanzia leo tutakuwa wamoja na wote tutafanya kazi ambayo tumetumwa na wananchi wa Tanzania kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niangalie vipengele vitatu, vinne katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Naomba nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuanzisha na kubuni mkakati wa Kilimo Kwanza. Tunafahamu sisi sote kwamba asilimia karibu 80 ya wananchi wa Tanzania wanashughulika na masuala ya kilimo ikiwa ni pamoja kulima nikimaanisha na ufugaji. Ninampongeza Rais kwa kuliona hilo na kusema kwamba sasa hivi kutakuwa na Benki ya Wakulima kwa sababu wakulima kwa kipindi kiredu sana, mimi ni mkulima mmojawapo, tumekuwa tukihangaika mahali gani pa kwenda kutafuta unapoweza kupata mkopo ili kujiendeleza kwa wote wenye mashamba makubwa na wenye mashamba madogo madogo.

Mheshimiwa Spika, nafikiri sasa hivi itakuwa ni fursa nzuri ya kuweza kuendeleza kilimo chetu. Nami naomba Serikali katika mipango yake iangalie wakulima wote. Tunaposema ukulima wa kumwagilia maji, basi uwaguse mpaka wale wakulima wadogo na tuwatumie wakulima wakubwa kuwasaidia wakulima wadogo kwa sababu huyu mkulima ambaye amezoea kulima na jembe na kuangalia rehema ya Mwenyezi Mungu ya maji, lini mvua itanyesha, ndiyo kama tunavyoiona kwamba sasa hivi kila unakopita mazao yamekauka.

Ili kuhakikisha kwamba basi matunda hayo yanapatikana kwa wote, basi tusiwasahau wakulima wadogo wadogo, tufanye kila njia ili kusudi na wenyewe washiriki.

Mheshimiwa Spika, tukitumia Kilimo Kwanza, tunaweza tukaondoa hata ukosefu wa ajira kwa vijana wetu. Vijana wengi sana sasa hivi hawana ajira. Nikisema vijana ninamaanisha wanawake kwa wanaume. Kilimo Kwanza inaweza ikatoa jawabu kwa sababu gani, kama Serikali inaweza ikaandaa mpango ambao wanaweza kuwatayarishia mashamba kwa sababu kumwambia kijana sasa hivi nenda kalime wakati hana mtaji, hana ardhi, hajui ataanzia wapi, inaweza kuwa ni mtihani mkubwa sana.

Lakini ikiwa Serikali itajipanga, tunaweza tukaondoa ukosefu wa ajira kwa vijana wetu kwa kuwatayarishia mashamba na kuhakikisha wamepewa sehemu za kuweza kulima na kuwapa mbegu bora. Lakini, siyo hilo tu, nilikuwa ninaangalia suala zima la ukulima kwa akinamama. Sisi wa mijini, kwa kweli hatuna mashamba na kama tunayo ni *vihamba* vidogo vidogo. Lakini tunao ukulima wetu ambao ni mkubwa ambao ni ufugaji wa kuku wa kisasa na wa kienyeji. Ninaomba suala hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya muda, ninaomba vijana hawa ambao wanamaliza vyuo, elimu yao na vyeti vyao ndiyo iwe dhamana ya mikopo ambayo wanaweza kupewa ili waweze kufanya shughuli za kujikimu.

Mheshimiwa Spika, nataka nisimalize kabla sijagusia elimu. Napongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuangalia suala la elimu. Kwetu sisi tunasema kwamba gari liko njiani, unajiuliza umewekewa chai na mkate, uanze nini? *"Uanze Sai, uanze nkate?"* Unatakiwa uanze chai kwa sababu mkate utakwenda kula ndani ya gari. Ndiyo Serikali ilichofanya ni kwamba shule zimejengwa, wasingeweza kufundisha walimu ambao baadaye watakwenda wapi? Kungekuwa na maneno kwamba wametumia hela nyingi, wamefundisha walimu, hakuna mahali pa kupeleka. Lakini, sasa hivi tumekunywa chai, sasa tunatafuna mkate wakati tuko ndani ya gari, walimu wanafundishwa. Nina hakika kwamba sasa hivi kwa maneno tuliyoyasikia kwa Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake, basi walimu wanakuja.

Mheshimiwa Spika, naomba nigusie kidogo kuhusu amani kabla *time* yangu haijakwisha. Amani jamani na maadili ya kwetu, sasa hivi vijana wengi wamekosa maadili. Sisi humu ndani ya Bunge na wazazi wanaponisikia ninawaomba tuwarudishe watoto wetu katika maadili. Tanzania hatuna jadi ya watoto kuwatukana wakubwa, kudharau wakubwa. Kwa hiyo, mimi ninaomba hizi ni tabia ambazo sisi wazazi tunaweza tukakemea na tunaweza tukarudisha maadili ya watoto wetu wakarudi kule ambako tulikuwa. Siyo jadi ya Watanzania watoto kufanya fujo, ni kisiwa cha amani, tusichoshwe na amani. Baba wa Taifa alituambia tusichoshwe na amani, hiyo ndiyo nguzo yetu kubwa. Ninaomba ndugu zangu tuendelee. Kambi ya Upinzani leo imetoa tumaini, natumaini watawaambia vijana hii njia mliyokuwa mnatumia siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hotuba hii ya Mheshimiwa Rais wa nchi yetu. Kwanza kabisa na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa jinsi ambavyo amenijalia kurejea hapa Bungeni kwa awamu nyingine tena ili niweze kuwatumikia wanawake wa Mkoa wa Manyara walionipa ridhaa ya kunipigia kura.

Mheshimiwa Spika, naomba kabla sijaanza kutoa mchango wangu, nimshukuru sana kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ufafanuzi wa swali langu kwake jana la kuwaelewesha Watanzania kilijadili katika vurugu zilizotokea Manispaa ya Arusha. Ni dhahiri kwamba wananchi wengi walikuwa hawaelewi na nimeona hivyo kwa sababu wengi wamenipigia simu, wengine wameniletea meseji kushukuru katika kuelewa hili jambo ambalo kumbe Watanzania wengi hawalielewi. Kwa nafasi hii, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu jambo hili linaweza kuleta amani na uelewa na kuweza kuendelea vizuri katika chaguzi zetu nyingine zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yangu mengine ya utangulizi, kabla sijachangia, naomba pia kutanguliza kuomba ufafanuzi kidogo kuhusu ushiriki wa wanawake Wabunge wa Viti Maalum katika mikutano ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu Wabunge wa Viti Maalum ni sehemu kubwa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika kutekeleza pamoja na vipaumbele ambavyo ametuwekea Rais wetu katika hotuba yake. Bajeti zote zinazotengwa za fedha za Serikali zinapitia Halmashauri na kwenye Manispaa zetu. Lakini, kinachoshangaza ushiriki wa Wabunge wa Viti Maalum katika mikutano ya Kamati ya Fedha tunambiwa kwamba haturuhusiwi isipokuwa Wabunge wa Kuchaguliwa. Sasa nadhani kuna haja ya kuweka ufafanuzi kidogo kwa sababu sisi Wabunge wa Viti Maalum pia baadhi yetu naona wa upande wa Chama cha Mapinduzi ni Wabunge wa Kuchaguliwa. Sio hivyo tu, tunapaswa pia kushiriki katika kugawa ama kuelekeza fedha za miradi katika miradi mbalimbali ambayo inaweza ikawasaidia wanawake zaidi na wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kuchangia haraka haraka hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nimeainisha maeneo machache na nitachangia kwa kifupi nikianza na sekta ya kilimo. Katika sekta hii, mengi yamezungumzwa. Suala la Kilimo Kwanza mimi naliunga mkono kwa asilimia 100 kwa sababu binadamu anaweza akaishi hadi miaka 100 bila kuwa na elimu, lakini hawezi kukaa hata kwa wiki mbili bila kuwa na chakula. Kwa hiyo, naamini kabisa Rais ameweka kipaumbele muhimu sana ambacho tunapaswa sisi sote tumuunge mkono ili tuweze kupata chakula cha kutosha kwa wananchi wetu na tusiwe na dharura za hapa na pale kutokana na hali ya njaa.

Mheshimiwa Spika, na katika sekta hii vile vile, naomba kusisitiza tu eneo hili la uwajibikaji hasa kwa Maafisa Kilimo, Maafisa Ugani ili kila Afisa Ugani au Afisa Kilimo ambaye atawajibika ipasavyo katika eneo lake, tunaweza kuachana na tatizo hili la njaa la kila wakati na uzalishaji wetu ukaongezeka.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la elimu, mengi yamesemwa, nisingependa kurudia suala la *division zero* kwa sekondari zetu za Kata. Lakini, nataka kutoa mfano mdogo tu kwamba *division zero* siyo sawa na kutosoma kabisa. Nina ushahidi wa wanafunzi kadhaa ambao wamepata *division zero* lakini wamekwenda kwenye shule za VETA, za ufundi wamefanya vizuri sana. Huwezi kumtoa mtoto ambaye hajasoma kabisa ukampeleka VETA akafanya lolote. Lakini yule aliyepata *zero* kwenye sekondari zetu kwa sababu nyingi ambazo sitaki kurudia, anaweza akafanya vizuri katika eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, sio hivyo tu, hizo *division zero* zinatokana na mambo mengi ambayo ni nje ya uwezo wa wanafunzi hao ambayo yakirekebishwa kwa muda muafaka, shule zetu hizo zinaweza zikarekebishika vizuri na wanafunzi wetu wakafaulu.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nichangie kidogo kwa upande wa Vyuo vya juu katika sekta ya elimu. Nadhani hakuna mzazi ambaye angependa mtoto wake aliyeko Chuo Kikuu akajihusisha kwa undani kabisa na masuala ya siasa. Siasa katika Vyuo Vikuu inashusha kiwango cha elimu kwa sababu wanafunzi watachukua muda mwingi sana kujadili masuala ya siasa na itikadi za hapa na pale na inaweza ikazua vurugu. Kwa hiyo, kwa nafasi hii ningeomba kabisa wanaotumia wanafunzi wa Vyuo Vikuu

kuhamasisha itikadi zao za siasa, mimi ningeomba Wizara iangalie upya ili kuweza kuona ushiriki wa siasa ni kwa kiasi gani katika Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, nichangie kidogo pia katika eneo la viwanda. Katika hotuba ya Rais, tumeona kwamba sekta ya viwanda inakua kwa asilimia tisa na mchango wake ni asilimia nane katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni dalili nzuri na ni dalili ya kuonyesha kwamba sasa uchumi wetu unaanza kutoka pole pole kutoka kwenye kilimo kuelekea kwenye viwanda ambayo ndiyo inaweza kuwa sasa uchumi endelevu na kwa hiyo, naomba tumuunge mkono Rais na kuweza kufufua viwanda.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Rasilimali ambayo inatumika kutoa mikopo kwa ajili ya viwanda au kufufua viwanda, basi iendelee kufufua vile viwanda vilivyokuwa vimekufa na zaidi sana naomba kukumbusha kiwanda maarufu cha *General Tyre*. Kile kiwanda ni kiwanda muhimu sana kwa nchi yetu, lakini sisi tunaopita eneo lile tunaona ni magofu, hatujui kinachoendelea. Kama kuna mpango ambao upo wa kufufua viwanda vya ndani, basi kiwanda cha *General Tyre* kiweze kuwa kiwanda mojawapo ambacho Serikali itakipa kipaumbele katika kukifufua.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii tunashukuru kwamba ni sekta ambayo inatuletea kipato katika nchi yetu na tumeainishiwa kwamba imeingizia Taifa dola milioni 4.9. Lakini, hii yote ni juhudi ya kuweza kutangaza utalii katika nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kutangaza utalii katika nchi nyingine ni jukumu la kila mtu na naamini kila Mtanzania akiweza kutangaza utalii wa nchi yetu, vivutio vingi tulivyonavyo Tanzania, sisi Tanzania tungeweza kupata kipato kikubwa zaidi kuliko hiki ambacho tunacho sasa hivi. Kwa hiyo, naiomba Serikali na Watanzania wote tuweze kuitangaza nchi yetu na vivutio vyetu zaidi nchi za nje ili tuweze kusukumu sekta yetu ya utalii na kuongeza kipato kwa ajili ya pato la letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya juhudi katika kuwezesha wananchi kiuchumi, *SACCOS* zimeanzishwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na *VICOBA* na taasisi nyingine ndogo ndogo za fedha tunaishukuru Serikali kwa sababu juhudi kubwa inayowekwa na wananchi katika kutekeleza azma hiyo na kujiongezea vipato imeweza kuongeza vipato vya wananchi wa vijijini na kupunguza makali ya umaskini.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna tatizo kubwa kwamba suala hili la kushughulika na fedha haliwezi kwenda bila benki vijijini. *(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Moshi Kakoso na Mchungaji Mwanjale ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii ya kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri sana, lakini pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Kisesa kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao, niwaahidi kwamba sitapumzika hadi maendeleo ya kweli yapatikane Jimbo la Kisesa.

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda, nami niendelee kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Katika kipengele Na.7 ambapo Rais ameainisha kipaumbele kile cha kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za umma. Kama nilivyozungumza jana kwamba tuna tatizo kubwa la matumizi yasiyoleta mabadiliko kwa wananchi wetu, sasa utashangaa kuona nchi maskini kama hii mwaka 2009/2010 tuli-*budget* asilimia 35 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo ni sawa sawa na trilioni 3.3. Mwaka 2010/2011 bajeti hii tuliyonayo tumebajeti asilimia 33 ya mapato yote ya nchi kutumia mapato ya kawaida ambayo ni sawa sawa na trilioni 3.8.

Mheshimiwa Spika, matumizi haya ya fedha ni makubwa mno kwa nchi maskini kama sisi, sasa ni jukumu letu kujipanga kuona kwamba haya matumizi ya kawaida tunayashusha kwa nguvu zetu zote, matumizi haya ya kawaida yanaweza kushuka hata yakafikia asilimia 20, bado nchi itakwenda. Wakuu wa nchi wanahangaika sana, Waziri Mkuu ni mdau mkubwa sana katika zoezi zima hili la kupunguza matumizi ya Serikali, lakini ni kazi ngumu sana kama ile ya kusema watu wanapotaka kuomba warsha mpaka wamwandikie ki-*note* Waziri Mkuu, wanapotaka semina, wanapotaka kununua magari, hii kazi itakwisha, sisi tukiwawekea fedha kiduchu, hawana namna ya kufanya, huwezi ukanunua gari ya kifahari wakati umepewa fedha ya kununua gari aina ya *Landcruser* au bajaji.

Kwa hiyo, zoezi zima hapa bila hata Waziri hatahangaika na kupitisha vibali, tunasema kwamba semina tumekuwekea milioni moja, kwa hiyo, kama wewe utafanya semina moja hela ziishe shauri yako.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine lililolisisitiza sasa litolewe agizo maalumu kwamba Wizara zitakapokuwa zinawasilisha pamoja na taasisi zake, zitakapokuwa zinawasilisha bajeti kwenye Kamati husika lazima ziende na *details* za nini walichokusudia kufanya badala ya hivi sasa ambapo bajeti zinakuja zimeandikwa tu posho ya kujikimu milioni 200, mnajikimu mkiwa mnakwenda wapi? Tuone *details* zake.

Mheshimiwa Spika licha ya mapato kupanda, mapato ya Taifa yamekuwa yakipanda mwaka hadi mwaka, makusanyo yetu ya ndani yamekuwa yakipanda mwaka hadi mwaka, lakini fidia ya vyanzo vya mapato ya fedha zinazopelekwa Halmashauri ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa imebaki hivyo hivyo, leo miaka zaidi ya kumi iko vile vile. Matumizi ya Serikali huku yanapanda, lakini fidia ya mapato ya Halmashauri iko vile vile mpaka leo. Kama toka mwaka 1997 Halmashauri inapelekewa milioni 300

mpaka leo, mambo mengi yamebadilika, uchumi umebadilika, gharama zimebadilika, bidhaa zimepanda bei, mafuta yalikuwa Sh. 500/=, leo yananunuliwa Sh. 2,000/=.

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya mapema kwa sababu tunakwenda kwenye bajeti. Fedha hizi sasa angalau Halmashauri zote fidia wanazopelekewa iwe mara mbili yake. Kama Halamashauri inapelekewa fidia ya shilingi milioni mia nne basi iwe Sh. 800/= wakati tunatafuta uwiano sahihi wa kutoka kipindi kile mapato yetu tulipokuwa tunakusanya wenyewe na leo, sasa iwe mara mbili.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu aliniahidi katika maswali yangu mbalimbali kwamba Wenyeviti wa Vijiji sasa nao watalipwa, Madiwani wetu posho wanalipwa Sh. 120,000/=, ni aibu! Wakati fedha nyingi zinatumika *Central Government* kwa matumizi ya kawaida lakini kule Halmashauri Madiwani wetu wanaofanya kazi zetu za kila siku tunamlipa posho ya Sh. 120,000/=, hii ni aibu. Madiwani wetu tuwabadilishie angalau hata kwa kuanzia sasa hivi wakati tunaangalia tuwalipe kiasi gani, lakini hebu tuanzie na hiyo Sh. 300,000/= basi kwa mwezi, lakini Wenyeviti wetu wa Vijiji nao wapate hiyo Sh. 120,000/=.

Mheshimiwa Spika, tunapanga miradi mingi, mtu wa kwenda kutekeleza ni Mwenyekiti wa Kijiji, ndiye anayesimamia maendeleo, ndiye mlinzi wa amani katika kijiji husika, mtendaji wake analipwa, lakini na yeye anaacha familia yake kwa ajili ya shughuli za umma kila siku. Maskini wa Mungu hana mshahara, anafanya kazi ya dini, inawezekanaje sasa?

Mheshimiwa Spika, muda umekwisha, lakini naomba niongelee suala la kukuza uchumi ambacho ni kipaumbele namba mbili. Ni suala la kujiuliza tu kwamba tunapotaka kujiondoa kwenye umaskini hapa nchini tunafikiria nini? Maskini ni akina nani? Wapo wapi na wanafanya nini? Tukishajua hivyo, hatutapata matatizo. Katika Maputo *declaration* nchi zote wanachana tulikubaliana kutenga fedha asilimia kumi kwa ajili ya mkulima, lakini kama alivyoongea Rais mwenyewe kwamba kiwango hicho hatujakifikia lakini sababu za kwanini hatujakifikia, nadhani hatujafikia tu kwa sababu hatutaki kufikia. Naomba sasa kwenye bajeti hii tunayotarajia kuianza sasa tusiwe tena na *story*, asilimia kumi zote ziende kwenye kilimo. Tena kwenye *investment* ya kilimo hasa, siyo tena kwenye mambo ya matumizi ya kawaida, ziende zika-*invest* kwenye kilimo. Wenzetu walioamua ku-*invest* kwenye kilimo sasa hivi wana hatua kubwa. Korea wana ni 10.2%, Thailand asilimia 8%, sisi tunacheza na asilimi 2.4 mpaka asilimia tatu ambazo ni fedha kidogo sana. Hizi ukiangalia zimekwenda wapi? Kwenye kilimo! Sana sana ni mishahara na mashamba darasa, lakini ni ngapi zinakwenda kwenye *investment* ya kilimo? Ni kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji, ekari milioni 29.4 lakini eneo linalomwagiliwa ni ekari 283,245 peke yake sawa sawa na asilimia 0.1. tuamue sasa tuwekeze kikamilifu katika suala zima la umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nashauri sheria mbovu zifutwe. Sheria nyingi tunazowapelekea wakulima wetu ni zile tu zinazowapa kero, kwa mfano, sheria ile

inayomzuia mwananchi kuchanganya mahindi na pamba ifutwe, imepitwa na wakati, na hakuna utafiti. Nimeangalia, hakuna utafiti wowote unaothibitisha mpaka sasa hivi kumzuia mwananchi kuchanganya mahindi na pamba. Utafiti wa sasa hivi unafanyika Maswa na Ukiriguru. Watu Ukiriguru wanafanya hilo zoezi la kuangalia madhara anayoyapata mwananchi. Sheria hii ni ya zamani. Mimi nataka nijue sheria hii ni ya mwaka gani, kama ni sheria au ni kanuni, kama siyo kufutwa, basi iletwe hapa tuiwekee marekebisho. Kule Meatu wananchi wamekamatwa wamewekwa *lock-up* kwa sababu ya kuchanganya mahindi na pamba. Sheria hii ifutwe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, anafuata Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Luckson Mwanajale na Mheshimiwa Ali Kessy Mohammed ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika katika Bunge hili Tukufu. Nichukue nafasi hii kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwako, lakini nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mpanda Vijijini kwa kuniwezesha kunipa nafasi ya kuingia kwenye Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nami nina wajibu wa kuchangia hotuba ya Rais aliyoitoa tarehe 18. Nampongeza Rais na Serikali yake chini ya kiongozi, Waziri Mkuu ambaye ametoa ushirikiano mkubwa sana wa kumsaidia Rais.

Mheshimiwa Spika, ningeomba nianze kuchangia hotuba ya Rais katika sekta ya kilimo. Nipango mizuri ambayo imewekwa na Serikali, tunaipongeza sana lakini kuna changamoto ambazo zinaikabili ili kuweza kufikia malengo halisi. Kitu cha kwanza, naipongeza Serikali kwa kuwaangalia wakulima kwa kuwapatia pemebejeo zenye ruzuku. Hili limeweka ubora zaidi na wakulima wetu wameanza kunufaika ndiyo maana maeneo ya kwetu tuna mazao ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, changamoto hiyo ambayo tunahitaji kuishauri Serikali ni kuangalia uwezekano wa kuweza kuwasaidia wakulima hawa kuwapunguzia gharama za pembejeo ambazo bado ni kubwa sana. Ukiangalia uwezo wa mkulima huyu kuweza kumudu kununua mfuko mmoja wenye ruzuku ya Serikali wa Sh. 30,000/= inakuwa ni ngumu sana. Tunaiomba Serikali katika mwaka huu wa fedha iangalie ni jinsi gani itaweza kumpunguzia kiwango cha gharama hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwamba wakulima wetu ni maskini sana, sasa hivi tuna kauli mbiu ya Kilimo Kwanza. Bahati mbaya wakulima hawa hawana sehemu yoyote ambayo wanaweza wakapata mikopo kupitia kwenye mabenki. Ninaomba Serikali iharakishe mpango wa kuwamilikisha wakulima hawa ardhi hasa kwenye mpango ule wa hati miliki za kimila.

Mheshimiwa Spika, wakulima wakipewa nafasi hiyo watakuwa na nafasi ya kuweza kupata fursa ya kukopa kwenye mabenki ambayo ninaamini ndiyo itakayosaidia kununua vifaa vya kurahisisha shughuli za kilimo kama vile matrekta. Ninaamini Serikali

ikielekeza mpango huu tutakuwa tumewajengea uwezo wakulima na watakuwa wanazalisha mazao kwa tija nzuri.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, katika kilimo, tunahitaji kuwatafutia masoko Serikali wakulima hawa. Tuna mazao mengi ambayo yanazalishwa hasa kutoka kwenye Jimbo langu na kwa Wilaya nzima ya Mpanda, tuna mpunga mwingi sana, lakini mpunga huu hauna soko kwa sababu tunategemea soko la kutoka kwa Walanguzi. Nilikuwa naiomba Serikali ifikirie mpango wa kuweza kujenga kituo cha ununuzi wa mazao katika Jimbo la Mpanda Vijijini ambalo litasaidia kuweza kunua mpunga, mahindi yanayozalishwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini bado tuna changamoto nyingine kwenye sekta hii ya kilimo hasa katika zao la biashara ya tumbaku. Zao la tumbaku lina wanunuzi wachache. Tunaiomba Serikali iweke juhudi za makusudi kuweza kuwasaidia wakulima hawa waweze kupata soko lingine ambalo litawasaidia kuimarisha zao hili. Zao la tumbaku mwaka huu tunatarajia kuzalisha kilo milioni 150, bahati mbaya zao hili wanunuzi waliopo nchini wana nafasi tu ya kununua kilo kama milioni 90. Kwa hiyo, tuna milioni 60 ambazo zinahitaji Serikali iangalie wakulima hawa watazipeleka wapi. Ninaiomba Serikali ifanye juhudi za makusudi kuwasaidia wakulima hawa ili waweze kupata soko litakaloweza ku-*cover* milioni 60 ambazo zitakuwa zinaelea.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kuishauri Serikali kwa sekta hii ya kilimo kuangalia mpango wa kujenga viwanda vya kusindika mazao ya wakulima sambamba na zao la tumbaku ambalo kimsingi wakulima wakiwezeshwa wakajenga kiwanda cha kusindika tumbaku, naamini soko linalokua la shida litakuwa limefutika.

Mheshimiwa Spika, niende sehemu ya uvuvi. Kule Mpanda tumezungukwa na ziwa Tanganyika, tuna wavuvi ambao hawajatumia rasilimali zinazotokana na ziwa hili, kama inavyofahamika ziwa Tanganyika lina kina kirefu, vifaa ambavyo wanatumia wavuvi hawa wadogo wadogo haviwatoshelezi na hazina tija yoyote ile ya kuweza kupata mazao yanayotokana na ziwa hili.

Hivyo, tunaiomba Serikali iangalie na iweke msukumo wa kipekee kuwasaidia wavuvi wa maeneo ya Ikola, Karema na vijiji vingine vinavyozunguka ziwa hilo ili waweze kuwezeshwa kimtaji waweze kuvua samaki kwenye vyombo vya kisasa zaidi. Naamini tukiwajengea uwezo wavuvi hawa tutakuwa tumewapa nguvu na wataboresha maisha yao na kuongeza uchumi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie miundombinu kwa maana ya barabara. Naipongeza sana Serikali kwa kuweka msukumo mkubwa wa barabara kutoka Tunduma kuja Sumbawanga ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami. Naipongeza Serikali kwa kuweka mpango mzuri wa barabara ya Sumbawanga - Mpanda inayojengwa kwa kiwango cha lami, lakini ninaiomba Serikali ielekeze nguvu sana kuboresha barabara ya Mpanda –Kigoma. Tukifungua hii barabara tutakuwa tumewapa nguvu sana wananchi wa mikoa hii miwili ambayo ipo nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, lakini barabara nyingine muhimu ni barabara ya Mpanda kupitia Inyonga kwenda Tabora. Barabara hii ni muhimu ambayo tunaihitaji nayo ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, nami nachukua nafasi hii ya kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kusimama na kuzungumzia kidogo hotuba ya Rais. Kabla sijaanza kuchangia, ningeomba niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini ambao walinipa ridhaa ya kuwa Mbunge wao.

Pamoja na hayo, naomba pia nimshukuru *DC* pamoja na *OCD* na wasaidizi wake ambao baada ya uchaguzi ule, vijana zaidi ya 400 au 500 walikuja kuvamia pale nyumbani kutaka kunidhuru, lakini bahati nzuri Jeshi la Polisi lilifanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba mimi nipo salama. Ninawashukuru kwa ulinzi wao kwa sababu walilinda karibu wiki nzima. Kwa hiyo, nilifarijika sana kwa kazi hiyo waliyoifanya. Ilikuwa katika harakati za uchaguzi na ndivyo ilivyotokea.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii, naomba nizungumzie kwamba Rais alitoa hotuba hii kwa umakini sana, alitupatia dira ambayo inatuonesha ni wapi tunahitaji kuelekea, lakini nje ya hapo alikuwa amezungumzia sana mafanikio tuliyoyapata huko nyuma ambayo ni mafanikio mazuri kwa kweli. Hakuna Mbunge ambaye yupo hapa ambaye hajaguswa na hilo kwa sababu tumeona barabara zikijengwa, umeme ukipelekwa mahali, maji yakielekezwa huko, kila mahali angalau amegusa. Hii ni nchi kubwa kwa hiyo, huwezi ukapata yote kwa pamoja. Lakini nashukuru Serikali kwa jitihada zake ambazo inazifanya, wananchi wanashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, lakini nilitaka niseme zaidi ilikuwa ni kuhusu barabara katika hotuba hii. Mheshimiwa Rais amesema kwa kipindi hiki ambacho tunacho barabara zitaboreshwa mara dufu zaidi. Naomba kazi hiyo ifanyike. Lakini kitu ambacho nilikuwa nataka kuelezea hapa, Halmashauri zetu zinakuwa hazina uwezo wa kutenga hela kwa ajili ya barabara za vijijini zaidi.

Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali kama inawezekana iongeze fungu kidogo katika Halmashauri hizi ili barabara zile vijijini ziweze kutengenezwa. Bila barabara inakuwa ni vigumu sana. *(Makofi)*

Nakumbuka siku moja nilikuwa katika ziara yangu katika vijiji kadhaa huko kwangu, mwalimu mmoja alikuwa ameletwa pale alipoangalia na kuona kwamba umbali wa kutoka pale alipo Makao Makuu ya Kata ni karibu kilimo 20, 30 alipoambiwa aende huko abebe sanduku alishindwa aliondoka akaacha kazi hapa hapa. Kwa sababu ilikuwa ni vigumu sana mtu ambaye ametoka mjini asafiri kwa mwendo huo huku amebeba begi lake. Kwa hiyo, kama barabara ingekuwa ni safi, bila shaka barabara zingeweza kuleta hamasa fulani kwa watumishi waweze kukaa kule. Kwa hiyo, naomba Serikali itenge hela zaidi kwa Halmashauri ambazo baadaye zitasaidia kujenga barabara za vijijini.

Lingine ambalo nilikuwa naomba niliseme ambalo kwangu limekuwa ni tatizo kubwa na siyo kwangu tu, maeneo mengi sana, lilikuwa ni suala la wakulima kunyanyaswa hasa kwa ajili ya lumbesa. Lumbesa ni gunia ambalo limeshonwa zaidi ya inavyotakiwa lishonwe. Kwangu kulikuwa na kelele nyingi sana na kila wakati wakipiga simu wanaeleza kwamba mbona watu wa mahali fulani wao wanakubalika kwa nini sisi tusikubalike?

Kwa hiyo, imekuwa kwa mkulima kwa kweli ni taabu kubwa na mazao yake yananunuliwa kwa bei ndogo kwa sababu ya lumbesa hii ambayo inazidi. Nilikuwa naomba hii *package* iwe ni *uniform* nchi nzima kuliko sehemu nyingine kuna lumbesa inakubalika, sehemu nyingine haikubaliki. Nilikuwa naomba Serikali kwa hapo iangalie, ijaribu ku-*monitor*.

Lakini la pili ambalo naomba kuzungumzia ni kuhusu fidia. Kila mahali tunasikia kuna malalamiko ya fidia kwa wananchi hasa wale ambao maeneo yao yamechukuliwa. Malalamiko hayo yamekuwa makubwa kwa sababu ni kama Serikali haiangalii vizuri hasa katika kipindi kile cha kuweza kumlipa mwananchi na kufanya tathimini.

Naiomba Serikali ijitahidi kufanya tathimini ya uhakika na kuweka mambo haya wazi ili mwananchi ambaye anatakiwa alipwe asiwe na maswali. Lakini anakuja mtu wa ardhi anapima, anaondoka, huyu mwananchi hajui ni kitu atalipwa hajui ni kitu gani kitatokea baada ya hapo. Nilikuwa naiomba Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba inapofikia hatua hiyo, kwa kweli wajitahidi sana kuweka wazi mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, bado migogoro hii ya ardhi imekuwa ni mikubwa hata kule kwangu, hasa kule Kitulo karibu na Kata ya Ilugu kumekuwa na shida kubwa sana. Wananchi wanalalamika na wametozwa hela nyingi sana kwa sababu ya mifugo. Nilikuwa naomba Serikali ijaribu eneo ambalo wananchi wale wanaweza kufugia mifugo yao. Lakini sasa hivi Serikali iko kimya, hakuna utafiti wowote unafanywa kuhakikisha kwamba wananchi tuwaweke vipi baada ya hapo. Naomba sana Serikali ijitahidi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa naomba nilizungumze ni mfumo mzima wa ugawaji wa mbolea. Jamani mbolea ni kweli tunashukuru Serikali inajaribu kutoa mbolea kwa ajili ya wakulima, lakini ugawaji wake bado haujaboreshwa. Ni mbaya kweli kweli! Malalamiko yamekuwa ni mengi mno! Wakati niko kwenye Jimbo langu mara simu kwa *DC*, mara kwangu mbolea huku sijui imepandishwa bei. Lakini hata hivyo nimeshangaa kuona kwamba katika *package* ya mbolea ilikuwa Sh. 17,000/= mwaka jana, mwaka huu karibu Sh. 40,000/=. Mwaka kesho wananchi wanategemea itakuwa Sh. 60,000/= au Sh. 70,000/=, kuna nini? Tulikuwa tunaomba kama kutakuwa na ongezeko, lakini lisiwe ongezeko kubwa kiasi hicho, liwe ongezeko ambalo ni kidogo. Maana sasa hatumsaidii mwananchi kwa mbolea hii ya ruzuku.

Ni kama bado tunamuumiza mwananchi wa kawaida ambaye hana kipato chochote kwa kweli kumwambia alipe Sh. 40,000/=, ni kazi kubwa sana. Nilikuwa

naomba Serikali ijaribu kuangalia hilo kwamba wanapojaribu kuongeza bei ya mbolea, basi waongeze kwa kiasi kidogo.  Lakini sio hivyo inavyokwenda sasa hivi.

Pia mfumo mzima wa kugawa mbolea uangaliwe. Wizara ya Kilimo ina watu watalaam wengi sana, kwa nini wasiangalie kwamba ni njia gani bora itakayosaidia kuhakikisha kwamba hawa wananchi wanapewa kuliko malalamiko ambayo yamejaa kila mahali sasa hivi?

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa naomba ni suala la umwagiliaji. Wenzangu wameshasema, lakini jamani kuna maeneo mengi ambayo bado hayajaainishwa kufanya kwa umwagiliaji. Nilikuwa naiomba Serikali ijaribu kuweka watalaam wake, tujaribu kuboresha hiyo hatua kwa sababu hapo ndio patatuokoa kwa ajili ya chakula. Kama kule kwangu Mbeya, maeneo ni mengi sana lakini maji yanapotea bure, hakuna kitu chochote kinachoendelea. Naiomba Serikali ijaribu kulifuatilia suala hilo kwa makini kwa uhakika kabisa ili tujaribu kujiepusha na hii shida ya njaa ya kila wakati. Naomba sana hilo lifanyike.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka nichangie ni kuhusu walimu. Jamani walimu wanapopelekwa vijijini, kama nilivyotangulia kusema, wanapata mazingira magumu sana. Kwa nini hawa walimu ambao wanakwenda vijijini zaidi iwe wa Sekondari au *Primary School* wasipewe motisha fulani itakayowasaidia waweze kukaa katika vijiji kuliko tukawalinganisha na mtu wa mjini? Watu wa mjini wana mambo mengi ambayo wanafanya. Atafanya biashara, atafanya chochote kile! Lakini wa vijijini wale hawana chochote, wanatembea mwendo mrefu, kwa nini wasipate motisha fulani ya kuwasaidia ili waweze kukaa vijijini? Maana hatuwezi kusema hii itajengwa kwa leo, lakini angalau tuonyeshe ishara fulani kwamba kwa kweli tunawajali. Ndio maana unakuta hata hii mitihani wanafunzi wanafeli kwa sababu shule za vijijini walimu wawili au mmoja shule moja, watoto 400 au 500. Unategemea nini hapo? Kitu gani kitatokea?

Walimu wawili watafanya nini? Watafaulisha watoto kweli! Nilikuwa naomba Serikali ijaribu kuangalia hawa walimu ambao wanakwenda vijijini wapewe motisha gani. Watalaam nafikiri wanaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nakushukuru kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa kwanza mwanamke kwa Bunge la Kumi. Pia natoa pongezi kwa Naibu Spika, kwa Waziri Mkuu, kwa Mawaziri wote na Wabunge wote wa Bunge la Kumi. Pia namshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa ustamilivu aliokuwa nao wakati wa Kampeni zote za uchaguzi wa mwaka jana.

Kusema kweli uchaguzi wa mwaka jana ulikuwa ni uchaguzi mchafu, simu zilisambazwa kila sehemu za kumkamshifu mpaka watu hawafahamu kama alikuwa ni mwana CCM au ni huyu bwana yuko upande wa Kikwete wanamtumia *message* za ajabu

ajabu. Kusema kweli ilikuwa ni kashfa kubwa, uchaguzi wa mwaka jana. Nampongeza sana Rais Kikwete kwa uvumilivu aliokuwa nao.

Pia namshukuru sana Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Waziri Mkuu kwa kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa. Ndugu zangu tulikuwa hatuna tegemeo kabisa kupata barabara za lami za Mkoa wa Rukwa, kutoka Tunduma kupitia Namanyele mpaka Mpanda, barabara ya kutoka Sumbawanga kwenda Kasanga, pia kujenga bandari katika Bandari ya Kipili na bandari ya Ikola kule Kalema. Ndugu zangu wanaosema kwamba Serikali ya Awamu ya Nne haikufanyakazi hawana macho. Kama wana macho, hawaoni.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali ya CCM. Mimi mwenyewe ndugu zangu nilikuwa mwana CHADEMA, nashukuru sana kusema kweli, sikufanikiwa kupata Ubunge kwa kupitia tiketi ya CHADEMA. Nashukuru kabisa kusema kweli nilikuwa nakosa Ubunge kwa tiketi ya Vyama vya Upinzani. Ni kama vile mtu aliyeokoka, kuingia CCM na kupata Ubunge kupitia tiketi ya CCM nashukuru sana. *(Makofi)*

Ndugu zangu kwanza nazungumzia kuhusu barabara katika Mkoa wa Rukwa hasa jimboni langu la Nkasi Kaskazini. Kwanza nawashukuru wananchi wa Nkasi Kaskazini kwa kunichagua mimi kupitia Chama cha CCM kuwa Mbunge wa Jimbo la Nkasi. Kusema kweli wangenichagua kupitia kiti cha CHADEMA ingekuwa ni kashfa kubwa sana. *(Makofi)*

Ndugu zangu naomba kuchangia kuhusu barabara. Katika vijiji vya Nkasi hasa Jimbo langu la Nkasi Kaskazini Kusini hii ni miaka 50 tangu tumepata uhuru lakini vijiji vingine hata *Land Rover*, hata bajaji hawajaziona. Hazipitiki! Kwa hiyo, naiomba Serikali chini ya Wizara ya Mheshimiwa Magufuli itazame vijiji vya mwambao wa ziwa Tanganyika, zitengenezwe barabara ndugu zangu.

Kule tuko mwambao, najitahidi kwanza kwa ulinzi wa watu wetu, kila mara matukio ya ujambazi yanafanyika katika Ziwa Tanganyika. Wanaegesha mitumbwi, wanapora mchana kweupe na mali za wananchi na wanawafunga wananchi wanafanya wanavyotaka. Ni kama hukuna Serikali.

Kuna vijiji vya Ikola kuanzia Mkombe, Kalila, Kazovu, Isaba, Chongo, Katete, vyote ndugu zangu kuanzia uhuru hawajaona magari. Nkasi Kusini Kigo Kisambala, Msamba, Izinga, Lyapinda pamoja sijui na Lupata hawajaona magari tangu kuzaliwa kwa nchi hii. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ndugu zangu iangalie sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kilimo ndugu zangu sisi Wana Nkasi tunalima tatizo kubwa, ni sehemu za kuhifadhi mazao.

**KUHUSU UTARATIBU**

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68 (7) ambayo ninarejea Kanuni ya 649 (1)(g) ambayo inasema: "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo ya majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayozalilisha watu wengine."

Mheshimiwa Spika, Mbunge ambaye anazungumza sasa hivi mbali na kuanza na lugha ya kujinasibu, tukaivumilia, lakini akafikia hatua ya kusema kwamba anashukuru hajachaguliwa ama hakuchaguliwa kwa tiketi ya CHADEMA kwa sababu ingekuwa ni kashfa kubwa.

Mheshimiwa Spika, unajua CHADEMA ni Chama cha Siasa kilichosajiliwa chenye Wabunge, chenye Viongozi makini. Sasa kwa Mheshimiwa Mbunge, aliyepita kusema kuchaguliwa kupitia CHADEMA ni kashfa, kwa mujibu wa Kanuni ya 64(g) lugha hiyo inaudhi, inadhalilisha CHADEMA, inadhalilisha Viongozi na inadhalilisha Wanachama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kwa kutumia meza yako Mheshimiwa Mbunge ama afute kauli yake, ama aombe radhi, ama atuhakikishie kwamba tunaruhusiwa na sisi kuzungumza lugha za ajabu ajabu za kuudhi wengine. Ahsante sana.

**SPIKA:** Anayeruhusu kuzungumza lugha za ajabu kama ikibidi ni mimi, sio Mheshimiwa anayejadili. Hasa anasema yeye hakusema CHADEMA, kwa hiyo, endelea na kuzungumza kwako. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Amesema amechaguliwa ...

**SPIKA:** Tumemaliza Mheshimiwa, ukae.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Maana yake niliposemea kwamba ningekuwa CHADEMA, mimi nisingekuwa na nidhamu potufu Rais anapozungumza mimi nitoke kwenye Ukumbi wa Bunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge endelea kuzungumza. Kwa hiyo, Wabunge wote mkae. Mheshimiwa Kessy endelea kuzungumza.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya Maji. Rais kazungumzia maji na kweli katika Jimbo langu la Nkasi hasa Namanyere, maji. Naiomba Serikali yako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, zile pesa ambazo zimekaa Uingereza kule tuwaombe Waingereza kwamba huku wananchi wana matatizo ya maji hususani mji wa Namanyere. Ni pesa nyingi zimekaa kule ndugu zangu, tungepata ile riba tu ya zile pesa na sisi wananchi wa Namanyere tungepata maji ya kuaminika. Kwa hiyo, naliomba Baraza lako Tukufu litusaidie zile pesa ziko Uingereza zimekaa za mahesabu ya rada, zirudi Tanzania ili zisaidie sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri katika ziwa Tanganyika tuna meli moja ya Lihemba, cha kushangaza badala ya kuongeza ratiba, imepunguza ratiba, imekuwa kila baada ya wiki mbili inasafiri mara moja na vijiji katika mwambao wa ziwa Tanganyika havina usafiri mwingine, vinategemea usafiri wa meli. Kwa hiyo, ninashangaa badala ya kuongeza usafiri, zimepunguza usafiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ardhi. Ndugu zangu wananchi wa Jimbo la Nkasi wanategemea ardhi. Kitu cha kushangaza, kule wakija watu wanachukua ardhi za wananchi kwa kutumia vyeo vyao bila kutumia utawala bora. Kila kiongozi anayekuja kule ndugu zangu anachukua ardhi, ni kama vile inakuwa mikataba ya yule Mjerumani aliyekuja Morogoro, *Carl Peters* kuwapora wananchi ardhi. Ardhi ya kule kwetu yote imeporwa na baadhi ya viongozi wanaokuja kule kwetu kwa muda mfupi, kuwandanya wanakijiji kupewa ardhi ya kutosha na wananchi wanabaki hawana ardhi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, sisi ni wakulima wazuri tunaishukuru Serikali kwamba mwaka jana imenunua mazao yote ya mahindi kule kwetu, lakini maghala ya kuhifadhia mazao hayatoshi. Tuna ghala ndogo kabisa pale Namanyere Mjini na nyingine Mtenga, hazitoshi kabisa kuhifadhi mazao. Mazao yaliyonunuliwa mwaka jana mengi yalinyeshewa na mvua, Hifadhi ya Taifa ikataka kupata hasara na mazao wameshayanunua na mengine yako kwa wananchi ambao hawana uwezo wa kuyanunua.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali, ilitoa pesa kwa wingi na kumaliza mazao yote ya mahindi katika Jimbo langu la Nkasi Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, tunachoomba ni barabara. Tunaiomba Serikali ikubali kuchukua barabara ya kutoka Nkana kwenda Kala na kutoka Kitosi kwenda Mapembe, na kutoa Kasu kwenda Itindi mpaka Kibaoni. *TANROADS* wachukue maana yake Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi na hizo barabara. Kusema kweli ikifungua hivi nitaishukuru sana Serikali, sio zaidi mimi nimechangia hoja mpaka hapo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii. Awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kunifikisha humu katika nyumba yako Tukufu nikiwa mzima bukheri wa afya.

Lakini pili, naomba nitumie fursa hii kumshukuru mama yangu kwa kunizaa, na kunilea katika maadili mema hadi na mimi leo hii kuaminiwa na watu wa Nzega kuwa Mbunge na mwakilishi wao katika Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tatu, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Nzega kwa kunichagua mimi kuwa Mbunge wao, hawakujali maneno, matusi na kashfa zilizoandikwa kwenye magazeti yaliyonunuliwa na mafisadi wachache ili kunichafua na

hatimaye walinichagua kwa kura nyingi na mimi ninawaahidi nina uwezo, nina moyo safi wa kuwatumikia na wasitegemee chochote zaidi ya utumishi uliotukuka kutoka kwangu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie pia fursa hii kumpongeza Rais wa Serikali a Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Serikali yetu. Lakini pia naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe na Naibu wako kwa kuchaguliwa kuwa Spika na Naibu Spika, wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mwisho, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuingia katika nyumba hii tukufu ambayo ina heshima kubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, aliyoitoa wakati akifungua Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika hotuba hiyo alitoa vipaumbele 13 ambavyo ndiyo vitakuwa dira ya uongozi wa Taifa letu katika miaka mitano ambayo inaendelea kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kusema kwamba kumekuwepo na utaratibu au utamaduni wa kubeza mafanikio na kutokukubali kwa dhati kabisa na kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Serikali yetu. Huu ni utaratibu mbovu na hata kidogo hautii faraja kwa Watanzania wala hautii moyo bali unazidi kuwavunja moyo na unazidi kuondoa imani ya Watanzania kwa Serikali yao.

Katika Serikali yetu ya Awamu ya Nne kipindi cha kwanza tumeshuhudia mengi yakifanyika. Naomba nigusie machache ambayo mimi ninayafahamu kwa undani sana. Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake amekuwa kama *pioneer* wa kuboresha huduma za afya katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili. Kwa wastani nikigusa machache, ameongeza huduma za ubingwa kwa kiasi kikubwa sana katika Hospitali ya Taifa Muhimbili hususan huduma *Dental*. Sasa hivi Kituo cha *Dental* cha Muhimbili ni kituo kikubwa kuliko vingi katika Afrika Mashariki na nchi zote zilizopo *Sub-Sahara Africa.*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Rais wetu kwa jitihada zake binafsi amejitahidi kujenga Kituo cha kufanya Operesheni za Moyo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, lakini pia sasa hivi kutoa huduma za mafigo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na huduma nyingine nyingi za rufaa.

Bila shaka katika miaka michache ijayo Watanzania wanaohitaji huduma za rufaa watakuwa hawapelekwi nje ya nchi kwa ajili ya kupata huduma hizo, watazipata hapa hapa kwetu. Haya ni mambo machache ambayo rais wetu ameyafanya katika Sekta ya Afya na ni mambo ambayo yatakuwa *Legendre* pindi atakapokuwa amemaliza uongozi wake kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kuna wachache walisema hawauoni ubunifu wala utendaji kazi, uchapakazi wa Rais mwadilifu na mwaminifu Dr. Jakaya Mrisho Kikwete. Mimi

ninaomba nitumie fursa hii kupingana nao na kuwaomba waende wakafanye utafiti kwanza kabla ya kuongea, kubeza na kudharau mafanikio ya Serikali ya CCM ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitumie fursa hii kuipongeza Serikali yetu kwa mengi mazuri ambayo imeyafanya, kweli safari haikamiliki siku moja na maisha ni safari na sisi tunaanza safari kwa hatua ya kwanza. Tumekamilisha miradi mingi ya maendeleo katika sekta ya elimu na miradi hii inapaswa kupongezwa japo mapungufu yapo, lakini Watanzania tuondokane na utamaduni wa kubeza mafanikio wa kutosherehekea mafanikio na kudharau kila kitu ili mradi tu sisi ni Wapinzani, ni wapinga maendeleo, hiyo haikubaliki na ni utaratibu mbovu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naomba nitumie fursa hii kujielekeza katika kipaumbele cha sita na cha saba ambapo Mheshimiwa Rais anatoa mwongozo wa kuongeza jitihada za kuhakikisha Taifa letu linanufaika zaidi na maliasili zake na kile kipaumbele cha saba kinachohusiana moja kwa moja na kuboresha zaidi ukusanyaji wa mapato ya Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwenye hivi vipaumbele naomba nivihusianishe sana sana na miradi mikubwa ya uwekezaji kwenye sekta ya madini ambayo imekuwa kama *fashion* ya Serikali katika zama hizi tulizopo leo hii, kwamba tunawakaribisha wawekezaji wengi sana katika sekta za madini na sasa hivi tunaelekea katika sekta za gesi na mwisho kwenye sekta za mafuta. Wawekezaji hawa wanakuja kuwekeza katika nchi yetu na kwa kisingizio kwamba wanawekeza pesa nyingi, tunashuhudia wakiondoka na maliasili hii ambayo tuna uhakika haitaota tena, itaisha na mwisho wa siku tutabaki na mashimo, tutabaki na madhara yanayosababishwa na miradi hii mikubwa, lakini Taifa letu halipati manufaa makubwa na hata wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo uwekezaji huu mkubwa unafanyika, wamekuwa hawafaidiki na miradi hii.

Mheshimiwa Spika, leo hii ukipita katika Jimbo ninalotoka la Nzega, ukaenda kwa jirani zetu wa Kahama na wale wa Geita ukawaambia hapa kuna miradi mikubwa ya uwekezaji kwenye sekta ya madini, wananchi wale hawawezi kukuelewa kwa sababu wamevumilia, wamedhulumiwa, hawajalipwa fidia, bado kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira na miradi hii mikubwa inatumia maji mengi ukilinganisha na wazawa.

Mheshimiwa Spika, katika hili nimekuwa nikiwaahidi wananchi wa Nzega kwamba nitawasilisha hoja yangu binafsi ili kufafanua kwa undani zaidi ni jinsi gani Bunge lijadili matatizo ambayo yanajitokeza katika uwekezaji huu mkubwa katika sekta ya madini. Bila shida nitakapopata fursa ya kufanya hivyo, basi nitaeleza kwa undani zaidi ni nini hasa kifanyike na nitaliomba Bunge lako liweze kuichukua hoja na kutoa mapendekezo kwa Serikali. Lakini naomba niwahakikishie ndugu zangu wa Nzega na wengine katika migodi hii, kwamba sitalala, sitakaa kimya mpaka nione haki inatendeka kwa wachimbaji na wakazi wa maeneo ambapo migodi hii ipo ili nao waweze kufaidika na rasilimali na maliasili ambayo ni haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nikuombe kumalizia kwa kusema kwamba Taifa halitoendelea endapo tu tutafumbia macho mambo kama haya, endapo tu Serikali yetu haitoyapa kipaumbele maslahi ya wananchi, hatatoa kipaumbele kwa wananchi walio na kipato cha chini na badala yake kuwaweka pembezoni badala ya kuwaleta katikati katika ushiriki wa ujenzi wa uchumi wa Taifa letu.

Hii inaendana moja kwa moja na Kanuni alizozitoa mwanafalsafa, mwanazuoni wa Marekani aliyekuwa akiitwa John Rolls kwamba endapo inatokea rasilimali hazitoshi basi wananchi wa kipato cha chini wapewe kipaumbele, halafu wale wengine wasipewe kipaumbele. Lakini leo hii tunashuhudia wananchi walioko kwenye migodi, wananchi walioko kwenye sehemu ambapo rasilimali ipo wakikosa huduma….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALA:** Hivi ni mimi huyo?

**SPIKA:** Yes, ya pili.

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALA**: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, namshukuru Mungu kwa kuniweka hai mpaka leo. Nawashukuru pia wapiga kura na wananchi wote wa Musoma Mjini kwa kunichagua kupitia CHADEMA na nina wahakikishia wananchi walioko Musoma Mjini, wengi wako Chama cha Mapinduzi, lakini wamenichagua kupitia tiketi ya CHADEMA, nawashukuru sana.( *Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Rais, pia nashukuru kwa taarifa aliyoitoa Rais katika Bunge hili katika ukurasa wa tisa, nanukuu, kwa ruhusa yako, anasema: “Nafurahi kusema kuwa mipaka ya nchi yetu iko salama na wala hakuna tishio lolote la kutoka ndani au nje ya nchi yetu”.

Mheshimiwa Spika, hii ni taarifa nzuri sana, naipongeza. Lakini katika ukurasa wa 10, napenda kunukuu tena anasema: “Napenda kuhakikisha kuwa kazi tuliyoianza ya kuimarisha Jeshi letu kwa kulipatia zana na vifaa vya kisasa vya utendaji kivita tutaiendeleza bila ajizi”.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni kwamba Taifa ambalo halina tishio ndani na nje ya mipaka yetu, tunanunua silaha nzito za kivita kwa ajili ya nini? Tunanunua vifaa vizito wakati hatuwezi kupigana na Marekani kila siku tunakwenda kuwaomba misaada? Tunanunua vifaa vizito vya kivita kupigana na nani? Kenya wakati ni ndugu zetu?

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zingekwenda kuwasaidia vijana ambao wako mjini wanahangaika. Leo vijana wengi wa Kitanzania wako Mijini wanaokota makopo na

chupa cha plastiki unashindwa kutofautisha nani ni kichaa, nani ni mzima, wote wanaokota makopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunachukua fedha kuziwekeza kwenye silaha, nchi isiyo na vita kununua silaha nzito za kivita ni *dead money*, ni fedha iliyokufa. Fedha hizi tungezirudisha tukaziingiza katika migodi, tukawatoa wawekezaji tukafanya kazi hiyo sisi wenyewe,tungepata faida ya kutosha na baadaye tukanunua zana hizi za kivita. Nawashangaa sana Wabunge ambao tuko hapa ndani, tunashindwa kuangalia matatizo yaliyopo katika shule za Kata tunazisifia wakati watoto wetu hawasomi shule hizo. Naomba mtoto mmoja wa mmojawapo wa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awe anasoma katika shule za Kata au watoto wetu wawe wanasoma katika shule za kata. Leo tunazisifia wakati watoto wetu hawako kule. Ningekuwa sizingatii Kanuni ningongea lugha zinazoudhi, ningesema tuache unafiki. Lakini siwezi kusema hivyo kwa sababu Kanuni zinanikataza. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Unatukana kijanja. (*Kicheko*)

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, tunawasahau Watanzania na nasikitika sana Wabunge wa Bunge hili wanashindwa kutofautisha amani na utulivu. Tanzania amani haipo, kilichobaki ni utulivu, amani inatoka moyoni. Kwa mfano rahisi wa amani, tuko katika benki, wanaingia majambazi, wakatulaza chini kwa ajili ya kutupora na kila anayenyanyuka anapigwa na tukatulia, pale hakuna amani kuna utulivu ndipo tunapoipeleka Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wanadhani ni kukaa bila vita, huo ni utulivu. Tanzania amani imekwisha katika kipindi kirefu, nadhani kipindi cha Awamu ya Pili amani ndiyo ilianza kutoweka, kilichobaki ni utulivu na unaelekea kutoweka kwa sababu hatutaki kuwa wakweli.

Mheshimiwa Spika, ningependa tuliangalie hili kwa umakini, yametolewa majibu mazuri sana na Manaibu Waziri. Naibu Waziri wa Afya alituambia sasa kuna mashine ya kusafisha figo Dar es Salaam, lakini kule Vijijini watu hawana nauli ya kufika Dar es Salaam, hiyo mashine inawasaidia nini wao? Tungewasaidia watu hawa kwanza kuepukana na umaskini waweze hata kuwalipia watoto wao shule. Hizi shule za shilingi elfu ishirini kuna watu hawawezi kulipa, lakini sisi tunakaa tunasifia kama vile Watanzania wote wana raha.

Mheshimiwa Spika, inawezekana ninyi waliowachagua wana raha, lakini Musoma Mjini kuna watu hawana raha, wala hawawezi kuwalipia watoto hizi shilingi elfu ishirini, hata tukisema wasome bure bado uwezo wa kununua *uniform* haupo, hawa tumewasahau, sisi tunakaa tunasifia tu. Lazima sasa Serikali tuangalie jinsi ya kuendeleza wananchi wetu na namna gani ya kuepukana na shida za kila siku.

Mheshimiwa Spika, kuna watu mpaka leo yawezekana hawakulalia godoro, wanalala sehemu ngumu, wameamka saa kumi na moja usingizi umekwisha, hawa hawana amani, wana utulivu tu. Tunaposema amani, tuhakikishe tunairudisha amani

mioyoni mwa Watanzania. Leo ukienda kwenye Miji mikubwa utakuta vitumbua saa kumi viko *stand* vinauzwa, ukivikuta saa kumi *stand* vinauzwa ujue mpaka saa kumi kuna watu hawajanywa chai, amani iko wapi kwao? Halafu sisi tunakaa tunajisifia kuwa Tanzania ni nchi ya amani? Tanzania ni nchi ya utulivu unaoelekea kutoweka, sio nchi ya amani tena.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu ya umaskini wa Watanzania na *gape* limekuwa kubwa, sisi tuko hapa tunapumua hewa tunayoitaka kama vile tuko mbinguni. Juzi Naibu Spika anasema tupunguze baridi tuweke joto, lakini kuna watu wengine hawajawahi kuona hata feni, hawa amani inatoka wapi? Hawa ni utulivu tu na ni utulivu wa kulazimishwa. Kama tunaitaka amani tuitafute kwenye mioyo ya Watanzania tuirudishe, lakini mabomu ya kuwasha na mabomu ya machozi hayawezi kuleta amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, amani italetwa kama Watanzania wataweza kusomesha watoto wao, amani itaonekana kwa Watanzania kama wanaweza kuweka akiba. Tukiendelea kuyachekea haya na kurushiana vijembe hata huo utulivu utatoweka. Nilishangaa kusikia Mbunge mmoja anasema kwamba tufunge milango turushiane ngumi humu ndani, hata hapa Bungeni sasa utulivu uishe? Naomba katika ziara za Wabunge aende kwenye Bunge la China, wamfungie ajaribu kuzipiga hizo ngumi kama atakuja na medali au mapengo.

**TAARIFA**

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa yake siikubali.

**SPIKA:** Hajaisema hata taarifa yenyewe. Hebu sema taarifa kwanza, hebu ukae chini, ile Kanuni inasema mtu akisema taarifa wewe unayesema unakaa chini, yeye anatoa taarifa yake, akimaliza unasema aaa! Siitaki. Enhee, haya sema taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8), Mheshimiwa Mbunge anayesema sasa hivi inaonekana katika maelezo yake mengi kuna taarifa nyingi muhimu ambazo hana au hazifahamu. Kwa mfano, kuhusiana na masuala ya kusema kwamba nchi yetu haina tishio, kwa hivyo, haoni sababu kwa nini Jeshi wawe na silaha za kivita ambazo zinapoteza fedha bure. Ni kwamba katika masuala ya usalama kuna kitu kinaitwa *threat level* na kuna kitu kinaitwa *preparadeness* kwamba kwa sababu kiusalama hatujui kesho kutatokea nini, lazima tuwe tayari kwa lolote litakalotokea tuweze kukabiliana. Kwa hiyo, nampa hizi taarifa awe anazifahamu katika maelezo yake. Ahsante.

**SPIKA:** Haya Nyerere una haki ya kukubali au sio kukubali.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa yake siikubali kwa sababu ushindi wa vita sio....

**SPIKA:** Huna sababu ya kusema sababu, kubali basi, sasa. (*Kicheko*)

**MHE. VINCENT J. NYERERE:**Mheshimiwa Spika, ushindi wa vita sio silaha nzito, ni moyo.

**SPIKA:** Endelea bwana we, usiwasikilize, we endelea.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ni ushahidi wa kutosha, wakati wa vita ya Uganda, wananchi wa Uganda waliibadilikia Uganda kwa utawala wa Iddi Amini na wakaisaidia Tanzania. Leo tukipigana vita wananchi watakuwa *against* Serikali yetu kwa sababu wana chuki nayo, ni ukweli usiopingika. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ila hayo maneno ya mwisho ondoa kwa sababu ni ya uchochezi. Haya endelea.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda tunapopanga mambo yetu tuwafikirie wananchi kwanza kuliko vitu. Kwanza, maendeleo ni maendeleo ya watu sio maendeleo ya vitu. Kama kweli amani tunayoiongea tukiirudisha mioyoni mwa Watanzania itarudi, lakini kama tunataka utulivu wa kulazimisha na wenyewe utapotea.

Mheshimiwa Spika, nisingependa kunyoosheana vidole kwamba ni nani mchochezi na nani sio mchochezi. Matendo tunayoyafanya sisi wanasiasa yanapelekea kupoteza hata utulivu uliopo. Naomba tu sisi wote ni Watanzania, tuache habari ya itikadi, tuungane pamoja, tuwajaze moyo Watanzania wenzetu walioko Mijini na Vijijini wanaopata shida, tuukuze utulivu uliopo na amani itarudi pole pole.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma watu walikuwa hawana kitu lakini walikuwa wana amani, leo hawana kitu na hawana amani na utulivu unalazimishwa. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu Wabunge wa vyama vyote tuache sasa kutupiana vijembe, tuache kudharauliana na kukashifiana kwa vyama vyetu, tuwe watu wamoja katika kulijenga Taifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mungu na kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Watanzania wote kwa kushiriki vyema katika uchaguzi mkuu uliopita kwa amani na utulivu na matokeo ambayo yametufanya sisi wote tuwe hapa siku hii ya leo. Kwa sababu hiyo, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza wote waliofanikiwa kuchaguliwa katika Uchaguzi Mkuu uliopita. Nawapongeza Wabunge wote wa vyama vyote, nawapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri na naomba niseme kwamba sasa uchaguzi umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi iliyotuleta ni kujenga nchi yetu na kwa sababu hiyo hotuba tunayojadili ni hotuba ya Rais wetu, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza kwa hotuba yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, wajibu tulionao sote kwa pamoja ni kusimamia utekelezaji wa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama wengi walivyosema huu sio wakati wa kupigana vijembe, nadhani kazi ambayo tunapaswa kuifanya ni kuchangia katika hotuba hii ili hatimaye kitakachofanyika kiweze kuwanufaisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hilo niseme mawili, matatu. Nikisema kwamba Serikali haikufanya chochote nitakuwa najitia upofu. Kwa sababu natambua michango mingi ambayo Serikali imefanya katika awamu mbalimbali katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa nililonalo ni baadhi ya watendaji ndani ya Serikali ambao nadhani kwa namna moja au nyingine wanahujumu mipango mizuri ambayo Serikali inaikusudia kwa watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, pale Rombo, *CAG* alikagua Halmashauri ya Rombo na kwa bahati mbaya akatoa hati chafu kwa sababu ya upotevu wa shilingi milioni 916, ali-*site* watendaji ambao walisababisha upotevu huu, lakini hadi leo hii kuna mvutano sijui wa namna gani, ambao mpaka sasa hivi watu wa Rombo hatuelewi ni kwa nini watendaji ambao wanahusika na hasara hiyo hawachukuliwi hatua. Hili litapelekea watu wa Rombo kuadhibiwa kwa kunyimwa ruzuku ya maendeleo. Kwa hiyo, naiomba Serikali, mipango hii mizuri ambayo inaletwa mbele yetu iambatane na usimamizi mzuri ili iweze kuwanufaisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hili ambalo nimelizungumza, naomba sana Waziri anayehusika, pengine hata kwa kusaidiana na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mtaa ya Mheshimiwa Agustino Lyatonga Mrema, watembelee pale Rombo na kuona nini kinachoendelea kwa sababu matatizo ni mengi, fedha za wananchi zimehujumiwa, lakini watu wanaendelea kama vile hakuna lolote lililotokea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, nizungumze kidogo kuhusu shule za Kata. Ni kweli shule za Kata zina matatizo, lakini ndugu zangu shule za Kata zimeleta mchango mkubwa sana kwa wananchi wetu. Kule Rombo nina shule 41 za Kata na Kata 24, karibu kuna Kata zenye shule mbilimbili. Hivi sasa nazungumza habari ya watoto wa Rombo waliotokana na shule za Kata walio Vyuo Vikuu na vyuo mbalimbali. Sasa ninachoomba tusibeze hizi shule za Kata tuzisaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shule zina matatizo kweli ya maabara, Walimu, maktaba na matatizo mengi kwa ujumla. Lakini ninachokiona Roma haikujengwa kwa siku moja. Lazima tupate mahali pa kuanzia. Naomba sana wale watoto ambao wanamaliza *Form*

*Four* na *Form Six* wasaidiwe kwa namna ambavyo wanaweza wakajengewa uwezo wa kuweza kukopa au kukopesheka ili wapate kitu cha kufanya na kwa hili naomba sana stadi za ufundi ziimarishwe na ikiwezekana vyuo vya ufundi viimarishwe kwa ajili ya kuwasaidia watoto hawa ili hatimaye waweze kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie masuala ya maandamano ya vyuo vikuu. Kwa maoni yangu, inawezekana hoja ya wanafunzi wa Chuo Kikuu ni nzuri na inajadilika na naomba Serikali iichukue na kuifanyia kazi. Lakini naomba sana wanasiasa tuache kufanya siasa na wanafunzi. *(Makofi)*

Mwaka jana tulisikia baadhi ya wanafunzi wamewachangia wagombea *favour* za kuchukua *form*, wakati wa chaguzi zao za Mabaraza yao kunakuwa na kampeni kabisa za vyama. Sasa hali hii inawafanya vijana hata katika mambo ya kijamii waya-*approach* kwa mtindo huo wa sisi wa upande wa huku na sisi wa upande wa huku. Hii haitatusaidia, mimi nafikiri imefikia wakati wanafunzi wakae na mapenzi ya vyama vyao katika mioyo yao, wasubiri wakati wa uchaguzi wafanye maamuzi yao na sisi wanasiasa tuondoe kabisa siasa kwenye vyuo ili vyuo vile vitulie, wanafunzi wasome na hata baadaye waweze kufanya yale ambayo wanatamani katika uhuru. Yale matatizo yao tuyapokee kama hili la sasa hivi la posho zao tulipokee, ni jambo ambalo linajadilika na tuwasaidie ili waweze kuwa na amani na wasome vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ningependa pia nizungumzie suala la kilimo. Serikali inajitahidi kutoa vocha za pembejeo. Lakini vocha zile zinachakachuliwa sana na Watendaji.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Msemaji wangu wa mwisho asubuhi hii atakuwa Mheshimiwa Leticia Nyerere.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Awali ya yote naomba niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kwimba kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa wakati wa zoezi la mchakato mzima wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Wanawake wote ambao walijitokeza kugombea wakati wa uchaguzi bila kujali wanatoka vyama gani. Naomba niwapongeze wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siwezi kuendelea kusema bila kugusia manyanyaso ambayo wanawake wagombea wameyapitia wakati wa uchaguzi na manyanyaso haya yalifanywa kwa wagombea wa vyama vyote.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kwamba baadhi ya Viongozi wetu wanaendeleza unyanyasaji wa kijinsia na kwa nini mgombea mwanamke ananyanyasika eti tu kwa sababu…

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 64(b), mzungumzaji hatazungumzia jambo lolote ambalo haliko kwenye mjadala. Hapa tunazungumzia hotuba ya Rais na siyo yaliyojiri kwenye kampeni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge endelea, kwa sababu Rais ameeleza jinsi walivyofanikiwa kuweka wanawake wengi kwenye uchaguzi ule. Nadhani yuko sahihi tu. *(Makofi)*

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunilinda. Naomba niendelee katika suala hili hili. Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais kuna kipengele kilichozungumzia haki sawa kwa wanawake kupewa nafasi za maamuzi. Ndiyo maana nazungumzia hili la mwanamke anavyonyanyasika wakati yuko kwenye mchakato wa kuzitafuta hizi nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kabisa kuona kwamba watu wenye uelewa wanajiingiza kwenye vitendo vya kumnyanyasa mwanamke. Nitashangaa kusikia mmoja wetu hapa atasema kwamba hakutokana na mwanamke. Sisi tuliokaa ndani ya Bunge hili wote tumetokana na mwanamke. Kwa hiyo tumheshimu mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nijikite moja kwa moja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nakwenda moja kwa moja kwenye kipengele cha pili. Naomba nizungumzie suala la kilimo, wananchi wa Kwimba uchumi wao unategemea kilimo, ufugaji, ujasiriamali na ajira.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza sasa Serikali bado haijaweka mkazo wa kutosha kwenye sekta hii ya kilimo. Nimesema hivyo kwa sababu juzi juzi mnamo mwezi wa kwanza hivi uongozi wa Halmashauri ya Kwimba uliamua kufyeka mahindi ya wakazi wa Ngudu Mjini, walifanya hivyo kwa kudai wanapunguza mbu. Tunaomba ufafanuzi, je, ni kilimo kwanza au ni mbu kwanza.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu niingie kwenye masuala mengine na naahidi nitakwenda haraka haraka kuzingatia muda. Naomba nizungumzie suala la wafugaji. Nikiwa kama mkazi wa Kwimba siwezi kulipuuza suala la wafugaji. Wafugaji wa Jimbo la Kwimba wamekuwa wakiishi kama wakimbizi ndani ya nchi yao. Hawajui malisho ya mifugo yao yako wapi, hawaelewi mifugo yao itanyeshewa wapi. Naomba Serikali ilitazame hili kwa makini na kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na kipaumbele hicho hicho cha pili lakini nijikite kwenye suala la ujasiriamali. Kama unavyotambua Taifa letu lina matatizo ya

ajira. Vijana wetu kama mlivyoona juzi wanaofeli wanajiingiza kwenye ajira za binafsi, maana yake ndiyo ujasiriamali huo.

Mheshimiwa Spika, lakini sioni kama hawa vijana wetu wanasaidiwa vya kutosha ili hatimaye waweze kujiendeleza wenyewe kwa kujengewa mfumo wa kujitegemea. Wakati tunatekeleza hotuba ya Mheshimiwa Rais, naomba tusiwasahau wananchi wa Jimbo la Kwimba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba muda unanitupa mkono. Naomba nijitahidi kwa haraka haraka nizungumzie suala la afya ambalo lipo kwenye kipaumbele cha tisa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Wakazi wa Ngudu, Kwimba tuna tatizo kubwa, tuna hospitali ya rufaa ambayo ina vyoo hatarishi. Nikisema vyoo hatarishi ninamaanisha vyoo vipo, lakini ukivitumia unatafuta magonjwa mengine, kwa sababu havitumikiki.

Mheshimiwa Spika, naomba wahusika wote au Serikalini au Halmashauri ya Kwimba ilichukulie suala hili kama dharura, kwa sababu tutaendelea kupoteza maisha ya wananchi wetu kwa uzembe ambao nadhani unaweza ukatafutiwa ufumbuzi mara moja. Suala la kuwa na vyoo vichafu si suala la bajeti ya Serikali, ni lazima tuanze sasa kutatua matatizo yetu bila kutegemea Serikali kuja kututatulia. Suala la kusafisha vyoo ni suala la watendaji.

Mheshimiwa Spika, naomba popote walipo walizingatie hili. Siwezi kumaliza bila kukupongeza kwani sasa hivi tunajivunia nafasi yako. Mwanamke yeyote Mtanzania akitoka nje ya nchi anasifiwa kwa sababu ametoka nchi ambayo imepata Spika mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu hutanigongea kengele kwa sababu naomba niendeleze kidogo hili. Mwaka jana kwenye tarehe 13 mpaka 14 Julai, nchini Austria huko Vienna, Maspika wanawake duniani walikutana wote kwa pamoja na waliazimia kupinga ukatili kwa mwanamke.

**SPIKA:** Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

Nakushukuru sana, natamani nisikie hilo, lakini lazima nitende haki. Lazima nitende haki lakini ningependa kusikia hiyo habari. Mbona hujaniambia. Ningekuwa nimeisikia. Waheshimiwa Wabunge tuna hizi dakika chache tulizonazo hatuwezi kumpa nafasi mwingine. Lakini naomba niwatangazie watakaochangia mchana ili wajiandae. Nao ni Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Ali Hamis Seif, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Kidawa Salehe, Mheshimiwa Sylvester Mabumba na Mheshimiwa Kangi Lugola na wengine watatajwa mchana. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 1100 jioni.

*(Saa 6.54 mchana Bunge lilifungwa*
*hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipokuwa tumesitisha shughuli za Bunge kipindi cha kwanza, niliwataja wafuatao waje wawahi kuzungumza. Mheshimiwa Mendrad Kigola...

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu aliyeniwezesha kufika katika Bunge hili. Pili, napenda kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Mufindi Kusini, walioniwezesha kupata kura za kutosha na sasa hivi nipo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye hotuba ya Rais. Ukweli kabisa katika hotuba hii ya Rais, nimesoma kwa makini sana. Ukiangalia Mheshimiwa Rais, amejaribu kugusa vipengele vyote. Lakini katika masuala yote lengo kuu linaloongelewa katika hotuba hii ni kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Sasa katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini tutafanyaje?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Rais, namshukuru sana kwa sababu ameeleza ndani ya miaka mitano tulifanya nini. Halafu ameeleza miaka mitano ijayo tutafanya nini, kwa hiyo tayari ameshatoa mwongozo wa kufanya. Kwa hiyo, sisi Wabunge, tunaweza kusema kazi kubwa imepungua kwa sababu mpango kazi umeshapangwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo napenda kusisitiza, ni miundombinu. Miundombinu ni tatizo, kwa mfano, katika Jimbo langu katika Wilaya ya Mufindi, ni Wilaya Kubra, ni Wilaya ambayo ina viwanda vingi sana. Ukifika pale, ukitaka kuona Viwanda vya Mbao vipo Mufindi, ukitaka kuona Viwanda vya Chai vipo Mufindi, ukitaka kuona Kiwanda cha karatasi Mgololo kipo Mufindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kitu kikubwa cha ajabu ambacho nimekiona ni tatizo la barabara, tatizo ni barabara inayotoka Nyololo, kupitia Igolole, Sawara inakwenda mpaka Kiwanda cha Chai, maeneo haya yana hali ngumu sana. Sasa ukizingatia wawekezaji kule tayari wameshawekeza, kwa mfano, Kiwanda cha Chai kiliwekezwa toka mwaka 1932, mpaka leo lami haipo. Sasa utakuta magari makubwa kipindi cha masika, kwa mfano kipindi kama hiki yanashindwa kusafirisha chai. Sasa naiomba Serikali katika maeneo yale ambayo ni muhimu na ukiangalia katika uchumi wa Taifa letu, Wilaya ya Mufindi inachangia sehemu kubwa sana. Sasa kama Wilaya inachangia sehemu kubwa ni kwa nini ikose lami? Naomba Wilaya ya Mufindi ipewe kipaumbele, iweze kupewa msaada wa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili nakuja kwenye umeme. Ukitaka kuinua uchumi ni lazima uhakikishe suala la umeme linakuwa imara. Sasa hivi ni kipindi cha masika, kila mtu anaelewa, inatakiwa tuwe na umeme wa kutosha. Lakini sasa hivi umeme bado tunapata shida ni wa mgao. Tatizo kubwa linalokuja ni tunalenga umeme wa maji;

naomba wasomi wenzangu wajikite katika kufanya utafiti wa kutosha ili tuweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kuna siku moja nilitembelea Wilaya ya Njombe, kuna jamaa mmoja anaitwa Pwagu. Yule Pwagu ni darasa la saba, yule jamaa mpaka sasa hivi ana uwezo wa kuzalisha umeme na kuutawanya kwenye kijiji chake. Sasa ni kwa nini sisi tusiende tukajifunze kwa mtu wa darasa la saba ambaye anaweza akatawanya umeme kwenye kijiji chake? Pia ni kwa nini sisi Watanzania tutegemee umeme wa maji badala ya kugundua hata umeme wa upepo, ni masuala ya kujiuliza. Sasa je, kwa mfano, ikija kutokea mabwawa yote yanakauka, maana yake tutakaa giza mpaka lini? Bila umeme uchumi hautakua hata siku moja. Naomba katika Bunge hili Tukufu, kuanzia Mawaziri mpaka Wabunge, tutoe ushirikiano mkubwa, tuache kunyoosheana vidole, sasa hivi tusimamie uchumi, itakuwa ni suala la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakuja suala lingine ambalo linajitokeza sasa hivi, Wabunge wengi wamechangia kuhusu elimu. Serikali imejitahidi sana kujenga sekondari katika kila Kata. Napenda kuipongeza imefanya kazi nzuri sana, lakini suala linalojitokeza sasa hivi ambalo linatubana, sawa kuna tatizo la Walimu na hilo linaeleweka na sasa hivi Serikali imeshajikita kusomesha Walimu wengi sana. Sasa suala linalokuja ni je, hawa Walimu wote tunaowasomesha watakuwa Walimu na watakwenda kufundisha? Mwingine anaweza akasomea ualimu halafu asiende kufundisha, hiyo ipo.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linalojitokeza katika nchi yetu hii ni mishahara midogo. Katika hotuba yake Rais, amejaribu kueleza, amesema, sasa hivi ataboresha maslahi ya wafanyakazi. Sasa naomba Serikali ya Awamu hii ihakikishe kwamba Walimu wanalipwa mishahara inayotosha, kuanzia shule ya msingi, kwa sababu Walimu wa shule ya msingi ndio wanaotoa wanafunzi wazuri wanaoingia sekondari. Sasa hivi wanafunzi wanaokwenda sekondari hawafundishiki kwa sababu bado hawajapata elimu nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakuta mWalimu badala ya kwenda kufundisha anaanza kufanya biashara ndogo ndogo. Ukimuuliza anasema mshahara ni mdogo. Sasa hivi ukimlipa mtu mshahara wa shilingi 200,000/= au 100,000/= hawezi kufanya kazi nzuri. Naomba kazi ya ualimu iwe ni kazi ya kukimbilia kila mtu, ukiweka mshahara mkubwa watu wataomba wenyewe. Sasa hivi kazi ya ualimu inaonekana ni kazi ya kudharaulika, wale Walimu wa shule ya msingi ndio waliotufundisha sisi tukafika hapa, wale Walimu wa shule ya msingi ndio waliowafundisha Madaktari, wale Walimu wa shule ya msingi ndio waliotoa Marubani, sasa ni kwa nini walipwe mshahara mdogo? Naomba Serikali iangalie sana, kwa sababu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ameshaongelea, kwamba ataboresha mishahara, naomba sekta ya elimu iboreshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda niongelee ni suala la kilimo kwanza. Suala la kilimo kwanza, nakumbuka hata huko nyuma tulikuwa tunasema siasa ni kilimo. Kwa hiyo, napenda tusiige, siasa ni kilito, inawezekana kuna sehemu fulani tulishindwa lakini tusiige zile mbinu tulizozitumia kipindi kile. Naiomba Serikali hii kama tumejikita kwenye kilimo kwanza, tuhakikishe kilimo kinakwenda. Sasa tunaita

kilimo kwanza, bado mkulima anatumia jembe la mkono! Tunaita kilimo kwanza bado *power tiller* zinagawiwa kwenye vikundi. Naomba *power tiller* zigawiwe kwa mtu yeyote anayeweza kulima, kwa mwendo huu hatutafika mahali panapotakiwa. Sasa hivi bei ya mbolea imepanda sana, mfuko mmoja unauzwa kuanzia 37,000/= mpaka 40,000/= kwa *DAP;* kwa mkulima wa kawaida hawezi kununua hata siku moja.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna watu wengine wameanza kupanda mahindi bila kuweka mbolea, hivi unategemea atapata magunia mangapi katika eka moja? Kama tumeamua kujikita kwenye kilimo kwanza, tuwekeze. Tupeleke matrekta, kuna watu wanaweza kununua matrekta, tuweke ruzuku kwenye matrekta ili waweze kununua. Hizi *power tiller* sio tulenge kwenye vikundi tu, tulenge kwa wakulima wote. Nakumbuka miaka ya nyuma wakati sisi tukiwa wadogo, mkulima akifanya vizuri, alikuwa anapewa motisha ya trekta. Nakumbuka katika Mkoa wa Iringa, kuna mkulima mmoja enzi za Mwalimu Nyerere, aliwahi kupewa trekta kwa sababu amelima vizuri. Sasa ni kwa nini sisi tusifanye hivyo? Naomba tudumishe kilimo kwanza kwa kuwaangalia wale wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limeongelewa ni haki za utawala bora katika sheria. Kwenye Jimbo langu kuna tatizo kubwa sana, hasa Kiwanda cha Mgololo. Kuna watu pale waliachishwa kazi muda mrefu, sasa hivi ni miaka mitano imepita. Wale wafanyakazi wa Mgololo mpaka leo hawajalipwa haki zao, wako pale na wanakaa kwenye nyumba za wafanyakazi. Sasa kwa bahati nzuri kwenye hotuba ameelezea kwamba Serikali itashirikiana na Mahakama. Sasa mimi naomba, kuna watu pale wanapata shida sana, wanakaa kwenye makambi yale mpaka leo ni miaka mitano na wengine wameshapoteza maisha yao. Sasa naiomba Serikali isukume, kama ni kesi iishe, watu waangalie utaratibu mwingine. Mpaka saa hizi ninapoongea, kule wana shida kweli, wanashindwa hata kusomesha watoto. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, suala lingine, naomba niongelee masuala ya afya.

**WABUNGE FULANI:** Kengele ya Pili.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Ya Pili?

**SPIKA:** Ni ya kwanza.

**WABUNGE FULANI:** Ya Pili.

**SPIKA:** Ya Pili? Eenh?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo, ni kengele ya pili.

**SPIKA:** Ni ya pili naambiwa. Haya ahsante sana, umesema vizuri.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii jioni hii ili niungane na Wabunge wenzangu, kutoa mawazo yangu kwenye hotuba ya mpendwa wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete. Nianze kwanza kwa kuwashukuru wana Tandahimba wote walionirudisha tena kwa awamu ya pili Bungeni hapa.

Mheshimiwa Spika, napenda tu niwaambie wana Tandahimba wote kwamba nitawapa ushirikiano mkubwa kwa maana najua unapokuwa unagombea kwenye upinzani wa vyama vingi vya siasa mambo yakiisha unakuwa Mbunge wa wote. Lakini nitoe rai kwa Watanzania wote wakiwemo na wana Tandahimba, kwamba sasa tuanze kushirikiana uchaguzi umekwisha. Tulikuwa tunatafuta fito za kujenga nyumba yetu ya maendeleo ambayo ni Jimbo la Tandahimba na nchi yetu ya Tanzania, fito zimepatikana ambazo ndio sisi viongozi. Viongozi wa vyama vyote tushirikiane bila kujali unatoka CHADEMA, *CUF, UDP* na kadhalika tushirikiane tuijenge Tanzania yetu kwa umoja. Lakini pia nimeshuhudia vijembe vijembe hapa vikitembea kwa wenzangu waliotangulia kusema kutoka kwenye vyama vyote vya siasa vilivyomo Bungeni, nataka tu niseme jambo moja kwamba tukumbuke, ukitafuta heshima kwa gharama kubwa, utanunua dharau kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye hotuba ya Rais. La kwanza nitachangia kuhusu kilimo. Kama inavyojulikana katika nchi yetu mchango mkubwa na maendeleo makubwa yanachangiwa na kilimo, lakini niseme tuna tatizo kubwa kwenye eneo hilo la kilimo hasa la kutowasaidia sana wakulima wenyewe. Kwa mfano, kwenye zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, kule kwenye korosho gharama ya kupata pembejeo ni kubwa, gharama ya kulima kwenyewe ni kubwa, lakini inapofika wakati wa kupata malipo ya mazao ya korosho hizo kunakuwa na michango mikubwa mno inayowaathiri wakulima. Ndio maana wakati mwingine unakuta watu wanaandamana pamoja na kuwepo mfumo mzuri wa stakabadhi ghalani, lakini wanaandamana baada ya kuona makato wanayokatwa ni mengi na hasa wakipiga mahesabu gharama waliyoifanya na michango inayokatwa.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa Serikali, wakati fulani Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Kayanza Peter Pinda, alitembelea Tandahimba akapata malalamiko ya wananchi pale yakiomba wapunguze gharama ya makato yaliyoko kule, alitoa maagizo kule; lakini maagizo yale hayajafanyiwa kazi kwa nguvu sana, kidogo imepunguza lakini bado michango ile ni mikubwa, itaendelea kuwaumiza wakulima na kwa hiyo kupunguza kasi yao ya kufanya kilimo cha kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kule kwenye zao la korosho sasa hivi, mkulima anatakiwa akatwe michango ya karibu 245/= kwa kuchangia unyaufu, unachangia Chama cha Msingi kama 50/=, *TANECU* 21/=, utunzaji wa ghala 15,000/=, Halmashauri yenyewe inapata 5% na ni michango mingi. Lakini Mkulima huyo huyo anatakiwa achangie zahanati, shule ya sekondari, mambo ya pale kijijini kwake, vituo vya afya na kadhalika. Jambo hili linamletea mzigo mkulima na kwa hiyo linamvunja mori wa kufanya kazi kwa bidii. Tuangalie mara mbilimbili eneo hili ili wakulima wetu wajisikie uimara na kuepukana na unyonge wa kulalamikia makato haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni tatizo ninaliona ni watendaji wetu. Rais wetu ana mapenzi mazuri na Watanzania. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, inaonesha wazi ina mapenzi mazuri na Watanzania lakini baadhi ya watendaji wetu wana urasimu na ugumu wa kufanya maamuzi kwa haraka na hii ndio inatuletea matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano, kuna wakati fulani Wizara ya Nishati na Madini ilitudokeza hapa kwamba baada ya kupitisha kwa shida sana hapa Sheria inayoyataka makampuni kuwekeza kwenye umeme, wakabahatika *ARTUMAS* wakawekeza kule Mtwara na kwamba sasa usambazaji wa umeme ungekuwa ni wa rahisi na sisi wanasiasa tukatumia *loophole* hiyo kuwahamasisha watu wetu umeme unakuja. Pamoja na kwamba ni kweli umeme umefika, Tandahimba, Newala, Masasi, ule wa gesi asilia, naomba niipongeze Serikali kwa eneo hili, lakini kuna mapungufu madogo madogo. Watu wametarajia kupata umeme wa bei nafuu, lakini leo tunaambiwa ati *EWURA* imekaa na *documents* zilizokuwa zinasaidia kupata *relief fund* kutoka *Holland* ya karibu *Euro 28,000* ambayo zingesaidia kusambaza umeme kule vijiji vya Tandahimba na Newala na pia ingesaidia kuongeza kwenye gridi ya Taifa umeme wa karibu *megawatt* 300 na ushee.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake wamekaa na *documents* zile zaidi ya miezi sita, *Holland* wameondoa mpango ule. Hivi, Serikali imefanya nini na watendaji wale wa *EWURA* ambao wametusababishia kukosa kafungu kale ambako kangesaidia kuongeza umeme wetu kwenye gridi ya Taifa na wananchi wakajisikia *comfortable?* Lakini tupo tunawaangalia tu. Nadhani tunatakiwa ku-*revisit* namna ambayo tunafanya *vetting* kwa watendaji wetu, hawatutakii mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninaloomba niliseme hapa, ni lile katika *page* 28 ya hotuba ya Mheshimiwa Rais, ametaja suala la kuanzisha ujenzi wa vyuo vikuu katika kila Kanda. Nataka niikumbushe Serikali hapa kwamba katika Ilani ya uchaguzi ya 2005 ya *CCM*, ilitaja suala la Chuo cha Ualimu, Mtwara kuwa Chuo Kikuu Kiambata. Jambo hili halikufanikiwa kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, natoa rai, sasa tuanze na pale Mtwara, tuhakikishe kwamba sasa panaanza kwanza Chuo Kikuu pale na ndipo tuende pengine, maana ile Kanda ya Kusini hatuna Chuo Kikuu. Naomba niwapongeze wenzetu Wamisionari wa *St. Augustine,* wameweka pale angalau sasa wanafunzi 2,000 wanakuja pale, lakini bado haitoshi, mahitaji ni makubwa.

Mheshimiwa Spika, pia lipo tatizo la muda mrefu tumekuwa tukilisema hapa, la ujenzi wa hospitali ya rufaa. Ndugu zangu, kule tunateseka, hatujatengeneza mazingira mazuri ya watu kule. Kuishi katika mazingira mazuri ya kupata elimu kwa urahisi, ya kupata matibabu kwa urahisi. Tubadilike sasa, tu-*concentrate* na kule, barabara si ndio hiyo inamalizika? Ndugu yangu Dokta Magufuli hapa, amenihakikishia katika muda wa miezi sita ijayo barabara inakwisha. Basi panapokwisha barabara pawe na hospitali ya rufaa inakaribia kukamilika na Chuo Kikuu cha umma kianzie kule tufanane na maeneo mengine ya kanda hii.

Mheshimiwa Spika, sina matatizo na mpango wa kuendelea na kila Kanda, lakini ningeshauri tuanze kule kwa sababu kama tunavyojua ndio tulikosimama kwenye mambo ya kusaidia ukombozi wa wenzetu wa Kusini mwa Bara la Afrika ikiwemo Msumbiji. Kutokana na hilo hatukupiga maendeleo ya haraka na sasa mtufikirie tusogee mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba kutoa mchango wangu kwenye suala la maji. Sehemu kubwa ya Tanzania ina matatizo makubwa ya maji na wilaya ya Tandahimba na Newala, nafikiri zinaongoza na jambo hili ni la kihistoria. Naomba sasa tuweke mkakati maalum wa kuhakikisha maeneo yote yenye matatizo makubwa sana ya maji, tunamaliza matatizo hayo halafu tuende kule ambako kuna nafuu kidogo. Lakini nashangaa kwa kiasi fulani, tupo na wakala hapa wa uchimbaji wa visima virefu na vifupi, *DDCA*, hatujawatumia vizuri. Ukifika pale yaani hawajawezeshwa hali yao ni mbaya sana, kwa nini tusiwaongezee mtaji, tuwawezeshe wale ili wakaribie kumalizia tatizo hili kwenye maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwa kuanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima na kuweza kusimama hapa leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili nakishukuru Chama changu, Chama cha Wananchi *CUF*, kwa kuniteua na hatima yake wananchi wa Jimbo la Mkoani wakanipa kura. Tatu, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mkoani kunipa kura zilizotosheleza na leo naendelea kuwa Mbunge kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Rais katika ufunguzi wa Bunge hili la Kumi alikuwa na vipaumbele kumi na tatu, kati ya hivyo, cha kwanza ni umoja na amani. Kama inavyoeleweka kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano, kwa hivyo, kunapoonekana ishara ya kutokuwa na amani Zanzibar basi hali kadhalika inaathiri Tanzania Bara au Tanzania kwa ujumla. Uwepo wa Serikali ya Kitaifa Zanzibar, umeondoa wasiwasi wa kutokuwa na amani katika Zanzibar na umeleta umoja.

Mheshimiwa Spika, sasa yote haya anayebugudhi habari hizi za kweli hatumfahamu, kwa kweli tuseme nia yake ni kwamba, Wazanzibar waendelee kupigana

na kufanyiana mambo ambayo si ya kistaarabu. Niseme kuwa viongozi wawili waliochukua hatua hizi za kuleta maridhiano inawezekana walichukua historia za chaguzi nne ambazo zimefanyika Zanzibar katika mfumo wa Vyama Vingi, chaguzi ambazo zilianza mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa yako uchaguzi wa mwaka 1995 kwa matokeo ambayo yametajwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, CCM ilishinda kwa asilimia 50.2 na *CUF* ilipata asilimia 49.8. Huu ni uchaguzi wa mwanzo wa Vyama vingi Zanzibar, karibu asilimia 50 kwa 50. Lakini vile vile uchaguzi huu wa 2010 ukiachana na zile chaguzi mbili za 2000/2005 lakini huu wa 2010 kwa sababu ya muda haupo, CCM kwa mujibu wa taarifa ya Tume ya Uchaguzi ilishinda kwa asilimia 50.1, *CUF* ikawa mshindi wa pili kwa asilimia 49.1.

Mheshimiwa Spika, sasa matokeo kama haya busara gani zitumike katika kuwaokoa wananchi wa visiwa hivi. Kwa hiyo, nadhani kilichofanyika ni sahihi, kwa hiyo, ipo haja ya Watanzania wote kwa ujumla wetu kukiunga mkono kwa kweli kilichotokea Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi namshukuru sana Rais Mstaafu Mheshimiwa Karume na Katibu Mkuu wa Chama cha *CUF*, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, na pia namshukuru Rais Dokta Ali Mohamed Shein kwa kusimamia na kutekeleza maamuzi ya Wazanzibar kwa kupitia kura za maoni ambayo walisema wanataka Serikali ya Kitaifa kwa asilimia 66.4. Nampongeza Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na nampongeza Balozi Mheshimiwa Seif Ali Idd kwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumezuka maneno hapa, ya Wabunge na Majimbo yao. Nahesabu unapowahusisha Wabunge na ukubwa wa Jimbo na udogo wa Jimbo, nahesabu huo ni ubaguzi, kubaguliwa anayebaguliwa sawa lakini tatizo moja la ubaguzi haliishii hapo, utawabagua wale ambao unawaona watu ambao hampo pamoja, ukimaliza hapo utakuja kuwabagua wale ambao mpo pamoja, tahadhari ni hiyo tu. Kwa hivyo, nashauri hii si habari nzuri na kwa kweli ipo haja iachwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha saba ambacho Mheshimiwa Rais alikieleza ni suala zima la kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali Kuu na Mitaa na kuweka nidhamu ya matumizi. Ni sahihi kusema hivyo na vizuri kutekeleza lakini naomba niiambie Serikali kuwa njia moja ambayo nahisi inavujisha mapato ni misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke Tanzania ni nchi maskini, ina matatizo mengi, bajeti bado tegemezi, kwa hivyo, nakubali vilevile kuna taasisi na mashirika yanahitaji kusamehewa kodi, lakini kwa kweli kusamehe kodi kwa kupitiliza kwa kweli ni kuwabebesha mzigo wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa taarifa ambayo ameitoa iliyoishia Juni, 2006, Serikali ilisamehe shilingi bilioni 15,970,713,769/= kwa mwaka 2006. Kuna utatanishi mkubwa, Hazina

wanasema yao na *TRA* wanasema yao, siendi huko wakati hauniruhusu. Lakini ripoti hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya 2009 inayoishia Juni, fedha ambazo Serikali imesamehe, ni 752,398,800,000/=.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia pesa hizi leo nchi imetikisika kutokana na *DOWANS*, 94,000,000,000/=, lakini ukichukua hesabu ya bilioni 752 hizi ni *DOWANS* nane, Serikali imeweza kusamehe pesa hizo, kwa sababu *DOWANS* imetangazwa kwa hiyo hata Serikali inasema itafute mbinu ya kuweza kuona uwezekano wa kutolipwa lakini hizi ni *DOWANS* nane. Sasa hali hii kwa kweli ni ngumu. Kwa hiyo, nahisi katika njia moja katika kuboresha mapato ni suala zima la misamaha ya kodi, ipunguzwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna masuala ambayo mashirika ambayo tulitegemea sisi yachangie uchumi wa Serikali kinyume, Wizara ya Afya ambayo yahitaji ipewe ruzuku na Serikali hata Shirika la Reli nalo hivyo hivyo wakati Shirika la Reli ni Shirika la kiuchumi litoe mchango kwa Serikali, Shirika la Ndege *ATCL* sijui hilo liko wapi, umeme ndiyo hali kadhalika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu. Nami napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake nyingi kwa kunijalia na kunirejesha tena katika Bunge hili la kumi, si kwamba nilikuwa bora kuliko wengine lakini kwa rehema zake ilimpendeza kunirudisha ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, napenda niwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Kigoma kwa kuweza kunichagua kwa kura nyingi kunirejesha tena katika Bunge lako Tukufu, nawashukuru sana, Mwenyezi Mungu awabariki, nazidi kuwaomba ushirikiano wanawake pamoja na wanaume na wananchi wote wa Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, nami naomba niungane na wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri inayotoa mwelekeo wa 2010/2015, hotuba yake ni nzuri imesheheni mambo mengi. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuupa kipaumbele Mkoa wa Kigoma. Mkoa wa Kigoma tumependelewa sana, kati ya Mikoa aliyokuwa akiimba kwamba inampa kukosa usingizi ni pamoja na Mkoa wa Kigoma. Nafurahi kwamba tumepewa kipaumbele, sasa mawasiliano na uchumi vimefunguka. Kwa nini ninasema hivyo? Kwa sababu tayari barabara za kutoka Kigoma kwenda ndani na nje ya Kigoma zimefunguka na huu ni msingi bora kwa sababu kiuchumi barabara zikifunguka najua kabisa tutaweza kujiinua kiuchumi. *(Makofi)*

Barabara hizi zimefunguka na ninajua mkoa wa Kigoma ni lango kuu la uchumi Kitaifa na Kimataifa, kwa hiyo kwa kupitia Bunge hili namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuukumbuka Mkoa wa Kigoma. Tulichelewa lakini naamini tutafika. Naomba niwaambie wananchi wa Mkoa wa Kigoma kwamba, tulichelewa lakini sasa tunaanza kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo, barabara ya kutoka Mwandiga-Manyovu imekamilika, barabara ya kutoka Kigoma kuelekea Uviza Tabora inaendelea kujengwa na sasa hivi barabara ya kutoka Kidawe, kwenda Kasulu-Kibondo, mpaka Nyakanazi, sasa hivi tangazo la kumpata Mhandisi Msimamizi kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 50, mchakato tayari umekamilika, mwezi wa nne utaanza. Kwa nini tusimshukuru Mwenyezi Mungu kwa hicho ambacho tayari kimekwishaanza kupatikana. Naomba wananchi wa Kigoma wawe wavumilivu na wasisikie maneno yanayozungumzwa lakini mwenye macho haambiwi tazama. Mwaka huu 2010 ni tofauti na miaka mitano iliyopita, ukienda Mji wa Kigoma unang'aa kwa sababu barabara ni nzuri, ndiyo maana Mheshimiwa Serukamba aliposimama na Mheshimiwa Zitto hawajasemea barabara kwa sababu wanajua tayari mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo mwaka 2005 barabara ya Kigoma-Kasulu-Kibondo-Nyakanazi ilikuwa kwenye upembuzi yakinifu, lakini sasa upembuzi tayari umeshakamilika, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo. Najua kabisa kwa sababu Mkoa wa Kigoma tumewekwa kwenye mikoa sita ya kilimo kwanza naamini hata viongozi wetu wanafahamu kwamba barabara hiyo ya Kigoma-Nyakanazi ndiyo kiunganishi kikubwa cha Wilaya zote tatu kwa maana ya uchumi. Kwa hiyo, naamini kabisa kwa sababu walishatuweka kwenye mikoa sita ya uzalishaji wa chakula watafanya haraka kujenga barabara hiyo ili tuweze kupitisha pembejeo kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nisiishie hapa, naendelea kumpongeza Rais, Mheshimiwa Rais alisema kwamba Wilaya zote ambazo hazijapatiwa umeme zitapatiwa umeme. Namshukuru Mwenyezi Mungu, Wilaya ya Kasulu na Kibondo, tayari mashine zimeshapatikana na sasa hivi Mirangirangi zinaendelea kusimikwa na nyaya zinatandazwa, najua kabisa muda si mrefu umeme utawaka. Tunaishukuru Serikali ya CCM, kwa kuweza kutekeleza ilani, tunashukuru sana Serikali kwa kutekeleza ilani, kwa kweli mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma uliwahi kuwa Chuo cha Kilimo, Chuo cha Mbondo, naomba kwa kupitia Bunge hili kwa sababu sasa mkoa wetu umewekwa kwenye ile mikoa sita *the big six*. Naomba chuo kile kirejeshwe ili kiweze kuzalisha wagani kazi na wagani kazi wale waweze kusambazwa vijijini kwa ajili ya kwenda kusimamia mambo ya kilimo kwanza. Naomba kupitia Bunge hili wataalam wanaohusika Mheshimiwa Waziri na Bahati nzuri Naibu Waziri anatoka Kigoma. Naomba hili aliangalie na alichochee ili tuweze kurudishiwa Chuo kile cha Kilimo kiweze kuzalisha wataalam zaidi kwa ajili ya kwenda kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie *SACCOS* na VIKOBA, naomba wataalam waende vijijini kuendelea kuwaelimisha wananchi, kwa sababu baadhi ya wananchi elimu hiyo haijawafikia, kwa hiyo, hawajajua ni jinsi gani wanaweza kujiunga pamoja wakaweza kunufaika kwa kupitia VIKOBA na *SACCOS* na kwa sababu hawajaweza kupata elimu ya kutosha. Naomba kupitia Bunge hili, Maafisa Ushirika wasikae ofisini waende vijijini wakatoe elimu kwa wananchi ili waweze kujua ni jinsi gani wanaweza kujiinua kiuchumi kwa kupitia vikundi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vile vile wananchi wanahitaji elimu kwa sababu wengine wakikopa wanaweza wasirejeshe wakaishia jela au kunyang'anywa mali zao. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema kwamba, naomba Serikali itafute ni jinsi gani inaweza ikapata pesa kuwapeleka wataalam kwenda kuwafundisha wananchi jinsi gani ya kuweza kuanzisha vikundi vya *SACCOS*, kuanzisha VIKOBA. Lakini vile vile waweze kujua ni jinsi gani wakipata pesa kupitia vikundi hivyo ni jinsi gani wanaweza kutumia pesa hizo ziweze kuwasaidia kujiinua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la afya kidogo, vituo vya afya vimejengwa, zahanati zimejengwa lakini hazina Waganga wala Wauguzi. Nafikiri labda pengine, kwa sababu wako wanafunzi wengine bahati mbaya huwa hawapati nafasi za kwenda vyuoni na kwa sababu tatizo hili la kupata Waganga na Wauguzi limekuwa ni kubwa. Basi utafutwe utaratibu, wale watu ambao wanaishi kwa mfano, sisi kwetu Kigoma watu wakipelekwa kule Kigoma hawaendi basi wachukulie watu wa kutoka Kigoma wapelekwe vyuoni wasome ili waje kukabiliana na mazingira yale waliyoyazoea kwa sababu inakuwa vigumu, pengine mtu umemtoa Dar es Salaam unampeleka Zeze pengine anaweza asiende kwa sababu amezoea umeme, amezoea kuona lami, sasa anaenda kupamba na tope. Akifika Kigoma Mjini wakimwambia unakwenda Kasulu na huko kuna tope, anageuza anarudi alikotokea.

Mheshimiwa Spika, najua kabisa wataalam hawatoshi, lakini tunaomba mliangalie hili ikiwezekana wale wanaotoka maeneo husika wanaomaliza *form four* wachukuliwe wapelekwe vyuoni wakajifunze ili warejee vijijini kwao kwenda kuwasaidia wananchi. Najua hili ni gumu kwa sababu mara nyingi tumekuwa tukiomba wanafunzi waliomaliza Kasulu wapelekwe kwenye Vyuo ambavyo vipo Kasulu ili wakimaliza vyuo vile wapelekwe……

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kumshukuru mke wangu Rose, pamoja na Chama changu, Chama cha Mapinduzi kilichoniteua na wananchi wa Njombe Kaskazini kwa kunipa heshima ya kuniingiza mjengoni. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa namna ambavyo wameunga hoja za Mheshimiwa Rais hotuba ambayo aliitoa wakati anafungua Bunge hili. Kwa namna ambavyo hotuba hii imeelezea kazi zilizofanyika ndani ya miaka mitano na mwelekeo wa kazi wa vipaumbele kumi na tatu kuanzia mwaka 2010/2015. Lakini wako watu ambao wanabeza kwa kazi ambazo zimefanyika kwa kipindi cha miaka mitano. Nimpongeza sana Rais kupitia Chama chetu cha Mapinduzi, kazi zimefanyika nyingi nzuri na zinaonekana.

Mheshimiwa Spika, niwakumbushe wenzangu mahali padogo tu, nchi yetu ilikumbwa na tatizo la ujambazi ambalo ilifikia mahali imani kwa watu ilianza kutoweka kwa namna ambavyo watu walikuwa wanatembea wakiporwa fedha mbalimbali. Lakini jambo hili alilivalia njuga sana, kama mnakumbuka na likapungua. Hata kama halijakwisha lakini angalau limefika mahali pazuri watu wanaweza kutembea na fedha zao mfukoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine niwakumbushe ndugu zangu, suala la elimu limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Lakini napenda nizungumzie kwamba katika suala la elimu katika Mkoa wa Iringa, Mkoa Rukwa, Mkoa Mbeya na Mkoa wa Ruvuma huko nyuma historia inatuambia kulikuwa na sekondari moja tu katika Mikoa hii minne, nayo ilikuwa ni Malangali peke yake. Leo hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Iringa peke yake una shule za sekondari zaidi ya 240, jamani tumefika mahali pazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini niongeze tu kwamba, kilio hiki ambacho Taifa kimelikumba, watoto wetu ambao hawakufanya vizuri mtihani wa kidato cha nne hii juzi, maana inaonyesha takwimu kwamba watoto waliofanya mtihani walikuwa zaidi ya laki tatu na kitu. Waliofaulu ni 38,000 watakapofanya mtihani kidato cha sita inaonyesha hapa wanaweza wakafaulu kwa mfano, 20,000 katika vyuo vyetu vikuu ambavyo vipo kipindi cha kujiunga na mwaka wa kwanza kwenda vyuo vikuu, vyuo vitakuwa havina wanafunzi kwa sababu watakuwa ni wachache sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze suala sasa linalogusa Jimboni kwangu. Tatizo la upande wa barabara ambalo Mheshimiwa Rais amelizungumzia. Tuna barabara ya kutoka Njombe – Lupembe barabara hii ni barabara ya kiuchumi barabara ambayo kuna chai nyingi kule Lupembe na mbao. Naiomba sana Serikali itazame kwa jicho la huruma barabara hii kwani imekuwa ikiingizia Taifa pato kubwa.

Kipindi cha masika barabara hii hasa huu mwezi wa tatu kuna maeneo korofi mengi ambayo huwa hayawezi kupitika. Kwa hiyo, niiombe Wizara ya Miundombinu iangalie kwa jicho la huruma suala la barabara ya Njombe – Lupembe.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala la kilimo. Naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri ambayo inaifanya juu ya kilimo hasa ukizingatia ruzuku ambayo wanapewa wakulima kuhusiana na mbolea na mbegu. Mbolea hii ambayo wameizungumzia naiomba Serikali watu wanaoagiza hii mbolea imekuwa na bei tofauti sana ambapo imeonekana kwamba hii mbolea ukienda sehemu zingine inauzwa shilingi

45,000 ukienda sehemu zingine inauzwa shilingi 48,000 mpaka 50,000. Ukichanganya na ruzuku ambayo inayotolewa 26,000 unapata karibu shilingi 70,000 mpaka 72,000. Kwa hiyo, Serikali itupie macho kwa watu wanaoagiza mbolea hii ili bei ziendane kwa nchi nzima. Hata hivyo, labda Serikali itoe soko huru ili kila mmoja aweze kuagiza kwa masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nizungumzie suala la maji katika eneo la Jimbo la Njombe Kaskazini. Lupembe ni Mji Mkongwe, wa siku nyingi lakini watu wale tangu wapate uhuru kumekuwa na tatizo la maji ambalo tatizo hili limedumu kwa muda mrefu. Ingawa juzi nimeongea na Waziri wa Maji kumpa taarifa hiyo amenambia ataishughulikia. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la umeme. Suala la umeme pale kwetu Makambako ni tatizo. Umeme ambao wananchi wangu wanapata, wale wa Makambako pembezoni, ukiingia pale Makambako, karibu hata kilomita moja haifiki yaani nje kidogo, watu wale unadhani wanaishi kijijini kabisa wakati wako ndani ya mji. Tunaomba angalau jambo hili litiliwe mkazo ingawa tayari nalo nimeshaongea na Waziri wa Nishati na Madini ameniambia atalishughulikia.

Mheshimiwa Spika, unajua shughuli ambazo zimefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi hata baadhi ya watu wamekuwa wakibeza, hata Yesu wakati anakuja kutukomboa, wako waliosema asulubiwe. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Rais hayo yote aendelee kuyavumilia, kazi anayoifanya ni nzuri na amejipanga vizuri katika vipaumbele hivi 13 ambavyo ameviweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimalizie nikupongeze mwenyewe Spika, kwa heshima ambayo tumeipata Watanzania hususan Mkoa wetu wa Iringa kumpata Spika mwanamke, Mungu akubariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwapongeze na wenzangu Wabunge, tushirikiane, sisi ni Bunge moja, tujenge upendo, tujenge uhusiano mmoja na ndio haya yote tunayozungumzia yatakwenda vizuri. Hii ya kutokupendana, tuwaombe wachungaji humu ndani jamani mtuombee, tujenge upendo, tupendane na haya yote yatafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno haya nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa sababu Mheshimiwa Deo amesema nyie wachungaji mlioko hapa, natangaza kuwa Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa anaomba niwatangazie Wabunge wote waliokubaliana kuwa na *fellowship* na maombi ya pamoja waonane baada ya kikao hiki cha Bunge nje ya Ukumbi kwa dakika tano tu. Nadhani wanatekeleza haya anayosema Mheshimiwa Deo Sanga. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Lakini jambo la kwanza kabla sijaanza kuchangia hotuba ya Rais, nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mbozi Magharibi, kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mwakilishi wao. Nawaahidi kabisa kwamba katika miaka mitano nitakuwa Kiongozi bora na wa mfano katika Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, napenda kumshukuru Mwenyezi Bunge kwa kuninyanyua mpaka leo hii kuwa katika nafasi niliyopo, familia yangu ndugu, jamaa na marafiki, wote nawashukuru kwa upendo mmoja.

Mheshimiwa Spika, ningependa nianze na nasaha kidogo kabla sijakwenda kutoa hoja. Nalionea huruma sana Taifa langu. Nalionea huruma Taifa kwa sababu Watanzania wanateseka kwa kiwango kikubwa na tunashindwa kusema ukweli kwa sababu ya maslahi ya itikadi za vyama. Tunakopita, tunapokwenda kila mahali tunaona ni kwa kiwango gani Watanzania wanateseka. Mfano mdogo, ni kila siku asubuhi tunapita, tunakuta katika mageti ya Bunge, watu wanaomba wakiwa na magonjwa mbalimbali. Lakini mtu anafika Bungeni anadiriki kusema hadharani kabisa kwamba nchi inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, hata kama upo ndani ya itikadi ya Chama chako tuongee ukweli katika hali halisi jamani. Taifa lilipofikia kuna mahali tumeshindwa, twende kwa mfumo fulani, kuna mahali tutakwenda vizuri tutakapoweza kukamilisha kwa pamoja, hili ndilo Taifa ambalo tunahitaji. Taifa haliwezi kuwa na amani kama Watanzania wanateseka. Taifa haliwezi kuwa na usalama kama Watanzania wanaendelea kuwa maskini na wanaendelea kulala njaa. Hatuwezi kufika kwa mfumo huu. (*Makofi*)

Napenda kusema kitu kimoja tunahitaji sana na hili ni lazima nitoe nasaha kwamba Kiongozi bora ni yule anayeliombea Jimbo lake na kuliombea Taifa lake kila anapoamka. Lakini sidhani kama hapa kuna viongozi wanaweza kutekeleza hili. Kiongozi bora ni yule anayeweza kujinyenyekeza kwa Mwenyezi Mungu ili yeye aweze kumnyanyua, sio unakaa unajinyanyua kwa kujisifu huwezi kufika mahali popote. Watanzania hawahitaji viongozi wa mfumo huu. Kiongozi bora ni yule anayezihisi sababu zilizomfanya afike mahali alipo, ndio kiongozi bora tunayemhitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya nasaha fupi, napenda niende kwenye kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Hotuba ya Mheshimiwa Rais ina vipaumbele 13 lakini ukiangalia kwa undani zaidi katika vipengele 13 utakuta vingine si vipaumbele, mengine ni mahitaji ya msingi, mengine ni utekelezaji, mengine ni mambo ya kawaida kabisa.

Suala la Utawala Bora, suala la Demokrasia, Suala la Usalama na Amani, Serikali yoyote hata wangeingia CHADEMA wangelinda usalama na amani wa nchi hii, utawala bora wangeshikilia, wangepigana kuhusu rushwa. Tunapozungumzia suala la vipaumbele tunatakiwa tuwe na mambo ya msingi matatu au manne yanajitosheleza.

Tungesema leo ilani ama hotuba ya Rais inahusisha mambo labda matatu, kwamba labda barabara, maji pamoja na kitu kingine, tunazungumzia miundombinu kwa

maana ya barabara. Tunasema hivi vitu ndivyo ambavyo tunasema ndani ya miaka mitano lazima tuvisimamie na Taifa litambue ndivyo tunavyovihitaji. Lakini hatuwezi kusema amani sijui nini na nini ni vitu ambavyo kila mmoja anaweza kuvitekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa nigusie baadhi ya mambo. Katika Hotuba ya Rais, tuzungumze katika uhalisia ili tuweze kufika, tusibishane bila hoja. Kwa hiyo, ndugu zangu napenda niende katika kipengele kimoja kuhusiana na maji kwenye kukuza uchumi, maana yake ni huduma za jamii. Tunapozungumzia maji tunazungumzia uhai wa Mtanzania ndio maana ya maji. Bila maji ndio tunakosa nishati za umeme zinazoyumba, bila maji ndio akinamama unakwenda vijijini ndoa nyingine zinavunjika, akinamama wanakwenda umbali muda mrefu wanachelewa kurudi, waume zao wanawapiga, wanawafikiria vibaya, ndoa zinavunjika. Bila maji ndio haya matatizo yanatokea, watu wanazeeka kabla ya umri wao wanakaa wanateseka ni vitu viko wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huwa najiuliza Serikali kwa takriban miaka 50, hatuzungumzii miaka mitano sasa, kwa sababu Chama ni Kimoja na Serikali ni ya watu wale wale. Kwa hiyo, unaangalia miaka 50 bado tumeshindwa kupeleka maji kwa asilimia angalau 50 ya Watanzania wote, kila siku tunazungumzia hayo malalamiko. Nalizungumzia hili kwa sababu nalijua na nalifahamu. Unakwenda *Bonite* anazalisha maji Kilimanjaro anasambaza nchi nzima mtu mmoja, Dasani anasambaza maji nchi nzima mtu mmoja, sijui uhai, Bakhresa anasambaza maji nchi nzima mtu mmoja, lakini unakuta Serikali inashindwa, unajiuliza maswali mara mbili hupati jawabu. Ni suala la kwenda na kuliangalia kwa makini. (*Makofi*)

Suala la pili ni suala la kilimo kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa letu ambalo Watanzania wengi kwa uwingi wao wanahitaji kupata viongozi ambao watawatoa na kuwaweka katika kilimo bora na cha kisasa. Lakini kwenye kilimo tumekuja na sera ya kilimo kwanza, kwenye kilimo kwanza tumekwenda na kauli mbiu kwamba sasa tuwawezeshe wakulima.

**TAARIFA**

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68 (8) inaelezea kuwa Mbunge anaweza akasimama pale na kutoa taarifa. Mzungumzaji aliyesema *it is very unfortunately* kwamba hakuisikiliza hotuba ya Rais. Sasa katika kuichambua ameichanganya na amechanganywa zaidi na neno kipaumbele akiona kwamba kwenye kipaumbele yametajwa mambo mengi. Lakini Rais alipokuwa anahutubia na kwenye hotuba yake ameainisha kuna mambo makuu matatu aliyoanza nayo kwa hiyo, kwenye kipaumbele unaweza ukawa, kipaumbele kwa kingereza wanasema *priority* na unaweza ukawa na *top priority*. Sasa kuna la kwanza ameongelea kuendelea kuwa na nchi moja, la pili kaendelea kusukuma gurudumu la maendeleo, kukuza uchumi na kupunguza umaskini na la tatu kuhusu demokrasia. Lakini kwa ajili ya upana wa uchumi ndio maana akayaainisha haya kwenye ngazi ya pili ambayo yako 13. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge endelea.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa wala siihitaji. Nakwenda kwenye mambo ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nazungumzia suala la elimu. Jamani elimu imeshuka, unapokwenda katika Taifa la watoto wa kidato cha nne karibu nusu ya wanafunzi wamepata *division zero,* hatuhitaji kujadili mara mbili. Tunakubaliana na ukweli tunaujua. Lazima tukosoe ili mfanye kazi vizuri.

Lakini kitu kingine kinachosababisha elimu kushuka jamani muwe mnasikiliza vilio vya Walimu siyo tu madarasa, siyo maabara siyo maktaba, msikilize vizuri vilio vya Walimu. Mkielewana vizuri Walimu wenyewe naamini kabisa ndani ya mwaka mmoja kiwango cha elimu katika Taifa hili kitabadilika. Lakini kama hili halitaendelea kusikilizwa hata ujenge madarasa mazuri kwa kiwango gani, hata ujaze maabara vifaa vyote na maktaba ukajaza vitabu vya kila aina, elimu itaendelea kubaki vile vile kwa sababu hivi vyote vinahitaji Mwalimu ambaye atawaelekeza wale watu kutoka katika kutokujua kuelekea katika kujua ili kupata mustakabali bora wa elimu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine katika Hotuba ya Rais ukiachilia kwamba anasema sikuisikiliza lakini nimeisoma na nimeielewa. Nimetoka *University* juzi tu akili bado inachangamka. Kwa hiyo, nimejaribu kuipitia kwa umakini sijaona kipengele cha walemavu, watu wenye mahitaji ya msingi katika Taifa hili, watu ambao walizaliwa si kwamba walipenda, tunahitaji namna gani ya kuweza kuwakomboa watu hawa. Lakini tunaitoa na hatuwezi kuigundua.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, bado muda.

**SPIKA:** Kengele ya pili tayari. Sasa namwita Mheshimiwa Kidawa Saleh.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake na rehema zake ameniwezesha kurudi tena katika Bunge lako Tukufu. Lakini pia kwa aina ya kipekee niwashukuru wapiga kura wangu, wajumbe wa Mkutano Mkuu wa UWT, Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kunipitisha kwa kura za heshima kabisa na kunifanya niwe Mbunge wa Bunge letu hili badala ya jina langu kuteuliwa na Tume. Nawashukuru sana na nawapongeza sana. Lakini pia naishukuru familia yangu kwa kuniunga mkono na kuniombea hadi nikafikia hapa nilipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nami naungana na wenzangu kuipongeza Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ni hotuba nzuri ni ya kina na imeeleza kwa upeo mkubwa kabisa mambo yote ambayo yanahitajika katika kuleta maendeleo ya nchi yetu na watu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niungane na Mheshimiwa Rais, kwa kuwashukuru Watanzania kwa kuichagua tena CCM na kuiwezesha kushika dola na kuunda Serikali. Ushindi uliopatikana kwa Chama cha Mapinduzi ni ushindi wa kutosha kabisa wala hauna mashaka. Kwa kutoa kielelezo ni kwamba ushindi alioupata Mheshimiwa Rais, umepitana na mshindi namba mbili kwa kura karibu milioni tatu. Kwa hiyo, takwimu hizi hazina mashaka ni ushindi mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushindi huu haukuja hivi hivi tu bali umekuja kwa kazi nzuri sana iliyofanywa na Serikali ya Chama Tawala, ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi katika kipindi kilichopita. Ni ukweli usiofichika kwamba kazi nzuri imefanywa na inaonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto nyingi ambazo Wabunge wenzangu hapa wamezieleza. Hakuna nchi yoyote ambayo haina changamoto katika kuleta maendeleo na katika maisha ya watu siku zote tunapambana na changamoto. Kuna changamoto katika sekta za elimu, afya, maji, miundombinu, sekta za kijamii na kiuchumi, isipokuwa sisi kama Watanzania tuungane kwa pamoja, wa Vyama tofauti, tuondoe itikadi zetu kwa kujua wote sisi ni Watanzania, tunajenga nyumba moja, tushikamane tulete maendeleo ya nchi yetu. Tuondoe malumbano, tuondoe tofauti zilizopo, tushikamane kwa jina la Tanzania, tuijenge nchi yetu, hii ni nchi yetu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, ukurasa wa nne, ameeleza majukumu ya msingi, lakini nataka nizungumzie lile jukumu namba moja. Naomba kunukuu, amesema:-

*"Kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kuwa nchi moja na watu wake wanaendelea kuwa wamoja, wanaopendana na kushirikiana licha ya tofauti zao za rangi, makabila, dini, maeneo watokayo na ufuasi wa vyama vya siasa"*.

Mheshimiwa Spika, hili ni jukumu la msingi kabisa. Tunahitaji mshikamano, upendo ndani ya nchi yetu. Ni ukweli usiopingika kwamba hivi sasa zimeshatokea cheche za kutuvurugia amani na upendo ndani ya nchi yetu, mojawapo ni cheche hii ya udini. Ndugu zangu Watanzania tusibaguane kwa sababu ya dini zetu, wote sisi ni Watanzania. Ukiniangalia usoni mwangu na ukimwangalia ndugu yangu hapa Susan, huwezi ukasema huyu anatokea dini gani kwa sababu dini ni imani iliyokuwa moyoni mwa mtu. Kila mmoja ana haki ya kuabudu dini anayoitaka na kila dini ni bora kwa yule anayeiamini, tusivurugane kwa dini, tujenge nchi yetu, tujuane kwa Utanzania wetu, tujuane kwa Utaifa wetu, tusijuane kwa udini. Tukiangalia nchi ambazo zimeenda katika upande huo wa udini, ndugu zanguni, zimevurugika sana, hakuna nchi, ni *chaos,* ni balaa, tusifike huko na wala tusielekee huko ndugu zangu.

Mheshimiwa Spika, cheche za ukabila zimeanza kujitokeza sana, tusivuruge nchi yetu ndugu zangu Watanzania. Tanzania imejengwa na makabila zaidi ya 120, tukianza kuvurugana kwa ukabila, nchi yetu itagawanyika vipande vipande, haitatawalika na wala hatutaweza kuishi katika nchi hii. Ndugu zangu hakuna hata mmoja aliyeomba kwa Mungu kwamba Mungu niumbe na niwe katika kabila fulani, ile ni upendo wake Mungu. Kwa hiyo, tusijuane kwa ukabila wetu, tusijuane kwa udini wetu, sisi wote ni Watanzania, tuondoe mambo hayo yatatuvurugia nchi yetu. Tuungane kwa pamoja, tujenge nchi yetu sote, sisi ni Watanzania, tupendane.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kwenda katika mambo ya kiuchumi, nitazungumzia sekta ya viwanda. Viwanda ni sekta moja muhimu katika kuleta maendeleo ya nchi yetu, lakini kusema kweli nchi yetu bado hali ya viwanda vyetu viko duni na ni vichache mno. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itoe kipaumbele na mikakati ya kujenga viwanda vikubwa na vidogo, viwanda vitatusaidia kupata ajira. Tunazungumzia hapa ajira kwa vijana hamna, vijana wanatembea ovyo barabarani, hawana, ajira, kwa hiyo, tukihakikisha kuwa tunajenga viwanda, kwanza, vijana wetu watapata ajira lakini vilevile nchi yetu itapata mapato mengi.

Mheshimiwa Spika, tungeanza kwanza na viwanda vile ambavyo vina *linkage* na kilimo. Watanzania wanaitikia wito wa kilimo, wanalima matunda mengi sana. Juzi nilikuwa natokea Tanga, mimi Kichama ni Mlezi wa Mkoa wa Tanga, nilikwenda kule kwenye matembezi ya mshikamano. Tanga kuna maembe mengi kweli kweli lakini wafanye nini, hakuna viwanda vya kusindika maembe. Nimepita Chalinze pale, pana mananasi ya kupindukia lakini wafanyeje, mananasi yanaoza. Kuna kipindi kunakuwa na nyanya yaani utawaonea huruma wakulima madebe kwa madebe ya nyanya wanayatupa kwa sababu yameshaoza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, tujengeni nchi yetu Watanzania wenzangu kwa pamoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia nafasi hii kwa mara ya kwanza kabisa kusimama katika Bunge lako Tukufu ili nami niweze kuchangia maoni yangu.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe kwa kupata nafasi hiyo kuwa Spika mwanamke wa kwanza katika nchi yetu baada ya miaka 50. Pia napenda kumpongeza sana Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dr. Jakaya Kikwete kwa uongozi wake mahiri katika Taifa hili. Pia kuwapongeza wananchi wa Tanzania kwa mapenzi yao kwa CCM, hadi leo hii chama chetu kinaongoza nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuipongeza familia yangu kwa msaada wao wakati wote wa mchakato wa Kampeni. Nawapongeza wananchi wa Jimbo langu la Dole, kwa mapenzi yao na kwa imani yao kubwa kwangu kunichagua kuwa mtumishi wao, nami naahidi kuwatumikia kwa moyo mkunjufu na wa upendo zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia masuala manne katika vipaumbele ambavyo Mheshimiwa Rais wetu ameviweka katika hotuba yake ya uzinduzi wa Bunge hili. Vipaumbele hivi 13, nasema ni vipaumbele elekezi kwa miaka mitano ijayo. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuunga mkono maelekezo haya ya mpendwa Rais wetu ili Taifa letu liweze kusonga mbele. Mengi yamesemwa hapa kwamba Taifa lina njaa, Taifa lina shida, yote yatakwisha kama sote tukitambua wajibu wetu ambao tunapaswa kuutekeleza hapa ndani ya Bunge hili. Tuondoshe itikadi zetu, tuunge mkono Sera za Serikali yetu ili kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia eneo la umoja, kipaumbele cha kwanza. Kwanza, nayapongeza maoni ya Mheshimiwa Rais wetu lakini naomba Bunge lako Tukufu hao wanaochochea mfarakano katika Taifa letu, Serikali yetu iwadhibiti na hao wanaoleta udini napendekeza wasiruhusiwe kugombea nafasi za kisiasa kwa sababu Taifa letu hawalitakii mapenzi mema.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ni eneo la kukuza uchumi. Nampongeza Rais wetu katika eneo hili na nitazungumzia habari ya kilimo. Naamini kupitia mipango ya maendeleo ya muda mrefu MKUKUTA na MKUZA, Serikali imeelekeza mambo mazuri sana. Naomba Waheshimiwa Wabunge wote kuunga mkono Sera hizo kwa sababu tumelenga ifikapo mwaka 2020 na 2025, Tanzania iwe ni nchi yenye vipato vya kati. Lakini kwa mazungumzo ninayoyaona humu ndani kwamba sisi wenyewe hatuko wamoja, ni vigumu sana kufikia Dira ya 2020 na 2025. Naomba sana tuwe wamoja, tuwe na mapenzi kwa Taifa letu. Naomba sana kupitia Bunge hili, tunapozungumzia habari ya kuwekeza katika kilimo kama njia kuu ya kuajiri Watanzania na kama sekta inayochangia mapato ya Taifa, tuwekeze katika Kilimo cha Umwagiliaji. Kilimo cha kutegemea mvua hakiwezi kutusaidia na mara nyingi kinawakatisha tamaa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi hapa Dodoma tunaona wananchi wamelima sana lakini jua hili linakatisha tamaa. Kama tungekuwa tumewekeza katika kilimo cha umwagiliaji, naelewa wataalamu wa kilimo wanafahamu ile mifumo ya *irrigation* ilivyo kama ile ya *grip irrigation* ambapo maji machache sana hutumika lakini uzalishaji huwa ni mzuri na mavuno huwa ni mazuri.

Mheshimiwa Spika, pia niombe kupitia Bunge hili, Serikali iwekeze katika Vituo vya Utafiti vya Kilimo ili wananchi wetu waweze kutumia mbegu ambazo zimefanyiwa utafiti kwamba zinafaa eneo gani la kilimo, eneo gani la ardhi na wakati gani mbegu zile zitumike. Lakini pia eneo hili la kilimo niombe pia kupitia Bunge lako Tukufu, Serikali yetu ihakikishe wataalamu ugani wanakuwa karibu sana na wananchi vijijini, wasikae maofisini, wao wawe sawa na wakulima kwa sababu wakulima wetu wanahitaji kupata maelekezo ya kiufundi na kiutaalam ili tuweze kuondokana na tatizo la njaa. Nchi yetu Mwenyezi Mungu ameijalia, tunaweza kusema ni Kaanani ya Afrika, yenye kuwa na asali na maziwa. Tuna maziwa makuu, tuna mito mingi basi tukitumia kilimo cha umwagiliaji, tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu nitazungumzia kuhusu kuwawezesha wananchi kiuchumi katika makundi mbalimbali, tuthamini mawazo yao kwa sababu wao ndio

wanaojua kiatu kinabana wapi. Kuwa msomi ni moja lakini kusikiliza ambao unawatumikia ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho, nataka kuzungumzia sekta binafsi. Kila mmoja anaamini kwamba hii ni sekta muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Hata kule Japan si kwamba viwanda vikubwa au sekta kubwa ndiyo ambayo imefanikisha uchumi wa Japan, ni sekta binafsi. Sasa nachopendekeza katika Serikali yetu, ni kuweka mazingira mazuri, wananchi wetu ni maskini, Mabenki yaliyoko sasa hivi yana masharti mengi sana, wananchi wetu hawawezi kumudu masharti yale. Napendekeza kupitia Bunge lako Tukufu, Serikali yetu ijitahidi kuhakikisha Mabenki yanakuwa na masharti nafuu ili sekta binafsi iweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache, naunga mkono hoja na naomba Bunge lako Tukufu liwe linathamini sana maelekezo ya Rais wetu, tumtie moyo kwa mapenzi yake mema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, nawashukuru wananchi wote wa Jimbo la Mwibara kwa kunichagua kuwa Mbunge wao, nawaahidi sitawaangusha. Aidha, namshukuru mke wangu Mary na watoto wangu akina Marietha, wamekuwa nami kipindi chote cha Kampeni. Namshukuru Mchungaji wangu, Samwel Nasali wa FPTC na waumini wote, kwa maombi yao, kweli ukimtegemea Mungu inalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze moja kwa moja kuipongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Rais na hasa lile eneo la barabara, limefufua matumaini ya wananchi wa Mwibara, walishakata tamaa juu ya barabara yao ya kutoka Bunda - Nansio ya kilomita 93 kupitia Kibara - Kisorya na barabara hiyo imepewa kipaumbele namba moja kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mwelekeo wa Rais ni kwamba, barabara zote zilizowekwa kwenye Ilani zitawekwa lami. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kuchangia kwenye eneo la mapambano dhidi ya umaskini kwa mwelekeo wa Rais wetu. Tatizo kubwa la Watanzania ni umaskini uliokithiri na umaskini huo unasababishwa na mambo mengi lakini makubwa zaidi ni mifumo ya kinyonyaji katika maeneo ya biashara ya mazao ya wakulima, mifumo ya unyonyaji katika mazao ya uvuvi, pamoja na Sheria mbalimbali kandamizi na ambazo zinabagua. Kwa nini nasema hivyo? Mwaka 2000 kuna taasisi ilifanya utafiti ikabaini kwamba Wilaya ya Bunda ndiyo inayoongoza kwa umaskini kati ya Wilaya zote za Tanzania. Ninasikitika sana. Leo hii mtu akiulizwa mlima mrefu katika Tanzania unapatikana wapi atasema Kilimanjaro lakini akiulizwa maskini anayeongoza katika nchi hii anapatikana wapi, atajibu Jimbo la Mwibara. Akiulizwa Mbunge maskini kuliko Wabunge wote katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atasema ni Kangi Lugola, Mbunge wa Mwibara kwa sababu Mwibara ndiyo inayoongoza kwa umaskini. Haya ni masikitiko makubwa, umaskini uliokithiri, hakuna anayependa kuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, napenda niishauri Serikali juu ya mifumo inayonyonya mazao ya samaki, ni kwa nini mnunuzi wa samaki ndiye anapanga bei, ndiye anayemiliki mzani, ndiye anapima samaki na anayetamka kilo zilizopatikana? Kadhalika, kwenye pamba. Mifumo hii, Serikali ipige marufuku kwa kutunga sheria ya kuwatetea wavuvi pamoja na wakulima ili wakulima wamiliki mzani, wapange bei na wawe na kauli juu ya pamba yao na wavuvi wawe na kauli juu ya samaki zao. Hakuna Mtanzania leo ataenda kwenye duka la mtu pale kununua sukari akiwa na mzani wake, yeye ndio akapange bei ya sukari, yeye ndiye akatamke bei, muuza duka atampigia kelele za mwizi, mwizi, mwizi na atakimbia.

Mheshimiwa Spika, kuna sheria zinazowakandamiza wakulima pamoja na wavuvi. Kuna sheria ya mazingira ilipitishwa kwa nia njema, kutoharibu mazalia ya samaki. Wakaharamisha makokoro na nyavu zingine zenye matundu madogo lakini sheria hii inawabana wavuvi ambao ni maskini ambao hawana uvuvi mbadala kwa sababu hawakupewa fedha na Serikali kwa ajili ya uvuvi wa maji marefu ili waweze kuwa na zana za kisasa, wamebaki na makokoro na kufukuzwa na Polisi, makokoro yanachomwa moto wakati sheria inasema anayetengeneza, anayesambaza na anayevulia, wote wanatenda kosa. Sijawahi kuona Polisi wakichoma kiwanda chochote katika nchi hii kwa sababu ya kuzalisha zana haramu. Utekelezaji wa sheria ni wa kibaguzi.

Mheshimiwa Spika, wapo watu leo hii wanaishi Ziwa Victoria na kilimo ndio msingi mkubwa wa Ziwa Victoria lakini hawaruhusiwi kulima ndani ya mita 60 kwa sababu ya Sheria ya Mazingira. Lakini leo hii ukienda kwa wananchi wengine mjini utakuta mahoteli yameota, yameelea juu ya uso wa maji, hizi ni sheria za ubaguzi. Naishauri Serikali, sheria zote zinazokandamiza, mianya yote ambayo ni ya mifumo ya kinyonyaji kwenye biashara, ipigwe marufuku.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ina nguvu za kutosha katika kupambana na matatizo na majanga. Umaskini ni janga sawa na maradhi, tumeshuhudia kunapokuwa na maradhi kama vile kipindupindu, wanaweka karantini kuzuia ugonjwa usienee. Tumeshuhudia kunapokuwa na maandamano ya wanafunzi, Serikali inatumia vyombo vyake kuyadhibiti maandamano hayo. Vyama vya Siasa vinapoandamana bila vibali, vinadhibitiwa. Sasa ni wakati, kama Serikali iliamua kuweka Kanda Maalum ya Kipolisi kwa maana ya kudhibiti ujambazi, kwa kweli umaskini uliokithiri wa Mwibara na Bunda ambao wanaongoza, sasa ni wakati wa Serikali kutenga Jimbo la Mwibara kama Kanda Maalum ya kupambana na umaskini. Tutakapokuwa tumefanya vizuri kwa kutenga Kanda Maalum kwa kupambana na umaskini, hiyo itakuwa *split over* au *pilot area*, tutakwenda kwenye Wilaya zingine ambazo zilifuatia kwa kuongoza umaskini na zenyewe zitengwe kama Kanda Maalum ya kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, haya mambo ya MKUKUTA, MKURABITA, hii si dozi nzuri kwa mgonjwa ambaye umaskini wake umekithiri. Ugonjwa ambao umekithiri lazima uongezewe na *drip*. Mwibara wanahitaji *drip* kwa maana ya mipango mingine madhubuti ikiwemo miradi mikubwa ya uvuvi, miradi mikubwa ya kilimo cha umwagiliaji pamoja na wananchi kukopeshwa fedha ili waweze kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema jambo hili, wapo watu wanakejeli Shule za Sekondari, wengine wanasema zifutwe, wanaangalia upande mmoja tu kwamba mtu akifaulu, apate kazi, aende *high school*, aende Chuo Kikuu, lakini kwenye upande wa jamii sasa hivi kuna wanaume ambao wanasema hawawezi kumwoa binti ambaye hajamaliza *Form Four*. Kwa hiyo, hata kule kumaliza *Form Four* kwa msichana, kuna mtengenezea soko la kuweza kuolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iendelee kuboresha maeneo haya ya shule kwa sababu matokeo mabaya ni kujikwa na kujikwaa si kuanguka ni kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawapenda wananchi wa Tanzania na wananchi wa Tanzania wanaipenda Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ninaamini kwa mtindo huo huo wa *reciprocal*, wananchi watandelea kuiweka madarakani Serikali ya CCM kwa sababu ya upendo wake.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapa ili dakika zangu zilizobaki jirani yangu Dr. Mgimwa aweze kuzitumia. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Isipokuwa moja tu, hakuna mwanamke ambaye anataka mwanaume ambaye hajasoma maana watakuwa hawaelewani Kiswahili. *(Kicheko)*

Sasa namwita Mheshimiwa Dr. Mgimwa atafuatiwa na Mheshimiwa Capt. John Komba.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyenzi Mungu, kwa kunipa nafasi hii ya kuchaguliwa kuwa Mbunge ili niweze kuwawakilisha wananchi wa Jimbo langu. *(Makofi)*

Pili, nachukua nafasi hii, kuwashukuru sana wale wananchi wa Jimbo la Kalenga, kwa kuniamini na kunipa nafasi hii niwawakilishe na naahidi kabisa siwezi kuwaangusha. *(Makofi)*

Tatu, namshukuru mke wangu Jane, kwa uvumilivu wake wakati wa kampeni na katika shughuli hizi za kisiasa nikiwa mbali naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakishukuru sana Chama hasa Rais kwa namna ya pekee alivyofanya kazi na anavyoendelea kufanya kazi kwa ajili ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kuchangia na nitachangia upande wa elimu na uchumi na nitagusa matatizo ya Jimbo langu yanayoendana na kipengele namba tisa ambacho Mheshimiwa Rais amegusia masuala haya.

Mheshimiwa Spika, upande wa elimu kama walivyozungumza wenzangu, kuna maeneo ambayo napenda kuyasisitiza. Ni kweli tumefika mahali ambapo sasa si vizuri kulaumu tunakotoka, tunatakiwa tuzungumzie tufanye nini. Tumepata matatizo na tunaambiwa sasa hivi *World* Bank imetoa msaada wa Dola milioni 1050 ikielekeza kwanza kutupa nafasi ya kufundisha Walimu zaidi, kujenga nyumba 1200 za Walimu, kukarabati nyumba 500 za Walimu, kujenga maabara na vilevile kusaidia *capitation grant* ya shilingi 25,000/- kwa kila mwanafunzi. Huu ni msaada mkubwa na nichangamoto kubwa lakini niseme bado hilo halitoshi.

Mheshimiwa Spika, bado tuna matatizo makubwa ya madawati katika shule zote za msingi na sekondari. Mimi mwenyewe nimefanya tathmini katika Jimbo langu, katika shule zote za msingi nimepata upungufu wa madawati 5,289 na katika shule za sekondari 15 katika Jimbo langu nimepata upungufu wa madawati 689. Hii yote ina maana kwamba bado tuna kazi kubwa ukiachilia mbali suala la kuongeza zaidi nyumba za Walimu. Ili *performance* ya shule iboreke, tunahitaji ku-*combine* msaada huo na kuelekeza nguvu za Serikali na wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa nini kifanyike? Pendekezo langu ni kwamba Serikali katika Bajeti inayokuja itenge kiwango kikubwa kuliko kiwango kilichokuwa katika Bajeti iliyopita ili kuelekeza katika upungufu huu. Mpaka sasa hivi, Serikali ilikuwa inatenga asilimia 18 katika Bajeti lakini napendekeza iwe zaidi katika kiwango cha pesa zitakazopatikana ili tuboreshe elimu maana hakuna mbadala wa elimu na kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa nimesema hilo la upande wa elimu, naomba sasa kuzungumzia upande wa uchumi. Ni sahihi kabisa kama Mheshimiwa Rais alivyozungumzia, akaweka kipaumbele namba mbili na namba tatu. Namba mbili akizungumza namna tunavyohitajika sasa kuboresha uchumi katika nchi hii. Sina sababu ya kurudia kutoa takwimu za hali halisi ya kudorora kwa uchumi lakini katika hali tuliyonayo, napendekeza yafuatayo katika kipengele namba mbili.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, kwa mtizamo wangu wa dhati kabisa, tunahitaji sasa kuboresha zile sera ambazo zina-*promote performance* ya uchumi. Sera zile lazima ziwe zinalenga *majority* kwa maana ya *percentage* kubwa ya watu walio vijijini. Sasa *contribution* hiyo italeta mkusanyiko, *combination* kubwa ya kuboresha uchumi katika nchi, Sera ambazo zinalenga kuhamasisha watu walio wengi waingie katika msukumo wa kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, la pili, tunahitaji kuboresha Sera za Uchumi ambazo zinalenga *percentage* ya *performance at around seven percent rate of economic growth.* Hii *single digit* katika umaskini tulionao Tanzania, haitoshelezi. Nchi tajiri ni sawasawa hata uki-*perform one or two percent* kwa sababu ni *developed country is okay* lakini kwetu haitoshelezi tunatakiwa tu-*perform at a level of two digits*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati wa tatu katika huo uchumi, tunatakiwa tuangalie zile Sera ambazo zinafanya uchumi ziwe *sustainable* kwa maana kwamba tukishakuwa na

sera zenye msukumo, kwanza watu wengi waingie katika *performance* ya uchumi na pili zile zinazolenga ku-*target* ku-*perform* katika *rate* ipi, tatu ni sera ambazo ziko *sustainable*, tusiwe na sera ambazo zinabadilika kila wakati, tutakosa *consistence* ya *investment*.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba nizungumzie kipengele namba tisa kama Mheshimiwa Rais alivyosema, ni suala la ku-*invest.* Sasa katika *critical resources* zitakazosaidia hii *performance* iwepo, tuwe na umeme, tuwe na *full exploitation* za *energy*. Katika Jimbo langu la Kalenga, kuna vijiji vikubwa ambavyo vinastahili kuwa na umeme. Tuna kijiji cha Magulilwa, Mugama, Kiponzero na kijiji cha Wasa. Vijiji vikubwa na vina shule kubwa, vina taasisi kubwa na vina watu wengi. Katika mwelekeo wa vipaumbele vya Rais, ni vizuri sana kutazama namna hii ili tuweze kueneza umeme katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunahitaji kuboresha barabara inayounganisha Kalenga na Hospitali Teule ya Ipamba. Barabara hiyo naomba ichukuliwe na Serikali Kuu kusudi kurahisisha usafiri wa wagonjwa wanaokwenda kupata huduma katika Hospitali ya Ipamba. Naomba sana suala hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Rais katika vipaumbele hivyo alivyoviweka mbele yetu na mwisho kabisa naunga mkono hoja ya hotuba ya Rais. *(Makofi)*

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, nami kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo kwa mara ya kwanza tangu nirudi humu kwa mara ya pili katika jumba hili, ingawa juzi gazeti moja limenitoa kwamba nawaombea wale wanaokataa amani hapa, nawaombea, wanasema sijui nasinzia, mimi nilikuwa naomba nimefumba macho, nakemea. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kukemea kwangu leo ndiyo maana nimeona hata Mwenyekiti wa CHADEMA ametoa maneno mazuri, hii inaonyesha kwamba maombi yangu yamekubalika ndani ya kemeo langu. Kwa hiyo, mambo haya yaendelee. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimshukuru mke wangu Salome, watoto wangu, wananchi wa Jimbo langu la Mbinga Magharibi ambao kila kukicha wananitegemea mimi tuvutane na wao katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu ambapo suala hilo Rais wa nchi amekubali na ametusaidia mwezi wa saba liwe Wilaya mpya ya Nyasa. Nawashukuru sana kwa kura zao nyingi, za upendo kwangu, kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa Madiwani wa Chama cha Mapinduzi. Mimi nawaambia wenzangu katika nchi hii, maana mimi nakaa mpakani mwa Malawi, Zambia na Msumbiji, tunapozungumzia amani, watu wa kule wanajua amani maana yake ni nini. Tuna amani kweli kweli maana ukienda Msumbiji unaona fujo, ukienda Malawi fujo, Zambia unaona fujo, lakini hapa tunakemea amani watu wanafikiri ni utani utani tu.

Mheshimiwa Spika, jana mtu anahimiza watu waandamane, nchi isitawalike, leo anazungumzia amani na Mwalimu Nyerere alisema hivi, huyo anayesema kitu kama

hicho unamwangalia usoni, unamwangalia huyu anachosema anaamini ndani ya roho yake? Wapo watu hawaamini ndani ya roho zao kwamba wanachokisema ndicho wanachokitenda. Lakini amani ikitoweka katika nchi hii atakayeumia si Chama cha Mapinduzi peke yake, CHADEMA, *CUF* sijui nani, wote mtindo mmoja. Tena afadhali sisi wa Chama cha Mapinduzi tumetawala muda mrefu tunajua pa kukimbilia, ninyi hamjui pa kukimbilia mtaumia kweli. Ni vizuri tuendelee na amani ili pengine kama Mungu atawasaidia mpate kutawala nchi hii, muendeleze amani ambayo Chama cha Mapinduzi imeileta. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, watu wengi wamezungumzia habari za Shule za Kata, wanafunzi wamefeli na nini. Jambo lolote zuri lina matokeo yake, mengine mazuri, mengine mabaya zaidi. Nakumbuka kwa watu wa umri wangu, mimi ni mmoja kati ya wale waliofanya mtihani mmoja wanafunzi wa Darasa la Saba na la Nane mwaka 1967, wa Darasa la Nane walifaulu sana, sisi wa Darasa la Saba karibu 99 tulifeli wote na mimi nilifeli. Lakini kwa sababu ndiyo maendeleo na mabadiliko yalivyo, tuka-*struggle* na mpaka leo mimi ni Mbunge hapa. Kwa hiyo, haya yaliyotokea mwaka jana ndiyo *struggle* ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1965, Mwenyekiti Mao wa China alileteww trekta na Wanasayansi wa Uchina. Wakamwambia, Mzee tumetengeneza trekta, njoo tuzindulie. Mwenyekiti akaenda kulizindua lile trekta wakijua kila kitu kiko sawa, walivyowasha lile trekta badala ya kwenda mbele likawa linarudi *reverse*. Wale vijana walifikiri watafungwa au watanyongwa, lakini Mao aliwaambia hapana huo ndiyo mwanzo mzuri, trekta la pili litakuwa zuri zaidi kuliko hili. Kwa hiyo, akawapa moyo endeleeni. Kwa hiyo, nafikiri hili lililofanywa na Chama cha Mapinduzi kila Kata kuwa na Sekondari, faida hii hamuwezi kuiona miaka miwili au mwaka mmoja, mtaiona miaka mitatu, minne mbele, ndiyo utaratibu wa maendeleo, hauwezi kuja tu kama mvua. Kwa hiyo, naomba wanaolaumu pia waangalie, hivi ni Upinzani tu au ni ukweli ndani ya roho zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, CCM tulichokifanya sisi pamoja na mimi, ni jambo jema na ndiyo maana juzi nikuwa naomba kabisa kabisa na Mungu akasema mmefanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwenye Jimbo langu la Mbinga Magharibi. Jimbo langu ni la wavuvi, zana zao ni duni sana na ukiangalia upande wa pili wananchi wa Malawi, nadhani kwa vile sisi tuna maji mengi, tuna maji ya Bahari, Maziwa, wenzetu wana maji moja maana yake wana maji ya Ziwa moja. Upande wa Ziwa hilo wamelitumia vizuri zaidi kuliko upande wetu sisi huku, wanatucheka sana lakini sasa hatukufanya vibaya na mimi siilaumu Serikali ya CCM, maendeleo haya lazima uweke akiba hata Benki lazima uweke akiba. Sasa moja ya akiba tuliyoweka Wana-CCM ni kusubiri kuwekeza maeneo ya Ziwa Nyasa na mengine ya Kusini, sasa ndiyo wakati wa kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, namwomba Waziri wa Uvuvi na Samaki, Waziri wa Kitoweo, unaposema Ukanda wa Ziwa, watu wanafikiri ni Ziwa Victoria tu, Ukinda wa Ziwa ni pamoja na Ziwa Nyasa, ni pamoja na Ziwa Tanganyika,

ni pamoja na Ziwa Rukwa, ni pamoja na Ziwa Eyasi, Natron na mengine, tukirudi kule ni Bahari ya Hindi. Kwa hiyo, naomba sana sasa tuwekeze kwenye Maziwa haya. Ziwa Victoria tumewekeza kiasi cha kutosha na samaki wanakwisha, Ziwa Nyasa bado. Naomba sana tuwekeze katika Ziwa lile kama wenzetu wa Malawi walivyowekeza. Wenzetu wana viwanda vya samaki, sisi hatuna. Naomba sana turudi kule, tukasaidie wananchi wa Ziwa lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia liko jambo la nyavu za kuvulia. Wananchi nyavu zao zinakamatwa lazima ziwe na matundu makubwa. Sasa dagaa hata akikaa miaka mia moja, atakuwa ni yule yule tu wa miaka miwili iliyopita. Sasa tundu kubwa itamvuaje dagaa huyo? Watu wanakamata nyavu za dagaa kisa matundu makubwa. Dagaa ni samaki asiyekua, akae miaka 20, miaka 10 hakui lazima avuliwe na nyavu za tundu ndogo. Kwa hiyo, naomba ninyi mnaopata nafasi ya kuwa Mawaziri, hebu kwanza jifunzeni utaratibu wa samaki sio kutunga Sera tu lakini angalia utaratibu wa samaki, samaki gani anavuliwa na nyavu gani, toa sera hiyo. Sasa utakuta dagaa hatuvui, wenzetu wa Malawi wanavua dagaa vizuri, sisi watu wetu wanakamatwa, naomba sana tusaidie jambo hili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, michezo na utamaduni. Ni kweli Serikali imerudisha michezo shuleni lakini inakuwa kama tunafanya maigizo. Unarudisha michezo shuleni lakini huwi *serious*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Ndiyo mwisho? Siku nyingine tena. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kutoa mchango rasmi, nichukue fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuingiza kwenye historia ya Taifa hili kwamba safari yangu kufika hapa ilikuwa ndefu kidogo, ilianza mwaka 2005 lakini kwa sababu ya udhaifu wa mifumo yetu ya Kikatiba na ya Kisheria ya usimamizi wa haki, safari hii imekuwa ya miaka mitano na nimefika leo hapa kwa nguvu ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii, kuwashukuru sana wazee wa Jimbo la Ubungo bila kujali tofauti za Vyama, Jimbo lenye wapigakura 450,000 ambao waliona wanitume mtoto wao nije kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru akina mama wa Jimbo la Ubungo, wanawake ambao katika kipindi kigumu sana cha kampeni walikuwa wakiniombea kwa Mwenyezi Mungu na leo nimefika hapa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi, niwashukuru vijana wenzangu wa Tanzania nzima na Jimbo la Ubungo. Vijana wa mtaani, vijana wafanyakazi na vijana wa Vyuo

Vikuu ambao walikuwa tayari kukesha kwa siku tatu kulinda ushindi mpaka tukatangazwa. Ahadi yangu kwao ni kuwatumikia katika kipindi cha miaka mitano cha utumishi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunavyozungumza ni wakati pekee sana kwenye historia ya Taifa letu. Tunazungumza ikiwa ni miezi michache kuelekea kuadhimisha miaka 50 toka Taifa letu lipate uhuru. Lakini tunazungumza wakati ambapo Taifa linakabiliwa na mgawo wa umeme. Miaka 50 baada ya uhuru, Taifa likikabiliwa na matokeo mabovu ya wanafunzi. Miaka 50 baada ya uhuru, Taifa linakabiliwa na kupanda kwa hali ya juu kwa gharama za maisha ambako kunasababisha tishio la migomo mbalimbali. Migomo ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu tunazungumza leo wakiwa wamerudishwa nyumbani kwenye Vyuo mbalimbali, migomo ya wafanyakazi na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya yangeweza kutupa sababu ya kukata tama lakini mimi ninayo sababu ya kuwa na matumaini. Nina matumaini kwa sababu tupo kwenye chombo hiki na natarajia kwamba hatutaendekeza itikadi na maslahi ya Vyama badala yake tutasimamia maslahi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na upungufu wake, Ibara ya 63 inasema kwamba hiki ndiyo chombo kikuu kwa niaba ya wananchi waliotutuma, chenye wajibu wa kuishauri na kuisimamia Serikali. Kwa hiyo, naomba nieleweke tu hapa, tunapokosoa, tunapounga mkono, ni sehemu ya kuishauri na kuisimamia Serikali. Natarajia kwamba, Wabunge kwa umoja wetu, hatutajigeuza kuwa na jukumu la Serikali, badala yake tutaendelea kuwa na jukumu la kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niishauri Serikali, kwa kweli ili tuweze kufika Desemba 9, tukiadhimisha uhuru tukiwa na sababu ya kuadhimisha uhuru kwa maana ya kusherehekea, lazima Serikali iamue kwa dhati, Bunge lijalo la mwezi Aprili, lilete mapendekezo ya msingi wakati tunatengeneza vipaumbele vya bajeti ya safari hii. Ni mambo gani ya haraka ambayo kama Taifa tunaweza tukafanya kwa umoja wetu, kwa makubaliano yetu ili ikifika Desemba, pamoja na yote yaliyojitokeza miaka 50 iliyopita, tuseme walau hapa tuna sababu ya kujivunia na nitasema machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeisoma hotuba ya Rais na nitaichangia kwa uchache wa maneno. Rais amezungumzia vipaumbele mbalimbali, ukurasa wa 12 na 13, amegusia suala la umoja wa kitaifa na hili ni jambo ambalo hatupishani kwa sababu hata Ngao ya Taifa letu inasema Uhuru na Umoja. Lakini kuna jambo moja napenda nitoe tahadhari, suala la udini. Hotuba ya Rais ukurasa 12 inasema kwamba Tanzania ni moja, watu hawabaguani, kwa hiyo, Tanzania hakuna mgawanyiko hata wa kidini lakini ukurasa wa 13 anasema kuna mpasuko wa kidini. Mimi naomba vyombo vya Ulinzi na Usalama, vikamshauri Rais kwamba kadri viongozi wa juu tutakavyoendelea kupiga kelele nyingi sana za udini, ndivyo kadri tunavyopandikiza mbegu ya udini kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuja kwenye kikao hiki, nimezunguka vijiweni, nimekaa vijiweni, Watanzania ni wamoja kweli kweli, viongozi tusije tukawa ndiyo tunasababisha mgawanyiko miongoni mwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichangie eneo lingine, Rais amezungumzia kuhusu kukuza uchumi na ukurasa wa 15 amezungumzia suala la kupanda kwa bei ya mafuta kwenye Soko la Dunia na chakula kama sehemu ya matatizo ya kimaisha ambayo yalitokea mwaka 2007. Mimi naomba tu Serikali ituletee taarifa Bungeni kuhusu hali halisi. Takwimu hapa kwa mujibu wa hotuba ya Rais, inaonyesha kwamba mfumko wa bei ni asilimia 4.2. Wakati Rais anazungumza, bei ya sukari kilo moja ilikuwa Sh.1,200/=, leo tunazungumza kilo moja imepanda mpaka kufikia Sh.2,000/=. Gharama za maisha zinapanda kwa Ari, Kasi na Nguvu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali ikatuletea pendekezo la namna gani Tanzania inakabiliana na tatizo hili la kupanda kwa gharama za maisha. Tunaweza kuwalaumu wanafunzi kwa nini wanagoma kwamba wanalipwa Sh.5,000/= lakini wanalalamika, bei ya chakula inapanda! Sasa kuwalaumu wafanyakazi kwa nini wanalalamika, wanataka kuandamana, bei ya umeme imepanda, kama hatutadhibiti kupanda kwa bei, tunatengeneza mgogoro kwenye Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais amezungumzia kuhusu kufufua viwanda, niseme tu kwamba kazi hii ni nzito, inahitaji vilevile kama Taifa tuzungumze, hivyo viwanda vilivyokufa vilikufaje? Mimi pale Jimboni kwangu Ubungo kuna Kiwanda cha Urafiki ambacho mwanzoni Tanzania ilikuwa inakimiliki, sasa hivi ina hisa 49 peke yake. Kiwanda kinaelekea kufa na sasa hivi ninavyozungumza, wafanyakazi wamepewa likizo, tena wamepewa likizo kwa asilimia 50 tu ya malipo. Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili la Urafiki nitaliletea maelezo kwa sababu ni suala la kina sana, kuuzwa kwa mitambo na kadhalika nitawaletea maelezo.

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye eneo la msingi ambalo ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Ubungo, nayo ni maji. Mheshimiwa Rais, amezungumza kuhusu ongezeko la mgawo wa fedha za bajeti kwenye maji na amezungumza kuhusu Miradi ya Benki ya Dunia lakini mimi nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Maji na nimwahidi tu kwamba tulifanya Kongamano la Maji, tarehe 31 Ubungo, tukayajua matatizo na nitaleta taarifa kamili kwake kama ambavyo tumekubaliana na nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano, tunahitaji, pamoja na mipango ya muda mrefu ya ujenzi wa mabwawa ya Kidunda, miradi ya Kimbiji, Mpera na kadhalika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi hii. Kwanza, nipende kutoa shukrani za dhati kwa mke wangu Willelmina na watoto wetu, kwa wapendwa wana-Jimbo la Karatu, wana-CHADEMA pamoja na wana-

CCM, maana walinipa kura za kishindo na wanajua mimi ni Mbunge wao bila kujali itikadi ya Vyama, dini na rangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu tulipoanza Bunge hili na kwa kuwa mimi ni mara yangu ya kwanza katika mjengo huu, niliangalia mwenendo wa hoja katika mjengo huu, nikajiuliza, Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kimsingi wakiwa katika mjengo huu, hawana Chama, hawana itikadi maana wapo kwa ajili ya kuwawakilisha Watanzania wote na Watanzania wote wanataka kusikia kutoka katika Bunge hili kwamba wanapata ahueni ya maisha yao. Mimi ni muumini wa falsafa inayosema "tukubali kutokukubaliana na tubaki ndugu" *(let's agree to disagree and remain friends). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ambazo zimejengwa hapa ukiangalia kwa mapana yake kimsingi hazina tija kwa maendeleo ya Mtanzania anayetaka aondokane na unyonge wa uchumi wake. Ni wazi hakuna atakayepinga kwamba demokrasia Tanzania bado ni changa na labda ndiyo maana kumekuwa na vijembe vingi vingi ndani ya Bunge hili visivyo na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mila na desturi zetu Waafrika, baba akikaa na familia yake, baba akachafua hali ya hewa, mtoto hukemewa, ashakum si matusi Mheshimiwa Spika. Kama ndivyo, tumekubali kuwa na Vyama Vingi, Wapinzani kama *a watchdog* kwa Chama Tawala, nafikiri ni muda muafaka kwa Chama Tawala kujipanga vizuri. Sisi usiku tuna walinzi ambao ni mbwa na akibweka, mtu yeyote mwenye kujali hataendelea kulala, atataka angalie kulikoni huko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Rais, inatoa taswira ya Tanzania, hilo sina neno nalo lakini kilichobaki ni dhamira, ni kwa jinsi gani taswira hiyo iweze kufikiwa. Hapa niseme kwa Waheshimiwa Mawaziri, watendaji wa Serikali, kwanza, Waziri ametokana na nafasi ya Ubunge, kwa hiyo jambo la msingi ni Mbunge, mwakilishi wa mwananchi, halafu ndipo ukapewa ngazi nyingine ya kuwa Waziri. Dhamira nzuri ndani ya Serikali itatufikisha katika taswira ambayo kwayo Rais ameweka pia katika hotuba yake. Ni mambo mawili naomba kwa Serikali, *commitment and faithfulness* kwa watendaji wetu. Naomba hili tulizingatie watendaji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amezungumzia sehemu ya mwisho katika hotuba yake kuhusu utawala bora, ametaja mambo ya uwajibikaji, mambo ya ubadhirifu na mengine mengi huko ndani maana yake *we are not committed, we are not faithful*. Tumepewa dhamana ya kuongoza nchi hii, Bunge kama mhimili mmoja maarufu katika mihimili mitatu maana tunawakilisha wananchi, labda ujiulize Waziri mtendaji maana wewe ni Mbunge halafu ni Waziri unawakilisha wananchi, labda niseme baada ya kuwa Waziri ile hali ya Ubunge, ya kuwa mwakilishi wa wananchi, umeiacha wapi?

Mheshimiwa Spika, nimeangalia hotuba ya Mheshimiwa Rais, ukiangalia afya, elimu, ni mambo ya msingi ambayo watu wameyazungumza sana na mimi nishukuru Serikali ya CCM kwa sababu walikuwa wasikivu na walichukua toka Ilani ya

CHADEMA, Zahanati kila kijiji na hili tulilifanya Karatu na nashukuru. Pokeeni mambo mazuri kutoka Ilani ya Chama cha CHADEMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tusiendelee ku-*lament*, ku-*lament*, ku-*lament*, tufanye kazi. Hatuna Waganga, hatuna Wauguzi, Zahanati tunazo kila kijiji na kwa Jimbo langu hilo tumelitekeleza. Tunaomba Serikali iweke mpango mkakati kuzalisha Wauguzi, Waganga, Walimu na Walimu watunzwe. Wale wafugaji wanafahamu, ukitaka kupata maziwa ni lazima yule ng'ombe umpe *cotton cake* ili upate maziwa. Hawa walimu ndio wanaozalisha watalaam, Serikali iwajali, iwathamini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mheshimiwa Rais amezungumza juu ya utawala bora, utawala wa sheria na amesema na ndivyo ilivyo, Mahakama ni moja ya vyombo vinavyotoa haki. Naomba Waziri anayehusika, katika Jimbo langu la Karatu tayari tumejenga Mahakama ya Wilaya lakini Mahakama ile bado haifanyi kazi. Wananchi wangu Karatu wanahangaika kufuata Mahakama ya Wilaya mpaka Monduli na hii imekuwa shida kubwa na kusababisha wale wanyonge kutopata haki yao. Naomba Waziri mhusika alifuatilie suala hilo ili wananchi wa Karatu wapate haki yao pale pale ndani ya Wilaya ya Karatu kwa *level* ya Jimbo , ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kujadili hotuba hii ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati wa kufungua Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka jana, 2010. Nampongeza pia Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri na yenye mikakati mizuri na yenye matumaini makubwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Liwale, kwa kunipa dhamana kubwa, wanawake tunaweza, naamini kabisa nitaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitautoa kwenye elimu na muda ukitosha nitachangia kwenye suala la usalama wa raia na muda ukitosha zaidi nitachangia kwenye suala la barabara.

Mheshimiwa Spika, wachangiaji wengi wamechangia kuhusu elimu na hasa uhaba wa Walimu, upatikanaji wa vifaa vya maabara na ukosefu wa maabara zenyewe na ukosefu wa vitabu vya kiada na ziada. Mchango wangu hasa utakuwa kwenye ukosefu wa mabweni ya kutosha, umeme wa jua na kuboresha maslahi ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, shule zetu nyingi za Sekondari za Kata, zina matatizo ya mabweni na vyanzo vizuri na vya kuaminika vya umeme. Mwanafunzi anapopangiwa Shule ya Sekondari ambayo haina mabweni ya kutosha, analazimika kupanga uraiani pamoja na raia wengine. Wakati mwingine mwanafunzi wa kike analazimika kupanga kwenye nyumba moja pamoja na wanafunzi wa kiume, hali hiyo husababisha nidhamu ya wanafunzi hawa kushuka na badala ya kusoma wanafunzi hawa wanaelekezwa kwenye kufanya mambo mengine ambayo yanawaletea pia kufeli kwenye mitihani yao ya Kidato cha Nne.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba ili kuboresha mazingira ya kuwafanya wanafunzi hawa waweze kusoma vizuri na ili wawe na nidhamu nzuri, Serikali ijenge mabweni ya kutosha kwa wasichana na wavulana ili waache kupanga uraiani vilevile shule hizi zipatiwe umeme wa jua *(solar power)*. Shule hizi za Sekondari za Kata zikipatiwa umeme wa jua maana yake wanafunzi watakuwa na uwezo wa kusoma hata kipindi cha usiku na hivyo kuboresha elimu zitolewazo katika shule zetu na kwa hiyo itaongeza ufaulu wanapomaliza mitihani yao ya Kidato cha Nne.

Mheshimiwa Spika, shule zetu nyingi za Kata zipo vijijini na shule nyingi ziko mbali na Makao Makuu ya Wilaya, Walimu hawa wanakaa kwenye mazingira magumu sana, wote tunafahamu kwenye vijiji tunavyotoka. Naishauri Serikali ili waweze kufundisha vizuri tusikazanie tu kwamba vifaa vya maabara, vitabu, vilevile tufikirie jinsi ya kuwaboreshea maslahi hao Walimu ili pamoja na vifaa vya maabara, vitabu, mabweni na wao waweze kupata motisha wa kuweza kuwafundisha wanafunzi hawa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais kwa kuweza kuona kwamba Maafisa wa Polisi na Polisi wa kawaida wanahitaji kuboreshewa maslahi, mazingira yao ya kufanyia kazi na makazi yao kwa ujumla. Hali ya vituo vya Polisi na makazi yao huko Mikoani na hasa katika Wilaya zetu, ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Liwale imekuwa Wilaya tangu mwaka 1975 lakini haijawahi kujengewa Kituo cha Polisi cha Wilaya. Ukiangalia hata nyumba wanazoishi Askari hawa wa Polisi pamoja na Maafisa wa Polisi, zinasikitisha sana kiasi kwamba nafikiri haiwezi kuwashawishi kufanya kazi inavyotakiwa. Namwomba Waziri mwenye dhamana aweze kutembelea Wilaya hii kwa sababu Wilaya haina Kituo cha Polisi na badala yake Kituo cha Polisi kipo kwenye nyumba kuukuu ambayo haifai na si salama, hata kama kuna wakosaji na wamefungiwa pale, inakuwa ni hatari. Naomba sana Waziri mwenye dhamana aweze kutembelea Wilaya hii ya Liwale na kuona hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuongelea kuhusu barabara. Wilaya yangu barabara ya kutoka Nangurukuru kwenda Liwale haipitiki na magari zaidi ya saba yamekwama. Naomba Waziri mwenye dhamana anisaidie sana kuendelea kuangalia barabara hizi za Liwale. Pamoja na barabara zilizopo bado namwomba Mheshimiwa Magufuli aharakishe ujenzi wa barabara hii mpya ambayo Rais ameipendekeza ya kutoka Liwale - Kingupila - Utete. Kwa kufanya hivi, itaisaidia Wilaya hii kuwa inapitika wakati wote badala ya sasa kutegemea barabara moja ambayo hivi sasa ninavyoongea magari kumi yapo barabarani yameshindwa kufika, watu wamekaa hawana chakula hawana chochote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii adimu ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ya hotuba ya Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama rasmi katika Bunge hili na kuchangia, naomba nitoe shukrani za dhati kwa wanawake wa Wilaya ya Kinondoni, Jijini Dar es Salaam kwa kuweza kunichagua na baadaye Chama Taifa kikaweza kuniteua ili kushika nafasi hii kwa mara ya pili, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee nikupongeze sana kwa nafasi nyeti ambayo umeipata, kwa kweli sisi akina mama tunajivunia sana na tunakuahidi kwamba tutakuunga mkono popote pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesoma hotuba ya Rais na nimeirudia sana, kwa kweli ni hotuba nzuri sana kwa kusoma, imeandikwa vizuri sana lakini tatizo naloliona ni utekelezaji wake. Nina hakika kabisa kama hotuba hii itatekelezwa, Tanzania haitakuwa tena katika kundi la nchi maskini bali itakuwa ni nchi iliyoendelea. Nasema hili kwa sababu ya matatizo ambayo yamejitokeza kwa hotuba iliyopita ya mwaka 2005 tulikuwa na vipaumbele kumi, siamini kama vipaumbele kumi vyote vilitekelezwa, kwa hiyo ninaamini vile vile kwa hali halisi ya Tanzania ya kifedha kwa sababu ukiangalia vipaumbele hivi kumi na tatu vyote vinahitaji fedha nyingi sana, hili naona ni tatizo kubwa sana. Nilikuwa nategemea kwamba tungekuwa na vipaumbele vichache zaidi, tungeweza kuwa na matumaini makubwa kwamba vipaumbele hivyo vingetekelezeka, lakini kwa hali halisi inavyoelekea itakuwa vigumu sana ndani ya miaka mitano kuweza kuvitekeleza kwa kina vipaumbele vilivyowekwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kumekuwa na dhana kwamba Wapinzani hatupendi maendeleo, siyo kweli, kazi yetu wote tuliokuja hapa Bungeni, Vyama ni madirisha tu au milango ya kutuingiza hapa Bungeni, lakini tunapoingia humu Bungeni kazi yetu ni moja ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maendeleo. Siamini kama kuna Mbunge hata mmoja wakati alipokuwa anaomba kura aliwaambia wananchi wake kwamba mimi sitawaletea maendeleo, siliamini hili. Tunapokuwa hapa Bungeni nia yetu wote ni moja ya kuwaletea wananchi wetu maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikijiuliza, maendeleo ni nini, tumeona mifano mbalimbali, je maendeleo ni majengo tunayoyaona Dar es Salaam, maendeleo ni magari yaliyopo kwa wingi Dar es Salaam na Mikoa mingine au maendeleo ni bidhaa zinazoonekana katika maduka mengi nchini zinazotoka China na sehemu zingine mbalimbali? Nadhani maendeleo tunaangalia pato la Mtanzania na vilevile tunaangalia huduma za jamii ambazo Mtanzania huyu anazipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba tunaingia katika mwaka wa hamsini wa uhuru lakini bado umaskini wa Mtanzania upo pale pale. Ukiangalia katika takwimu za *IMF International Monetary Fund* mwaka 2010 inaonesha dhahiri kwamba Tanzania ni nchi ya 156 kati ya nchi 182 kwa pato dogo la Taifa. Inaonesha wazi kwamba wastani wa Mtanzania pato lake ni dola nne kwa siku, wakati nchi inayoongoza ni Quartar ambayo pato lake ni dola za Kimarekani 242 sawa na shilingi karibu laki tatu. Ukiangalia kwa kweli unaona bado tuna tatizo kubwa na ndiyo sababu tunaposema kwamba tunahitaji tukae kwa pamoja tushughulikie matatizo ya

wananchi, tuangalie mustakabali wa Taifa letu linakwenda wapi, tusionekane kwamba sisi tunapinga, Upinzani maana yake siyo kupinga, pale ambapo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya vizuri tutawapongeza lakini wasitulazimishe kuwapongeza pale ambapo hawajafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Bunge la Tisa tuliongea sana na nakumbuka wakati huo kama siyo Dokta Slaa ni Kiongozi wa Upinzani, tulizungumzia sana suala zima la ukubwa wa Baraza la Mawaziri na tukasema hizi ni gharama kubwa sana. Naamini Serikali ya CCM mara zote mmekuwa mnasema kwamba ni wasikivu na mimi ninaamini, lakini ukiangalia gharama za Baraza la Mawaziri ni kubwa, nilitegemea kabisa kwamba Baraza hilo lingepungua lakini limeongezeka. Bunge lililopita walikuwa Mawaziri 48 sasa hivi wamekuwa 50, sina tatizo nalo. Tukiangalia nchi tajiri ambazo tunaenda kuomba misaada, Mabaraza yao ya Mawaziri ni madogo kwa sababu wanajua gharama. Tukichukulia mfano nchi kama Marekani, Baraza lao la Mawaziri ambao wanaitwa *Secretaries*, wapo 15 tu, nchi yenye watu milioni 318. Uingereza ambayo imetutawala na ni Taifa tajiri, wana Mawaziri 21 tu, kwa nini Tanzania tunakuwa na Baraza kubwa ambalo gharama zake za kuliendesha zinakuwa kubwa mno? Hakuna uwiano kati ya Baraza letu na wananchi tunaowaongoza. Nadhani kuna haja ya Serikali kuangalia ni jinsi gani wanaweza kupunguza gharama ambazo siyo za lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia, ni suala zima la *capacity charges* ambazo Tanzania tumekuwa tunalipa *IPTL* pamoja na *Dowans.* Ukichukua gharama hizo kwa mwaka kama kwa siku ni shilingi milioni mia nne hamsini na mbili, kwa mwaka ni bilioni mia moja sitini na tano. Fedha hizi zingeweza kujenga nyumba za Walimu laki moja na sitini na tano kwa gharama ya nyumba ya Mwalimu ya shilingi milioni kumi. Kwa hiyo, nadhani kuna haja kabisa ya Serikali kuhakikisha kwamba wanaweka mipango, kwa sababu kupanga ni kuchagua, tuangalie kama nchi zingine hazilipi *capacity charges* kwa nini sisi tulipe? Mimi nadhani mambo hayo ni lazima Serikali iangalie.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye kipaumbele cha tano kuhusu suala zima la hali halisi ya kijiografia ya nchi yetu. Ni wazi kwamba Mwenyezi Mungu ametupendelea sana, nchi yetu ni nchi ambayo ina bandari nzuri lakini nchi yetu pia imezungukwa na *land locked countries*, nchi ambazo hazina kabisa bandari, lakini tumeshindwa kuikuza au kuipanua bandari ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam inaweza ku-*handle* tani milioni saba tu kwa mwaka wakati nchi kama Singapore, nchi ambayo haina uchumi wowote zaidi ya bandari, inaweza ku-*handle* tani bilioni moja na laki tano. Nchi yetu jirani ya Kenya tu imeanza kupanua bandari yao ya Mombasa lakini sisi tumeshindwa jambo ambalo mimi naamini kabisa kama tungeweza kupanua bandari ya Dar es Salaam kwa kweli uchumi wetu ungepaa. Kwa hiyo, nategemea Wizara husika itahakikisha kwamba bandari ya Dar es Salaam inapanuliwa pamoja na zile bandari zingine za Mtwara na Tanga.

Mheshimiwa Spika, niendelee na suala zima la elimu. Ni wazi kwamba hakuna nchi iliyoendelea hapa duniani bila elimu na ndiyo sababu hata Waziri Mkuu wa Malyasia alipoulizwa kipaumbele chake cha kwanza ni nini, alisema ni elimu, cha pili

elimu na cha tatu ni elimu. Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba miaka hamsini ya uhuru bado elimu yetu inazidi kudorora, inatia aibu sana lakini tunajiuliza ni kwa nini? Mimi nailaumu sana Serikali kwa sababu unaona kabisa matatizo yote haya yanatokana na Serikali. Serikali mwaka 2008 ilifuta mtihani wa Darasa na Nne, na nataka niwaambie Wabunge wenzangu kwamba wale ambao waliondolewa mtihani wa Darasa la Nne ndiyo wanaoenda kufanya mtihani wa Darasa la Saba mwaka huu, kwa hiyo, tutegemee matokeo mabaya. Shule zinazofanya vizuri, wanautaratibu wa kuwa na mitihani kila mwaka, wale wanaofanya vibaya wanarudishwa lakini Serikali yetu imeshindwa kulifanya hilo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, napenda kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia kurudi tena na pia nawashukuru wapigakura wote wanawake wa Mkoa wa Pwani pamoja na wananchi kwa ujumla. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wale waliokuwa kwenye Kamati yangu ambao wamenipigia kura kuwa Makamu Mwenyekiti, safari hii Wabunge wameonesha ari ya kuweka uwiano katika Kamati kwa kuweka wanawake na wanaume. Napenda pia nikupongeze wewe pamoja na Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nimepata nafasi hii ya kuchangia hoja ya Rais, hotuba yake ilikuwa hotuba ambayo imetupa nafasi sisi kwenda kuifanyia kazi. Kabla sijachangia huko, napenda kuipongeza Serikali iliyopita ya 2005/2010, kwa kazi nzuri iliyofanya ya kutekeleza Ilani yake. Ilani ile imetekelezwa na Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi na wale ambao hawakuwa kwenye Chama cha Mapinduzi ndiyo maana leo tunajivunia na tuko ndani ya ukumbi huu.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mkoa wetu, ahadi za Rais zilikamilika, tumepata barabara za kutosha, vituo vya afya, zahanati, shule tumejenga lakini bado tuna tatizo ambalo ni muhimu tulizingatie kwetu sisi sote. Tumejenga shule za sekondari kwa kila Kata, hili ni tatizo la Kitaifa tunahitaji Walimu wa kutosha, tunahitaji maabara, tunahitaji maktaba kwa ajili ya watoto wetu waweze kusoma wafaulu. Huko nyuma haya hayakuwepo, hizi ni jitihada zilizotokana na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, sisi Waswahili wa Pwani tuna msemo unaosema: ‘mnyonge mnyongeni haki yake mpeni’, leo tumeona na wenzetu ni mashahidi watoto wetu wanasoma. Ombi langu mabweni tunayojenga, tunaomba Serikali itusaidie kuongeza kwenye bajeti. Tunafikiria sana watoto wa kike lakini pia kuna haja ya kuangalia na wale watoto wa kiume pia, tusije tukawa na kundi moja, kundi lingine tukaliacha peke yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niingine kwenye hotuba ya Rais. Hotuba ile ilikuwa na vipengele kumi na tatu na vipengele hivyo vyote vinazungumzia

suala la kuimarisha uchumi, suala la kuleta maendeleo katika nchi yetu, suala la kuleta mustakabali wa amani, suala la kuleta uwiano katika uongozi. Mimi nataka nijikite kwenye uchumi, uchumi wa nchi hii hauwezi kwenda kama hatuna miundombinu iliyokamilika, tunahitaji kuwa na barabara nzuri. Wote ni mashahidi kwenye Kata zetu, kwenye Wilaya zetu na Mikoa yetu, tunahitaji kuwa na maji ya kutosha. Bajeti za Halmashauri, Serikali imepeleka hela za kutosha lakini tuangalie kwenye maeneo, hasa ukiangalia Mkoa wa Pwani kuna baadhi ya maeneo hata ukitafuta maji kwenye ardhi uende mita mia moja bado huwezi kupata maji safi na salama. Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuweka utaratibu wa uvunaji wa maji ya mvua. Tusitegemee kila siku maji ya kutoka kwenye mito, mabwawa na mabomba, tuangalie uwezekano wa uvunaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika kila aliyesimama hapa katika kuchangia, baadhi yao wamegusia suala la tatizo la umeme. Serikali hii uchumi wake utakua kwa pesa za Serikali au kwa wafanyabiashara ambao wana uwezo, iwe taasisi, iwe mashirika ya umma au watu binafsi. Kulikuwa na swali leo hapa asubuhi limeulizwa kuhusu umeme unaotaka kuwekezwa na Shirika la *NSSF*, majibu ya Waziri yanatakiwa yafanyiwe kazi kwa kina. Kama tupo *serious*, tunataka nchi hii tuondokane na suala la uhaba wa umeme, naomba uwezekano wa Shirika hilo la *NSSF* au Mashirika yote ya Hifadhi ya Jamii yapewe kazi ya kuleta umeme kwa nchi hii. Sote ni mashahidi, miaka mitatu, nenda Chimwaga, utaona mabadiliko, wasiwasi unatokana na nini? Haya mashirika yana fedha na hizi fedha ndizo zilizoweza kuleta mabadiliko, kule tumeona Chuo Kikuu kile ambacho kimetuletea sifa kwa nchi yetu. Imemjengea sifa Rais wetu, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Chama cha Mapinduzi, Wabunge, Madiwani na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, *Consolidated Holdings* wameshafanya uchambuzi yakinifu, wameona hawa watu wa *NSSF* uwezo wanao, wameona wanaweza wakatuletea umeme *megawatt* 200 tu, tunaleta utata wa nini? Serikali ifanye kazi za Serikali, wafanyabiashara wafanye biashara tuweze kuleta maendeleo katika nchi yetu. Naomba ikibidi Waziri Mkuu aingilie, aangalie tatizo liko wapi, Nishati na Madini, tatizo liko Hazina, tatizo liko wapi ili tuweze kupata huo umeme kadri inavyowezekana ili tuondokane na adha ya umeme?

Mheshimiwa Spika, natumia taaluma yangu ya Uhandishi wa Habari, nitakuwa *very brief*, nataka sasa niende kipengele cha mwisho. Neno Tanzania lisingepatikana kama kusingekuwa na Muungano. Muungano huu wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar umetuletea sifa Watanzania. Nchi za Afrika hakuna ambayo tayari inaendeleza Muungano. Senegal walijaribu pamoja na Gambia wameshindwa, Gambia iko katikati ya *Senegal* lakini wameshindwa. Sisi mpaka leo Muungano wetu tunauenzi na umetuletea maendeleo mengi sana. Maendeleo tuliyoyapata kutokana na Muungano huu ni kwamba tumeweza kupanuka kibiashara, Watanzania tunatoka Bara tunakwenda Zanzibar, huulizwi *visa* wala *passport*. Tumejenga udugu, watu wameoana, wa Bara wameoa wa Zanzibar, Wazanzibar wameoa wa Bara, ushahidi upo. Wafanyabiashara wapo wanaotoka Tanzania Bara kwenda kufanya biashara Zanzibar, leo wako Wazanzibar wanaokwenda mpaka Sumbawanga, wako Kigoma, wako Mwanza…

**SPIKA:** Wako na Njombe pia.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante na Njombe kumbe wapo. Ombi langu, sisi Wabunge, tufanye kazi zetu za Kibunge. Tudumishe Muungano wetu, tuwe mfano bora, tuwe kioo kwa jamii yetu. Tunapoanza kulumbana humu ndani, wale tunaowaongoza watatuelewaje? Watoto wetu watatuangaliaje? Vijana wetu tunawafunza nini? Tunashangaaje sasa migomo ikitokea? Ndugu zangu nawaomba, bahati nzuri tuna Wachungaji sina uhakika wa Mashehe kama wamo humu ndani.

**WABUNGE FULANI:** Tupo.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Basi ninaomba Viongozi wa Dini tufanye kazi ya Dini na wanasiasa wafanye kazi ya Siasa. Dini iendeshwe na Viongozi wa Dini, siasa ifanywe na wanasiasa. Viongozi wa Dini, nawaomba Waislam na Wakristo waende kule kwa ndugu zangu akina Cheyo Gambushi, Kolondoto sijui wapi watu wanauana kwa nini, imani ya dini haipo. Waende wakafundishe kule ili wakashindane kuvuna waumini wa kwenye dini zetu, tusishindane kuingia katika siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya ndugu, rafiki, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, swahiba wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia hatimaye likatimia alitakalo Mwenyezi Mungu kwa binadamu anayeitwa Shibuda nikashinda kwa kishindo. Ndugu zangu, nawashukuru wote wana-CCM, Wana-CHADEMA na wananchi wote walioniunga mkono pamoja na viongozi wote wa madhehebu ya dini. *(Makofi/KIcheko)*

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za peke kwa mama Shibuda na watoto wangu wote, wajukuu zangu, wapwa zangu, mzazi mwenzangu mama Manga, viongozi wote na wanandugu wote mlioshirikiana nami. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wananchi wote wa Kata zote za Maswa Mashariki na Maswa Magharibi walioweza kutuenzi maana ulikuwa ni mchezo mkali, kati ya Yanga na Simba na Simba tukafunga magoli mawili, CHADEMA ikashinda Maswa Magharibi na Maswa Mashariki. Lakini tusibweteke kwa sababu dhamira yetu ya mashindano, ni kushindanisha nguvu za hoja na utamu wa nguvu za hoja ni ili tuweze kujenga mstakabali wa maslahi ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufalme wa Mwenyezi Mungu haupatikani kwa kukata tamaa. Kwa hiyo, nawaomba wote ambao hamkuweza kushinda katika uchaguzi wa mwaka 2010, basi mvute subira, iko siku Mwenyezi Mungu atawajalia.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa *IPP Media* pamoja na *ITV Televisheni* kwa sababu walitoa mchango mkubwa kubainisha kwamba mimi sikufutwa kugombea na hatimaye magazeti yote yaliunga mkono kuwahabarisha Watanzania kwamba Shibuda yupo katika wagombea na kwamba Mwenyezi Mungu atende haki yake kupitia wananchi wa Maswa. Nawashukuru sana, namshukuru Mwenyezi Mungu, navishukuru vyombo vya habari vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naahidi kwamba sina kisasi chochote au napenda kuwathibitishia wana-CCM ya kwamba malezi niliyotoka nayo kwa Waasisi wangu Wakuu wa CCM katika umri huu siwezi kuiga tabia fedhuli ambazo zitakuwa na kashfa za kubinafsisha nafasi za watu. Uzalendo wangu, uaminifu wangu, uadilifu wangu, daima utakuwa ni ule ule kwa sababu mimi ni mtu huria na siwezi kubinafsishwa na matakwa ya mtu binafsi ambayo hayana maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuendelea kusema kwamba tuna deni Watanzania wote ambao tuna dhamana za uongozi kujenga urithi ambao utaigwa na vizazi vya leo kwa maslahi ya vizazi vya kesho ili waweze kulinda amani na utulivu wa Watanzania. Wasukuma wana msemo wanasema ya kwamba: '*Kaya ya Vatengeke ikatengekaga'* maana yake mji wenye maadili mema hunemeka. Kwa hiyo, kila Chama kijitambue na kijifanyie uhakiki ili tuweze kusonga mbele. Nawaomba, subira ituunganishe, ufunguo wa mafanikio siyo ubinafsi bila ushirikiano. Ndio maana kuna Umoja wa Mataifa ambapo hata wale ambao hawasikilizani wako pamoja. Upo Umoja wa Mataifa ambapo hukutana na kuelezana yaliyo katika nafsi za kila mmoja. Si lazima mkikutana mahali mkubaliane lakini mkataliane kwa nguvu za hoja si kwa hulka za ubinafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli nilikuwa sehemu ya Chama cha Mapinduzi, nalichangia kwa uhuru wangu nikiwa mwana-CCM sasa niko Chama cha CHADEMA anguko langu CCM napenda kulitafsiri kwamba ni utashi wa Mwenyezi Mungu. Kuibukia kwangu Chama cha CHADEMA basi ni utashi wa Mwenyezi Mungu kwamba na CHADEMA ipate Kiongozi aliyepevuka, ngome kongwe ya kisiasa ili tuweze kushirikiana na tutatekeleza wosia wa Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiambia Serikali ya CCM na wana-CCM ya kwamba mna deni la kujenga, papatikane Mfumo wa Vyama Viwili Vikuu ambavyo vitakuwa vinazingatia uzalendo, utiifu na uaminifu kwa maslahi ya Taifa. Uingereza kuna *Labour* na *Conservative*, Marekani kuna *The Republican* na *Democratic* na nchi nyingi na sisi hapa ni nani mwenye deni hilo? Haiwezekani watu wawe wanalalamikia utovu wa nidhamu wa vijana ambao hawajatiwa unyago wa kisiasa, ni nani huyu anayepaswa kudaiwa hilo? Nawadai Serikali ya CCM, mlitelekeza wajibu wenu kwa muda mrefu na haya nimebaini baada ya kuja upande wa pili, ni nini kinahitajika, *inshallah* nitaendelea kuwashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu moja, Rais Kikwete kaleta hotuba yake hapa Bungeni ili tuichangie, tuitie ujazo akiwa na yeye ni sehemu ya Bunge lakini tunatuhumu, tunasuta, tunalaumiana tunamsaidia nini? Kesho akisema nilipeleka hotuba

Bungeni, je, Wabunge wameichangia nini, wameitia ujazo gani? Mwenzetu katuletea dira inayoonesha mustakabali wa fikra ambazo ni muhtasari siyo *book* kubwa. Kwa hiyo, tugeuke, tusiwe na tabia ya kusema kwamba ujana, unajua ujana ni papa, ujana ni harakati, uzee ni maono lakini ifikie mahali tujitambue hapa kwamba ukitaka kukomaa lazima ukae na wazee na hakuna ujana unaoweza ukashindana na ukongwe wa babu, hayo lazima tuyakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wasitara haumbuki, naomba niwatake radhi wananchi wa Zanzibar na Wabunge wote wa Zanzibar ambao walikarahishwa na tafsiri potofu, asiyejua maana haambiwi maana, dua la kuku halimpati mwewe, tulieni Muungano uko imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kutumia nafasi hii kusema kwamba tuna deni la kuhakikisha bajeti ijayo inakuwa na tafsiri sahihi ya yote ambayo yameelezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, naomba kutumia nafasi hii kuwaomba viongozi wa Serikali, mje na tafsiri sahihi na vilevile mtambue kwamba kuna viporo, Mama Spika, naomba nikokote viporo vyote, mtoto wa mwisho huyu. Kilicho mwanzo kina mwisho, kwa hiyo, naomba malumbano Bunge lijalo tuyaache.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kusema kwamba, kutokana na kifo cha Kivukoni *College,* kwa hiyo, tuna matatizo ya vijana wetu kupata wapi maadili na kuelewa elimu ya uraia. Siamini kila Mbunge ana elimu timilifu, maana ya elimu ya uraia na maana ya uzalendo kwa Taifa letu. Kwa hiyo, mkamia maji hayanywi, punguzeni harakati ili tuweze kwenda pamoja. Wajenga nchi ni wananchi na wanaobomoa nchi ni wananchi. Naomba wanaharakati, wanasiasa, tujitambulishe kwamba tuko hapa kwa maslahi ya uzalendo. Naomba mtuvumilie, tuvumiliane na kila mmoja aelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu, miaka mitano ni misumari ya jeneza la kuzika uhai wa mwanasiasa. Nawatahadharisha, wakongwe tuko hapa kwa sababu tunajua kukwepa mishale ya wawindaji halali na wawindaji haramu. Kwa hiyo, vijana kama hamtataka kujifunza, poleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kusema kwamba, kuishi kwingi kuona mengi. Dhana ya mkubwa ni kwamba Mwenyezi Mungu aliumba mzee wa leo ana jukumu la kumlea mtoto na mtoto ni mzee wa kesho kumlea mzee wa leo akiwa mkongwe. Sasa kama hampati unyago wa maadili, nchi yetu ina mmomonyoko na mporomoko wa maadili, elimu ya ma-*book* bila ujuzi na maarifa uliopevuka si maarifa timilifu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, migomo na maandamano…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Kwa heshima na taadhima, nadhani mnaniunga mkono niongezewe muda? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Kengele imelia.

**MBUNGE FULANI:** Aendelee!
**MBUNGE FULANI:** CCM! CCM!

**SPIKA:** Sipendi *microphone* zitumike kwa maneno ambayo siyo ya lazima. Sasa namwita Mkongwe mwingine, Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana lakini lazima nikubali kwamba Mheshimiwa ndugu yangu Shibuda leo alikuwa amelala sawasawa na amelitendea Bunge hili na wananchi wote ambao wamemsikiliza haki kabisa. Ahsante sana kwa hotuba yako safi na mahiri, tuendelee hivyo ndugu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii na mimi ni mara ya kwanza kuzungumza rasmi basi natumia nafasi hii kuwashukuru wapigakura wangu wa Bariadi Mashariki, kwa kufanya kazi nzuri sana ya kunipa kura zao kwa bure tu. Niko hapa, nawahakikishia kwamba nitawatendea haki kwa kuwatetea mambo yote ambayo niliwaahidi.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye *speech*. Mimi katika historia ya kuwa Mwanasiasa, nimeshakumbana na mambo mbalimbali mojawapo nililokumbana nalo ni pale ambapo Mheshimiwa Rais Kikwete alikuwa anafungua daraja la Gambasingu au Simiu ambapo mimi nilikuwa Kambi ya Upinzani na daraja liko pale. Sasa tatizo nililokuwa nalo, nimwambie kwamba hakuna daraja au nimwambie kwamba hongera sana kwa kutupa daraja hili Mheshimiwa na nakutakia mema ili ushinde uchaguzi wa 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachotaka kusema, sisi tukiwa Kambi ya Upinzani siyo kuwa haina maana kuwa hata kile unachokiona kinatendeka useme hakipo. Mimi naona hiyo dhana ni potofu kabisa na wale ambao wanatusikiliza wakiona kwamba sisi kazi yetu ni kukataa tu basi nafikiri tunajipunguzia kura. Mimi nafikiri ndio maana nimerudi hapa kwa sababu wananchi wangu wa Bariadi wanajua, palipo na mazuri nitasema, palipo na mabaya nitasema, ndio maana kwa ushirikiano huu kati yangu na Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, mimi naona nina Bariadi Mpya ambayo ina maendeleo sawasawa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachota kusema ni kwamba Mheshimiwa Rais katika kipeumbele namba 10 amezungumzia sana juu ya utawala bora, demokrasia na mambo kama hayo. Nafikiri tumpe Mheshimiwa Rais heshima ya kuweza kutuongoza katika miaka mitano ambayo wananchi wamempa. Kwa mfano, ametueleza juu ya Katiba Mpya, amesema wazi kwamba wala tu hataweka Tume lakini ataleta Muswada katika Bunge hili tuweze kutengeneza sheria ambayo itakayoongoza mchakato huo, sasa tunataka nini zaidi? Kama mtu amekuambia nakuletea sheria na wewe uitunge halafu utaratibu mwingine utafuata, mimi naona hili jambo ni zuri na Vyama vyote inafaa tumuunge

mkono ili tuweze kufika kweli miaka 50 na Katiba Mpya ambayo itakayoongoza siasa za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, vijana wangu ambao wameingia hapa, kwanza nashukuru kwamba tuna utaratibu ambao unaleta vijana katika Bunge letu ila tunawaasa kitu kimoja bado utamaduni wetu wa Kiafrika uko palepale. Wewe ukipata cheo cha kuwa Mbunge, haikupi kibali cha kumtukana mtu ambaye ni sawasawa na baba yako. Mimi nina hakika hata wale ambao wanawasikiliza, wamechaguliwa hapa na vijana wenzao, wamechaguliwa na mama zao, wamechaguliwa hapa na baba zao, wakisikia wanakiuka huu utaratibu wa Kiafrika ambao mtu aliyekutangulia umpe shikamoo, umpe heshima hawatawapa tena kura. Mimi naona njia ya kuhakikisha kwamba wanaendelea vizuri, tufanye siasa lakini tubakie kuwa watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimekaa hapa karibu miaka nane na sasa wamenipa kipindi kingine, hapa ni mahali pazuri, kwa nini utengeneze maadui? *Smile*, huwezi ukazungumza na kila mmoja, ufurahi, ukitoka pale nje, *come and have a cup of coffee*, twende tukanywe pamoja na mambo mengine. Wengine wameoana hapa hapa na wengine wameolewa humu humu. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kupata *blood pressure*, huyu ni CCM, huyu ni *UDP*, huyu ni kitu gani hakuna. Mimi naona siasa ni kitu kimoja, wote tushindane kwa hoja.

Mheshimiwa Spika, leo nimemshukuru sana mkubwa wetu wa Kambi ya Upinzani angalau ameleta moyo wa *reconciliation* kwamba tufanye kazi pamoja, huu ndio moyo ambao tumeujenga miaka mitano iliyopita na nashauri moyo huu uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nataka kumwambia, utupe na sisi ambao tumetangulia heshima kidogo. Mambo ya Katiba siyo Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA, tumekuwa tunazungumza mambo ya Katiba tangu tumeingia katika Vyama Vingi. Tumekuwa na Kamati ya sisi wote, UDETA na nini tunazungumzia mambo ya Katiba, rafiki zangu wa *CUF* mpaka wamepeleka na Katiba Mpya, kwa hiyo, tuheshimiane suala hili ni letu sote.

Mheshimiwa Spika, kwa wananchi wangu wa Bariadi, nimewaahidi nitaendelea kuwatetea katika kuhakikisha kwamba kila mmoja anapimiwa ardhi yake na anapata kipande chake na hati yake. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri anayehusika, mambo ambayo yaliyofanywa na Mheshimiwa Chiligati yalikuwa safi sana mpaka aka-*introduce* jambo moja, ime-*perpetuate* yaani unapopewa ardhi yako ni yako milele na milele, jambo hili liendelezwe. Mimi nashauri Mawaziri siyo kila Waziri anayekuja atengeneze mambo yake tofauti. Hii imetokea katika elimu, kila Waziri anayekuja anatengeneza mambo yake, mwingine anageuza tena, mwingine anaturudisha nyuma, mimi naona tujenge juu ya yale ambayo yametengenezwa. Kwa jambo hili la ardhi, naomba tuendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wakulima wangu wa pamba, kila siku nawaambia tunataka kumaliza umaskini, njia ya kumaliza umaskini siyo kuisubiri Serikali, uwe na nia ya kutengeneza milioni kila Kaya. Njia ya kutengeneza milioni kila Kaya, lima kilo

1000 na mimi nitasukuma Serikali bei iwe angalau ya 1000 kwa kilo, 1000 kwa 1000 ni milioni. Ndio njia ya kumaliza umaskini. Kwa hiyo, ndugu zangu wanaofuga mifugo, mimi naiomba Serikali iondoe *mindset* iliyopo wafugaji hiyo ndio biashara yao, *it is their business*. Kama tunavyosaidia wakulima, tuendelee hivyo hivyo kuwasaidia wafugaji kama inabidi tuchimbe visima vingi sana Longido na sehemu zingine za wafugaji tufanye hivyo. Ni aibu kwa nchi hii kuona mifugo mamilioni na mamilioni inakufa kwa sababu hakuna maji na chini ya ardhi kuna maji. Tutafute masoko, tuhakikishe machinjio tunayatengeneza, biashara ipo, kuna 40,000 *tones* ambazo zinahitajika Congo na sehemu nyingine, uwezo tunao, tunaweza kumaliza umaskini wa wananchi wetu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani muda umefika, hatuna namna ya kuendelea, mimi mngeniuliza, ningewaambia tunakwenda vizuri sana. Napenda mtu awe *free,* mwenzake akisema asichukulie kama ni ugomvi. Muwe *free*, hata mimi mkini-*provoke*, hamuwezi kuni-*provoke* kwa sababu najua ndio mchezo wa hapa. Kwa hiyo, yule nitakayemwambia ukae chini au nini, ni katika mchezo wa hapa siyo kwamba nina hasira au nina chuki na mtu yeyote. Kwa hiyo, naomba tuendelee hivi hivi kwa upendo kabisa, tusiwe na hila na mtu yeyote kichwani kwa sababu mkifanya hivyo hamtafanya kazi mliyotumwa kufanya hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache tu hapa, kwanza, nina tangazo la Katibu wa CHADEMA, Mheshimiwa John Mnyika, anaomba niwatangazie Wabunge wa Chama hicho kwamba kutakuwa kikao cha Kamati ya Wabunge wa CHADEMA mara baada ya kikao cha Bunge kuahirishwa usiku huu. Kikao hicho kitafanyika ukumbi namba 231.

Mheshimiwa Lediana Mg'ong'o, yeye ni Katibu wa Wabunge Wanawake wa CCM, anaomba niwatangazie Wabunge Wanawake wa CCM kuwa kutakuwa na kikao ukumbi wa Msekwa, saa tatu asubuhi kesho, anaomba wote muhudhurie. Lakini nimetangaza asubuhi kutakuwa na kikao cha Wabunge Wanawake wote katika ukumbi huo huo, kwa hiyo, nyie CCM msitubane pale muwahi.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Januari Makamba, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kuwa Kamati itafanya ziara katika Bwawa la Mtera, siku ya Jumapili tarehe 13 Februari. Wajumbe ambao hawataweza kushiriki, wawasiliane na Katibu wa Kamati mapema iwezekanavyo. Msafara wa kuelekea Mtera utaondoka hapa Ofisi ya Bunge saa moja kamili asubuhi bila kuchelewa. Kwa hiyo, wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini mna safari, muwasiliane na Katibu wenu.

Sina tangazo lingine, nawashukuru sana kwa kazi tuliyoifanya wiki hii, ilikuwa ni kazi nzuri sana. Sisi hatuna kazi nyingine kama Wabunge isipokuwa wale Wabunge Wanawake ndio watakuwa na kazi ya uchaguzi wa viongozi wa Chama chao cha Wanawake Bungeni. Yule mwanamke atakayechaguliwa katika mkutano wa kesho, ndiye anakuwa Mbunge wa *SADC*. Kwa hiyo, ni kikao muhimu kwa wanawake na pia ni kikao cha kwanza kwa wanawake kukutana, hatujawahi kukutana toka tumechaguliwa. Kwa

hiyo, naomba kila mmoja ahudhurie, kila mtu amwambie na mwenzake ambaye hajasikia tangazo hili.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba niwashukuru, niwatakie jioni njema na *weekend* njema, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu Saa Tatu Asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.42 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 14 Februari, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*